ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI
ZANZIBAR
MHE. PANDU AMEIR KIFICHO - SPIKA

1.Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	MBM/Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa na Rais.
2.Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Dimani.
3.Mhe. Omar Yussuf Mzee	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo/ Kuteuliwa na Rais.
4.Mhe. Haji Omar Kheri	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora/Jimbo la Tumbatu.
5.Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais/Kuteuliwa.
6.Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa.
7.Mhe. Abubakar Khamis Bakary	MBM/Waziri wa Katiba na Sheria/Jimbo la Mgogoni.
8.Mhe. Rashid Seif Suleiman	MBM/Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Ziwani.
9.Mhe. Ali Juma Shamuhuna	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Donge.
10.Mhe. Juma Duni Haji	MBM/Waziri wa Afya/Kuteuliwa.
11.Mhe. Zainab Omar Mohammed	MBM/Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto/Kuteuliwa.
12.Mhe. Said Ali Mbarouk	MBM/Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo/Jimbo la Gando.
13.Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban	MBM/Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Kuteuliwa.
14.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	MBM/Waziri wa Kilimo na Maliasili/Jimbo la Jang'ombe
15.Mhe. Nassor Ahmed Mazrui	MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Mtoni
16.Mhe. Abdillah Jihad Hassan	MBM/Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Magogoni.
17.Mhe. Haroun Ali Suleiman	MBM/Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika/Jimbo la Makunduchi.
18. Mhe. Shawana Bukheti Hassan	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/ Jimbo la Dole.
19. Mhe. Haji Faki Shaali	MBM/ Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Mkanyageni.
20.Mhe. Machano Othman Said	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Chumbuni.

21.Mhe. Othman Masoud Othman	Mwanasheria Mkuu.
22.Mhe. Issa Haji Ussi	Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Chwaka.
23.Mhe. Zahra Ali Hamad	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Nafasi za Wanawake.
24.Mhe. Dr. Sira Ubwa Mamboya	Naibu Waziri wa Afya/Kuteuliwa na Rais.
25.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	Naibu Waziri wa Habari,Utamaduni,Utalii na Michezo/ Nafasi za Wanawake.
26.Mhe. Haji Mwadini Makame	Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Jimbo la Nungwi.
27.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi	Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Fuoni.
28.Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak	Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili/Nafasi za Wanawake
29. Mhe. Mohammed Said Mohammed	Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi/ Jimbo la Mpendae.
30.Mhe. Abdalla Juma Abdalla	Jimbo la Chonga
31.Mhe. Abdalla Moh'd Ali	Jimbo la Mkoani
32. Mhe. Ali Mzee Ali	Kuteuliwa
33.Mhe. Abdi Mosi Kombo	Jimbo la Matemwe
34.Mhe. Ali Abdalla Ali	Jimbo la Mfenesini
35. Mhe. Ali Salum Haji	Jimbo la Kwahani
36.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	Nafasi za Wanawake
37. Mhe. Asaa Othman Hamad	Jimbo la Wete
38.Mhe. Asha Abdu Haji	Nafasi za Wanawake
39.Mhe. Asha Bakari Makame	Nafasi za Wanawake
40.Mhe. Ashura Sharif Ali	Nafasi za Wanawake
41.Mhe. Bikame Yussuf Hamad	Nafasi za Wanawake
42.Mhe. Farida Amour Mohammed	Nafasi za Wanawake
43.Mhe. Fatma Mbarouk Said	Jimbo la Amani
44.Mhe. Hamad Masoud Hamad	Jimbo la Ole
45.Mhe. Hamza Hassan Juma	Jimbo la Kwamtipura
46.Mhe. Hassan Hamad Omar	Jimbo la Kojani
47.Mhe. Hija Hassan Hija	Jimbo la Kiwani
48.Mhe. Hussein Ibrahim Makungu	Jimbo la Bububu

49.Mhe. Ismail Jussa Ladhu	Jimbo la Mji Mkongwe
50.Mhe. Jaku Hashim Ayoub	Jimbo la Muyuni
51.Mhe. Kazija Khamis Kona	Nafasi za Wanawake
52.Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa	Jimbo la Kikwajuni
53.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk	Jimbo la Kitope
54.Mhe. Mansoor Yussuf Himid	Jimbo la Kiembesamaki
55.Mhe. Marina Joel Thomas	Kateuliwa na Rais
56.Mhe. Mbarouk Wadi Mussa	Jimbo la Mkwajuni
57.Mhe. Mgeni Hassan Juma	Nafasi za Wanawake
58.Mhe. Mlinde Mbarouk Juma	Jimbo la Bumbwini
59.Mhe. Mohammed Haji Khalid	Jimbo la Mtambile
60.Mhe. Mohammed Mbwana Hamad	Jimbo la Chambani
61.Mhe. Mussa Ali Hassan	Jimbo la Koani
62.Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali	Jimbo la Uzini
63.Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa	Nafasi za Wanawake
64.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi	Nafasi za Wanawake
65.Mhe. Nassor Salim Ali	Jimbo la Rahaleo
66.Mhe. Omar Ali Shehe	Jimbo la Chake-Chake
67.Mhe. Panya Ali Abdalla	Nafasi za Wanawake
68.Mhe. Raya Suleiman Hamad	Nafasi za Wanawake
69.Mhe. Rufai Said Rufai	Jimbo la Tumbe
70.Mhe. Saleh Nassor Juma	Jimbo la Wawi
71.Mhe. Salim Abdalla Hamad	Jimbo la Mtambwe
72.Mhe. Salma Mohammed Ali	Nafasi za Wanawake
73.Mhe. Salma Mussa Bilali	Nafasi za Wanawake
74.Mhe. Salmin Awadh Salmin	Jimbo la Magomeni
75.Mhe. Shadya Mohamed Suleiman	Nafasi za Wanawake
76.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha	Jimbo la Mwanakwerekwe
77.Mhe. Subeit Khamis Faki	Jimbo la Micheweni

78.Mhe. Suleiman Hemed Khamis Jimbo la Konde
79.Mhe. Ussi Jecha Simai Jimbo la Chaani
80.Mhe. Viwe Khamis Abdalla Nafasi za Wanawake
81.Mhe. Wanu Hafidh Ameir Nafasi za Wanawake

Ndugu Yahya Khamis Hamad Katibu wa Baraza la Wawakilishi

Kikao cha Nne – Tarehe 8 Aprili, 2013

(Kikao kilianza saa 3.00 asubuhi)

DUA

Mhe. Spika (Pandu Ameir Kificho) alisoma dua

HATI ZA KUWASILISHA BARAZANI

Mwanasheria Mkuu: Mhe. Spika, naomba kuwasilisha mezani mswada wa Sheria kurekebisha Sheria mbali mbali na mambo mengine yanayohusiana na hayo. Naomba kuwasilisha.

Mhe. Ali Abdalla Ali (Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala): Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kuwasilisha mezani hotuba ya maoni ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala kuhusu Mswada wa Kurekebisha Sheria mbali mbali na mambo yanayohusiana na hayo. Naomba kuwasilisha.

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 41

Elimu ya Utunzaji wa Mazingira

Mhe. Saleh Nassor Juma (Kny: Mhe. Salim Abdalla Hamad) – Aliuliza:
Zanzibar ni nchi ambayo kila uchao ardhi yake huwa inapungua kutokana na kuongezeka kwa maji ya Bahari, vile vile rutuba yake inapungua kutokana na ukataji ovyo wa miti na utiaji wa mashamba moto katika siku za kilimo. Kutokana na kuwa kila mwaka idadi ya watu huwa inaongezeka, jambo ambalo husababisha hata zile sehemu zenye rutuba pia kutumika kwa majenzi.

(a) Ni kwa namna gani Wizara imejipanga katika kupambana na uharibifu huu wa mazingira, ili wananchi na hasa wakulima waweze kutumia ardhi hii ipasavyo.
(b) Ni kwa kiasi gani, Wizara yako inashirikiana na Wizara nyengine husika kuona kuwa zinatoa elimu ya kupambana na uharibifu wa mazingira.
(c) Ni kwa kiasi gani mafanikio yamepatikana, katika utoaji wa elimu hiyo.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais – Alijibu**:-**

Mhe. Spika, kabla ya kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake namba 41 naomba kutoa maelezo yafuatayo naomba kwa ufupi sana nitoe maelezo yafuatavyo:-
Dunia hivi sasa inaendelea kukabiliwa na athari za mabadiliko ya tabianchi zikiwemo za kuongezeka kwa kina cha maji ya bahari. Uongezekaji huo unaathiri zaidi nchi za visiwa ikiwemo Zanzíbar ambayo pamoja na mambo mengine husababisha mmong'onyoko wa fukwe hali inayopelekea kuathiri pia maeneo ya kilimo kwa kuingia maji ya chumvi / bahari na hata kuathiri makaazi ya watu na maeneo ya historia.

Ukataji wa miti ovyo na utiaji moto ovyo kwenye mashamba ni sababu nyengine zinzopelekea uharibifu wa mazingira ya visiwa vyetu.
Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo sasa kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake namba 41 lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

a) Katika kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi ikiwemo kuingia maji ya chumvi kwenye mashamba ya wakulima, Ofisi ya Makamu wa Kwanza imekuwa ikiwashajiisha na kuwaelimisha wadau na wananchi wa maeneo yaliyoathiriwa kupanda miti kwa wingi na ikibidi kujenga matuta ili kupunguza athari hizo na kupata nafasi ya kuendelea kuyatumia maeneo hayo kwa shughuli za kilimo. Mfano wa maeneo ambayo tayari yamejengwa matuta kwa ajili ya kuzuwia maji ya chumvi ni pamoja na Koowe, Ukele, Tumbe na kwa Jibwa iliopo Kengeja. Sambamba na hili, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais imekusanya taarifa za maeneo yote yanayoingia maji ya chumvi hapa Zanzíbar na imebaini kuwa yapo maeneo 148 Unguja na Pemba (123 Pemba na 25 yapo Unguja). Maeneo haya ni yale ambayo yameingiliwa na maji ya chumvi. Ofisi hivi sasa imeanza mchakato wa kutayarisha mapendekezo ya mradi kwa baadhi ya maeneo hayo ili hatua zinazostahiki ziweze zichukuliwe.

   Aidha, kwa kuwa tatizo la mabadiliko ya tabianchi ni kubwa katika visiwa vyetu, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais imejipanga kutayarisha mkakati wa kitaifa wa kujihami na kujilinda na athari za athari hizo. Ofisi hii hivi sasa ipo katika hatua za mwisho za kuajiri Mshauri Elekezi wa kufanya kazi hiyo kwa kushirikiana na wadau wote husika. Mkakati huo unatarajia kuainisha vipaumbele vya hatua zinazofaa kuchukuliwa za kujilinda na kujihami na athari za mabadiliko ya tabianchi Zanzíbar.

b) Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais kwa kiasi kikubwa inashirikiana na taasisi nyengine zikiwemo Wizara Kilimo na Maliasili, Wizara ya Mifugo na Uvuvi na Asasi za Kiraia katika kutoa elimu kwa lengo la kupambana na uharibifu wa matumbawe, ukataji wa miti ovyo na uchimbaji wa mchanga usiofuata taratibu zilizowekwa. Hivi karibuni Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais imeshirikiana na Jumuiya ya Uhifadhi wa Mazingira na Maendeleo ya Jamii (CODECOZ) katika kutayarisha vitini vya muongozo wa mafunzo wa Sera, Sheria na kanuni za mazingira kwa wanajamii na Asasi za Kiraia. Muongozo huo hivi sasa umeshafundishwa kwa wakufunzi 75 kutoka Wilaya ya Mkoani, Micheweni, Kaskazini A na B na mafunzo yanaendelea. Aidha ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais hivi sasa inatayarisha Mkakati wa Mawasiliano utakaotumika katika kuelimisha jamii juu ya hifadhi ya mazingira nchini.

c) Mhe. Spika, mafanikio ya utoaji elimu hiyo ni makubwa kwani jamii imekuwa na mwamko mkubwa wa kimazingira ambapo Jumuiya za Kiraia, Kamati na vikundi vingi vya jamii vya kulinda na kuhifadhi mazingira vimeanzishwa Unguja na Pemba. Aidha juhudi za utoaji wa elimu hivi karibuni zimepelekea kuanzishwa kwa mtandao wa mazingira Zanzíbar ambao unaundwa na Jumuiya kumi na moja (11) za mazingira ziliopo maeneo mbali mbali ya Zanzíbar. Mafanikio hayo ya elimu ya mazingira pia yamepelekea kuundwa kwa Kamati za Mazingira na Uvuvi katika shehia nyingi za Unguja na Pemba na hushirikiana na Serikali katika doria za baharini ili kupambana na uvuvi haramu.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Spika, kwanza nitoe shukurani kwa Mhe. Saleh kwa kuniulizia swali langu lilivyo na pili kupata majibu hivyo nilivyokusudia.

Lakini hata hivyo Mhe. Spika, nina swali moja tu la nyongeza lenye vifungu (a) na (b) kama hivi ifuatavyo.

a) Kwa sababu uharibifu wa mazingira hautokani na kuongezeka kwa kina cha maji tu na baadhi ya sehemu zikaingia chumvi na nyengine kuporomoka kwa sababu hiyo, pia inatokana na kazi kubwa inayofanywa katika nchi zilizoendelea ambazo ni nchi zenye viwanda vingi sana hivyo husababisha kuingiza hewa isiyotakiwa kwa wingi, hewa mkaa katika ulimwengu na sisi pia ni waathirika wa suala hilo. Mhe. Spika, kwa sababu ninasikia nchi hizi zilizoendelea ni ikiwa ndio wahusika wakuu wa kuleta uharibifu wa mazingira katika hali niliyoeleza wanatoa misaada kusaidia nchi zile zilizoathirika nchi zinazoendelea kama yetu. Jee, kuna msaada wowote Zanzibar imeupata kupambana na uharibifu huu ambao kwa makusudi unafanywa na nchi zilizoendelea.

b) Katika Jimbo langu la Mtambwe kuna kisiwa chenye historia kubwa sana, Kisiwa cha Mtambwe Mkuu na kisiwa kinachoathirika sana na mmomonyoko wa ardhi kutokana na chumvi inavyoingia kwa wingi na hali ya wananchi ilivyo ni ngumu hawana uwezo wa kuweza kukihami kisiwa kile kwa sababu sehemu nyengine hazihitaji kupandwa miti lakini zinahitaji hata kujengwa ukuta. Jee, Mhe. Waziri kwa umuhimu wa kisiwa kile ana mpango gani wa kusaidia kuona kuwa hakiendelei kuchukuliwa na ardhi kutokana na hali ambayo hivi sasa ni ya kutisha.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa ruhusa yako tena naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mhe. Mwakilishi kama hivi ifuatavyo.
Ni kweli uharibifu wa mazingira umechangia kiasi kikubwa na nchi zilizoendelea zenye viwanda vikubwa ambazo zilizosababisha mkusanyiko wa hewa ambayo tunaita gesijoto au hewa chafu katika dunia, na imekubalika kwamba nchi hizi basi kwa sababu ndio zilizokuwa zimechangia mno katika uharibifu wa mazingira ziweze kutayarisha mfuko wa fedha kwa ajili ya kuzisaidia nchi zinazoendelea nchi ndogo ndogo kukabiliana na mabadiliko ya tabia ya nchi.

Upo mfuko ambao umeanzishwa ni mfuko wa nchi maskini duniani au wanaita *Least Development Countries Fund*, ni mfuko ambao unachangiwa na nchi zilizoendelea ili fedha hizi zipewe nchi maskini katika kukabiliana na mabadiliko ya tabia ya nchi.

Mhe. Spika, tayari Zanzibar imefaidika na fedha hizi. Kipindi kilichopita zilipatikana fedha ambazo zimesaidia kuchimba kisima kwa ajili ya kuwapatia maji safi wananchi wa Nungwi. Shughuli hiyo karibuni inakaribia kumazilika na hivi karibuni wananchi wa Nungwi ambao wanaathirika mno na visima vyao vingi kupata maji ya chumvi watafaidika kwa kupata maji matamu.

Lakini kuna ahadi pia kwa Zanzibar kupata jumla shilingi milioni mia tano na arobaini na sita, laki nane na kumi na tano elfu, hizi ziliahidiwa kutokana mwaka jana Mhe. Spika, katika mradi wa miaka mitano wa *Global Environmental Fund*, fedha hizi zinazopitia mfuko wa nchi maskini ili zikabidhiwe Zanzibar kwa ajili ya kupambana na mazingira.

Nasikitika kusema kwamba ule mchakato wake umekuwa mrefu mno na hadi hii leo fedha hii bado haijapatikana. Lakini kwa kweli zipo jitihada hizo na mifuko mbali mbali ipo kwa ajili ya kusaidia kuathirika kwa mazingira.

Jibu la pili, Mhe. Spika, mimi binafsi nilipata fursa ya kwenda kutembelea kisiwa hiki chenye historia kubwa cha Mtambwe Mkuu na kwa kweli mimi na watendaji wangu, nafikiri na siku hiyo Mhe. Mwakilishi alikuwepo kwenye ziara hiyo na wananchi wa kisiwa hicho tuliweza kutembelea kisiwa kile tutakizunguka chote, na kwa kweli athari za mabadiliko ya tabia ya nchi zimepiga sana katika kisiwa kile cha Mtambwe Mkuu.

Kuna ufumbuzi wa moja kwa moja ambao tulitoa ushauri na kwa bahati wananchi wa sehemu ile tayari wana vikundi vya mazingira na wameanza kufanya kazi hivyo nzuri. Hatua ya kwanza ni kuweza kupanda miti.

Maji haya yalisogea katika kisiwa kutokana na kukatwa kwa wingi sana miti aina ya mikoko ambayo wananchi waliitumia katika shughuli zao za maisha hatimaye maji ya baharí nayo yamepanda juu na yameanza kula sehemu ya kisiwa.

Ushauri anaoutoa kwamba jee afisi yangu itaweza kujenga ukuta kwa ajili ya kukabiliana na mabadiliko haya ya tabia ya nchi, naomba Mhe. Mwakilishi nimuarifu kwamba siwezi kuchukua ahadi hiyo hivi sasa, kama nilivyomueleza kuwa tumefanya utafiti wa maeneo haya ambayo yanaharibiwa na mazingira ikiwemo kisiwa hiki cha Mtambwe Mkuu ni mengi; maeneo karibu 25. Afisi yangu inaandaa mpango mkakati na kuweza kuainisha vipa umbele na njia ambazo tunaweza kuzitumia katika kukabiliana na mabadiliko hayo ya tabia ya nchi.

Tunachoweza kumshauri sana Mhe. Mwakilishi kwamba aendelee kuwa na wananchi wake pamoja na afisi yangu kuhakikisha kwamba hii hatua ya kwanza ambayo haihitaji fedha nyingi ya kupanda miti, tunapanda miti kiasi tunachoweza ili hatimaye iweze kupunguza athari za mabadiliko ya tabia ya nchi.

Mhe. Panya Ali Abdalla: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kunipa fursa hii kuuliza swali moja dogo la nyongeza. Kwa kuwa serikali inafanya bidii kubwa ya kutunga sheria ili iweze kuendesha mambo yake vizuri na hivi sasa uharibifu wa mazingira unaonekana kupamba moto hasa kwa ukataji wa miti na uchomaji moto mashamba.

Je, serikali inachukua hatua gani kutumia sheria ya uharibifu wa mazingira ili kudhibiti mazingira yawe salama lakini pia kuweza kuwachukulia hatua kali ambao wanaharibu mazingira yetu.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa ruhusa yako napenda kumjibu swali la nyongeza la Mhe. Mwakilishi kama ifuatavyo.

Ni kweli kuna tatizo kubwa la wananchi wetu kutokuheshimu na kufuata sheria zilizopo za uhifadhi wa mazingira. Ofisi yetu imeliona hilo na katika jibu langu mama nimeeleza kwamba tumetengeneza vitini; vitini ni muongozo unaoelezea será, sheria na kanuni mbali mbali zinazohusiana na uhifadhi wa mazingira na tunazipeleka kwa wananchi katika wilaya zote.

Madhumuni yetu ni kwamba wananchi wazifahamu kwa sababu wengi wao ijapokuwa kama hufahamu sheria ukivunja sheria haitokuwa sababu ya wewe kukulinda, lakini tumepata malalamiko kwamba wengi walikuwa wanayafanya yale wanayoyafanya kwamba kisingizio hawazifahamu sheria au kanuni za uhifadhi wa mazingira.

Ofisi yetu imejipanga imetoa taaluma ya kutosha na tunaomba sana kupitia vyombo vya dola ambao wao ndio watekelezaji hasa wa kusimamia kuona kwamba sheria hii inatekelezwa, tusaidiane ili sheria hizi na kanuni za uhifadhi wa mazingira ziweze kufuatwa.

Nam. 26

Kuondoshwa Bandari ya Forodha Mchanga

Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Aliuliza:
Serikali yetu imekuwa ikitegemea kodi katika kuendesha shughuli zake za kuhudumia wananchi wake, kodi hii imekuwa ikikusanywa kutoka vyano mbali mbali nchini ikiwemo kodi za bandari na kadhalika. Hivi karibuni serikali yetu imekuwa na mpango wa kuondoa bandari Forodha Mchanga ambayo imekuwa ni chanzo kizuri cha mapato ya serikali kutoka kwa vyomo vinavyotumia bandari hiyo.

a) Je, kabla ya kuondoshwa bandari hiyho, serikali imeangalia athari za kiuchumi zitakazopatikana ikiwemo kupoteza kodi kubwa inayolipwa na wenye vyombo wanaotumia bandari hiyo.

b) Jee, ni zipi faida na hasara ambazo serikali imeziona kwa kuhamisha bandari hiyo kutoka Forodhani na kuipelekea pahala pengine.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano – Alijibu:
Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 26 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo

Kabla Mhe. Spika, kabla ya kumjibu Mhe.Mwakilishi naomba nichukue nafasi hii kumkumbusha Mhe. Mwakilishi kwamba eneo la Forodha Mchanga sio bandari rasmi kwa mujibu wa kuanzishwa Shirika la Bandari. Hata hivyo ufukwe huo hutumika kwa dharura kwa ajili ya kushusha na kupakia mizigo pamoja na magari katika vyombo vya *landcraft* kutokana na ufinyu unapotokea katika nafasi za kufuga gati kwenye eneo la bandari ya Malindi.

Wakati wa dharura kama hizo, taasisi za kibandari zinazohusika na ukusanyaji wa mapato pamoja na watu wa Forodha hupelekwa eneo hilo kwa ajili ya kusimamia na kuhakikisha mapato yanayostahiki yanakusanywa.

Mhe. Spika, la kwanza serikali imelizingatia suala hilo na kuona kwamba hakutakuwa na athari za kiuchumi zitakazotokana na kuhamishwa vyombo hivyo kutoka Forodha Mchanga, kwani vyombo hivyo vitahudumiwa katika bandari kuu ya Malindi ambapo kuna usalama zaidi na udhibiti mkubwa wa mapato ya serikali.

Eneo lililotengwa kutoa huduma hiyo ni kwenye *ramp* mpya ambayo kubwa na itakidhi haja hiyo.

Swali la pili, Mhe. Spika, hakuna hasara yoyote inayotokana na kuhamishwa vyombo hivyo kutoka Forodha Mchanga isipokuwa faida zake ambazo ni nyingi ikiwemo usalama wa nchi, udhibiti wa mapato ya serikali, kuondoa msongamano wa magari katika mabarabara ya Mji Mkongwe, uhifadhi na uendelezaji wa Mji Mkongwe kutokana na uzito wa magari yanayosafirishwa kupitia eneo hilo, kuepuka uchafuzi wa mazingira na mengineyo.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu ya Mhe. Naibu Waziri aliyotoa hivi sasa ya kutokuridhisha swali la msingi.
Kwa kuwa sheria za uwekezaji zinazuia mita 30 kutoka ufukwe wa baharí, leo inakuwaje mikahawa inaruhusiwa kupanga viti hadi eneo la baharí.

Swali la pili, kwa kuwa bandari hiyo ni asili na Mji Mkongwe ni wa asili na ile sehemu imekuwa ni kivutio cha watalii, huoni ni kuvuka utaratibu na watalii tunawategemea kwa kipindi hiki na vile vile kajibu swali hilo kuwa kuna magari yamezuiwa Mji Mkongwe, hivi sasa kuna magari yanapita pale zaidi ya tani 16 na pana askari na wananchi wenye haki ya kutumia njia hawapati na magari yao hivi yanapita.

Na baada ya kikao hiki kama utakuwa tayari nitakuwa tayari kwenda kukuthibitishia.

Mhe. Spika: Naona swali la mchanganyiko mkubwa kwa sababu lina mambo ya uhifadhi wa Mji Mkongwe lakini pale lilikuwa ni suala la bandari. Hebu litafutie utaratibu wa kuliulizia swali la msingi.

Mhe. Ali Abdalla Ali: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa fursa ya kuweza kuuliza swali la nyongeza.

Mhe. Naibu Waziri alipokuwa anajibu alisema kwamba bandari ya Malindi hivi sasa imekuwa finyu, huko nyuma nilisikia kulikuwa kuna utaratibu wa kujengwa bandari kubwa na ya kileo eneo la Mpigaduri ili tukatenganisha mizigo mbali na abira mbali. Jee, azma hiyo ipo na kama ipo imefikia hatua gani.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe.Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Mhe. Spika, azma ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kujenga bandari mpya ya Mpigaduri ipo na inatekelezwa na hatua tuliyofikia ni nzuri.

Nam. 4

Msaada wa Serikali kwa Msanii Mkongwe Bi.Kidude

Mhe. Saleh Nassor Juma – Aliuliza:
Kwa kuwa msani nguli katika tasnia ya muziki wa taarab, Zanzibar, Tanzania na Afrika Mashariki na Kati, *Sayyidati* Fatma binti Baraka (Bi. Kidude) ameipeperusha vyema bendera ya nchi yetu, tangu zamani na hadi sasa. Na kwa kuwa siku za karibuni imepatikana taarifa ya ugonjwa mkubwa uliomkabili msanii huyo nguli.

a) Je, serikali inayo taarifa hiyo.

b) Kama serikali inayo taarifa ni kwa kiasi gani imesaidia katika matibabu ya msanii huyo.

c) Kama serikali inayo taarifa na haijasaidia kumtibu si itakuwa sababu ya kuwarejesha nyuma hawa wasanii chipukizi wakiwemo wa kizazi kipya (*Zenj Flava* na *Bongo Flava*).

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo – Alijibu
Nakushukuru Mhe. Spika, kwa naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 4 kama inavyofuata.

Mhe. Spika, wizara yangu inayo taarifa juu ya hali ya afya ya Bi. Fatma (Bi. Kidude) kuwa sio nzuri.

Swali la pili, mara baada ya kupata taarifa ya ugonjwa wa msanii huyo wizara yangu ilifuatilia kwa karibu mipango ya tiba iliyopangwa na familia yake. Iliyobainika ni kwamba tiba yake imepangwa isimamiwe na familia yake na uongozi wa Sauti za Busara taasisi aliyokuwa akiitumikia kabla ya kupata ugonjwa na kwamba tayari wameshafanya mipango ya kumpeleka Dar es Salaam kwa matibabu. Hivi sasa msanii huyo yupo nyumbani akiwa chini ya uangalizi wa familia yake.

Swali la tatu, viongozi wa wizara mara mbili walipokwenda kumjua hali msanii huyo waliitaka familia yake kuwasiliana na uongozi wa Kamisheni ya Utamaduni na Michezo na wizara yangu juu ya msaada wowote unaohitajika katika tiba yake.

Mhe. Spika, nichukue fursa hii kumuomba Mwenyezi Mungu ampe nafuu haraka Bi. Kidude apone ugonjwa unaomkabili ili wapenzi wa nyimbo zake akiwemo Mhe. Saleh Nassor Juma wa Jimbo la Wawi waendelee kuburudika na matumbuizo yake.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba niulize swali moja dogo la nyongeza kama ifuatavyo.

Kwa kuwa *Sayydat* Fatma binti Baraka maarufu Bi. Kidude sio alitunga na kughani nyimbo zake mwenyewe, lakini vile vile alifanya ikirari kwa maana ya kukariri baadhi ya nyimbo za wasanii wengine akina Mwasiti binti Saad, Siti binti Bunia na kadhalika na hata wale wenye asili ya Kiajemi Farid Al Atrash na Ummul Kuluthum jambo ambalo sio tu liliwaburudisha Wazanzibari lakini vile vile walifurahia mno.

Mhe. Spika, kwa kuwa Bi. Kidude serikali imekiri matibabu yake wameiachia taasisi aliyokuwa akiitumikia Sauti za Busara, lakini vile vile huyu binti aliipeperusha vyema bendera ya nchi hii nje na ndani ya nchi. Leo kuiachia taasisi, serikali ikawa inafumba macho na kwa kuwa Bi. Kidude kupitia vyombo vya habari ikiwemo ITV tunamuona anaomba misaada hata kwa watu binafsi.

Sasa Mhe. Spika, kuendelea kumuachia Bi Kidude akipata shida anazopata si kuwavunja moyo wasanii wengine hata wale wenye fani ya maigizo akina Halikuniki, Makombora pamoja na Bi. Tele.

Swali la pili kumuachia Bi. Kidude amalizike kama tawi linalokauka katika mti wake na kuanguka chini, si kuvunja moyo hata hawa wasanii wa *Zenji Fleva* na *Bongo Fleva*.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Spika, ninakushukuru naomba nimjibu Mhe. Mwakilishi swali lake refu linalohusiana na suala la msanii wetu maarufu.

Ni kweli Mhe. Spika, kwamba kama nilivyosema awali kuwa hali ya Bi. Kidude si nzuri na sisi wizara tulipopata taarifa, sio kwamba tulidharau au kupuuza lakini tulikwenda na tumekuwa tukenda. Lakini iliyobainika ni kwamba familia yake yenyewe imetaka mambo haya, tiba yake ishughulikiwe na wao.

Sasa mgonjwa yeyote anayeumwa, jukumu la kwanza ni watu wake. Kwa hivyo anapozungumza mtu wake, mwanawe, mtu wake wa karibu kwamba mgonjwa wetu tuachie, wewe huna nguvu ya kumchukua.

Sasa tulikwenda kwa mashirikiano na bado ninavyokwambia kwamba tunaendelea kwenda kumjulia na msaada wowote ambao unaohitajika, sisi wizara kwa niaba ya serikali tupo karibu kuitoa.

Lakini pia nikubali kwamba Mhe. Spika, kuna tatizo hilo tumeliona kama miezi mitatu iliyopita nimekaa na *veteran* wa michezo mbali mbali waliochezea na kuipa sifa Zanzibar kwa miaka mingi ambao hali zao sio nzuri na wanahitaji msaada mkubwa. Tulichokubaliana pale wizarani ni kwamba katika bajeti inayokuja tutaweka kifungu maalum cha kuwaenzi wasanii wetu wa zamani.

Kwa hivyo, tutakapokileta Mhe. Spika, naomba Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi akiwemo Mhe. Saleh Nassor Juma watupitishie kifungu hicho, ili tuwe na uwezo wa kuwasaidia wasanii wetu wa zamani walioiletea sifa nchi hii, wengine kwa kweli hali zao sio nzuri hata kidogo wanahitaji msaada.

Mhe. Wanu Hafidh Ameir: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii ili kumuuliza Mhe. Waziri swali moja dogo la nyongeza. Mbali ya msanii huyu kupeperusha bendera nje ya nchi, serikali pia imekuwa ikimtumia sana katika matangazo mbali mbali ili kufikisha ujumbe kwa jamii.

Je, kwa kila tangazo serikali ilikuwa inamlipa kiasi gani msanii huyu.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Spika, masuala ya kutumika kwa msanii katika shughuli ya biashara ni makubaliano baina ya msanii na taasisi anayoitumikia. Kwa hivyo, kama kuna taasisi yoyote ambayo imemtumia basi ni juu yao yeye na taasisi inayohusika kuangalia ni fedha gani inahitajika katika kumlipa. Mimi Wizara yangu ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo sijawahi kumtumia kwa shughuli za kupeleka ujumbe, kwa hivyo kama Wizara ya Afya imemtumia basi ni juu yao Wizara ya Afya, kama Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali au taasisi yoyote ile, basi yenyewe ndio inapanga namna gani alipwe.

Mkakati wa Kuhamasisha Mchezo wa Kuogelea

Mhe. Saleh Nassor Juma – Aliuliza:-

Kuogelea ni moja kati ya michezo iliyotokea kuchukua nafasi kubwa katika mashindano ya "Olympic" na kwa kuwa wanaoshinda mchezo huu mara nyingi hata bahari katika nchi zao hakuna. Kwa kuwa Zanzibar tunayo bahari kubwa na watu wengi wanajua kuogelea.

(a) Serikali imechukua hatua gani kuwahamasisha vijana kushiriki katika mchezo huu.
(b) Je, tunazo timu ngapi za mchezo wa kuogelea hapa Zanzibar.
(c) Zanzibar tumeshiriki mara ngapi katika mchezo huu Kimataifa na tumeshinda mara ngapi.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo – Alijibu:-

Nakushukuru Mhe. Spika, naomba nimjibu Mhe. Mjumbe swali lake nambari 5 kama ifuatavyo.

(a) Mhe. Spika, serikali imechukua hatua mbali mbali kuwahamasisha vijana kushiriki katika mchezo wa kuogelea. Miongoni mwa hatua hizo ni kuwashajihisha kuunda chama chao cha mchezo huo, ambacho baadae tumekisajili na kina uongozi rasmi.

Pili, ni kuwashajihisha kushiriki katika mashindano ya kitaifa ya mchezo huo, ambayo hufanyika Dar es Salaam na kwengineko.
Tatu, serikali imewahi kumpeleka kijana mmoja kwenda kusomea ualimu wa mchezo huo wa kuogelea nchini Ujerumani.

(b) Mchezo huu unazo timu sita hivi sasa, timu hizo ni Timu ya KMKM, Jeshi, Polisi, Stone Town, Kawe Group Swimming Club na International School Mbweni.

(c) Zanzibar imeshiriki mara tatu katika ngazi ya kimataifa ya mchezo huu. Mwaka 2008 tulishiriki katika mashindano ya dunia yaliyofanyika China. Mwaka 2010 tulishiriki katika mashindano ya Olympic yaliyofanyika Italy na mwaka 2012 tulishiriki katika mashindano ya Olympic yaliyofanyika Uingereza na katika mashindano yote hayo kwa bahati mbaya hatujawahi kuchukua medali hata mara moja.

Mhe. Spika, naomba nichukue fursa hii kukitaka chama cha kuogelea na wapenzi wa mchezo huu kuzidisha ari ya mazoezi ili tuweze kushinda katika mashindano ya kitaifa na kimataifa.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri sana ya Mhe. Waziri, naomba kuuliza swali moja dogo la nyongeza. Kwa kuwa katika awamu ya pili na ya tatu Zanzibar ilikuwa ikifanya vyema sana katika masuala haya ya mchezo huu wa kuogelea, ikiwa ni pamoja na kuleta medali za dhahabu katika mashindano ya Olympic, kama kipindi kile walichokuwa wakishiriki vijana wetu akina Fidel Ali, waliwahi kutuletea medali za dhahabu hapa.

(a) Je, ni sababu gani za msingi zilizosababisha mchezo huu kuporomoka moja kwa moja.
(b) Kwa kuwa Jiografia ya Zanzibar inatoa nafasi kubwa ya Wazanzibari kuwa nguli sana katika masuala ya kuogelea, ni sababu gani za msingi zinazopelekea hata kushindwa na Burundi ambao hata ziwa hawana pale.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Nakushukuru Mhe. Spika. Mhe. Spika, sababu za msingi zilizofanya mchezo huu kushuka kiwango chake, ni kwamba chama cha kuogelea na wapenzi wake walipunguza ari ya mazoezi. Kwa hivyo, jitihada ambazo zifanywe ni kuwataka chama cha kuogelea na waogeleaji wenyewe wahakikishe kwamba wanafanya mazoezi kwa hali ya juu na kwa nidhamu kubwa na hicho ndio kitu pekee cha kuhakikisha kwamba wanafanya vizuri Mhe. Spika.

Nam. 9

Kazi za Mamlaka ya Mji Mkongwe

Mhe. Jaku Hashim Ayoub – Aliuliza:-

Mamlaka ya Mji Mkongwe ndiyo iliyopewa jukumu kisheria kusimamia na kuendeleza Mji Mkongwe wa Zanzibar, ambao ni sehemu ya urithi wa Kimataifa. Hivi karibuni imeonekana kuwa utendaji kazi wa Mamlaka hii umekuwa haueleweki kwa kuingilia kazi za Mamlaka nyingine kama Baraza la Manispaa.

(a) Je, ni zipi hasa kazi za Mamlaka ya Mji Mkongwe na mipaka ya kazi hizo ikoje.
(b) Inapotokezea kazi za Mamlaka ya Mji Mkongwe zinagongana na kazi za Mamlaka nyengine ni Mamlaka ipi inachukua nafasi (*prevail).*

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake nambari 9 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo.

Sio kweli kwamba utendaji wa Mji Mkongwe haueleweki. Mji Mkongwe unafanya kazi kwa mujibu wa sheria na kwa mujibu wa kifungu cha 7(1)(a) mpaka (j) cha sheria nambari 4 ya mwaka 2010, Mamlaka ya Mji Mkongwe ina kazi zifuatazo:-

(a) Kutayarisha mipango na mikakati kwa madhumuni ya kutekeleza na kufikia malengo ya mpango wa utawala wa urithi, yaani *heritage management plan.*
(b) Kuanzisha, kupanga, kuandaa, kuunganisha na kudhibiti masuala yote yanayohusiana na kutunza, kuhifadhi na kuendeleza eneo la uhifadhi.
(c) Kuchunguza na kuruhusu miradi na pia kuhifadhi na kimaendeleo katika eneo la uhifadhi na kufuatilia maendeleo ya miundombinu.
(d) Kutayarisha na kutangaza mpango mkuu wa uhifadhi, yaani *conservation master plan* na mpango wa utawala wa urithi, yaani *heritage management plan* katika eneo la uhifadhi na kufuatilia miradi ili kuhakikisha kuwa miradi hiyo inakwenda sambamba na mpango husika.
(e) Kukutana na kutoa ushauri kwa taasisi binafsi, idara za serikali na mamlaka za uendeshaji, yaani *regulatory authorities* au taasisi nyenginezo juu ya mambo yanayohusiana na uhifadhi *restoration*, ukarabati *revelation*, uhifadhi wa majengo na mazingira yake.
(f) Kuwa waangalifu juu ya matumizi mazuri ya utunzaji wa maeneo ya jamii na majengo yaliopo ndani ya eneo la uhifadhi.
(g) Kuchukua hatua za kisheria kwa yeyote anayejenga, anayetumia, anayevunja, anayeweka au kubadilisha jengo lolote au eneo la wazi kinyume na sheria ndani ya eneo la uhifadhi.
(h) Kupanga viwango vya malipo yanayohitajika kulipwa katika sehemu yoyote ndani ya eneo la uhifadhi, kama vinavyoruhusiwa na Mhe. Waziri.
(i) Kuitisha mkutano wa wadau angalau mara moja kwa kila mwaka, ili kurahisisha mahusiano na utekelezaji wa sheria na
(j) Kufanya kazi nyengine zozote ambazo zitakuwa muhimu na zenye manufaa katika kufanikisha malengo ya mamlaka kwa mujibu wa sheria.

(b) Inapotokea kazi za Mamlaka ya Mji Mkongwe zinagongana na kazi za mamlaka nyengine, kama vile za Manispaa zinazohusiana na matumizi ya ardhi, miradi, udhibiti na uhifadhi ndani ya eneo la urithi wa dunia wa majengo, basi sheria nambari 4 ya mwaka 2010 itakuwa juu ya sheria nyengine inayofuatiana na sheria hii. Hali hii imeelezwa katika kifungu cha 48(2) cha sheria nambari 4 ya mwaka 2010.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante Mhe. Spika, pamoja na majibu ya Mhe. Waziri. Alipokuwa akijibu swali la msingi alisema sio kweli. Je, Mhe. Waziri kwa mujibu wa Katiba yetu ya Zanzibar hii ya mwaka 1984 binadamu wote huzaliwa huru na wote ni sawa, kila mtu anastahili heshima ya kutambuliwa na kuthaminiwa utu wake, watu

wote ni sawa mbele ya sheria na wanayo haki bila ya ubaguzi wowote wa kulindwa na kupata haki katika sheria mbele.

(a) Mhe. Waziri, utakubaliana na mimi kuwa Mji Mkongwe kuna baadhi ya sheria hawazifuati na watu wengine wanahukumiwa vyengine na wengine wanapata haki nyengine. Je, utakuwa tayari kuchukua hatua nikisha kuthibitishia suala hilo.
(b) Kwa kuwa Mji Mkongwe ni kivutio kikubwa cha watalii na watalii hivi sasa wanapata shida ya kuporwa mali zao wakati wa usiku. Nadhani kuna sababu za makusudi za kuweka taa katika Mji Mkongwe huo.

Mhe. Spika: Mhe. Jaku hili swali la kwanza mimi sikulifahamu vizuri.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Spika, alipokuwa kijibu swali la msingi Mhe. Waziri alisema sio. Nilimuuliza kwamba kuna baadhi ya sheria za Mji Mkongwe kuna watu wengine wanalazimishwa kufuata sheria za Mji Mkongwe na wengine hawaruhusiwi kufuata sheria za Mji Mkongwe. Je, yuko tayari nimthibitishie mimi na hatua gani atachukua Mhe. Waziri kuhusu ubaguzi huu wa Mji Mkongwe.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Spika, sheria ni sheria, kila mtu ana wajibu wa kufuata sheria. Kama yeye anayo taarifa kwamba kuna watu wanakwepeshwa au wanakwepa sheria, basi ni vizuri aisaidie wizara yangu au ausaidie Mji Mkongwe kujua taarifa hii.

Mhe. Spika, swali lake la pili linaulizia juu ya suala la wizi, kuporwa usiku na kila kitu. Mhe. Spika, nakubali kwamba suala hili madam binadamu tunaishi linaweza kutokea mahala popote. Nakubaliana na ushauri wake kwamba kama kuna maeneo yana kiza kikubwa, basi Mji Mkongwe ujitahidi kuweka taa katika maeneo hayo.

Mhe. Ali Abdalla Ali: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa fursa ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, hivi sasa Mji Mkongwe kumezuka wimbi kubwa la kufanywa mahoteli katika nyumba za makaazi, pamoja na ofisi zinazohamwa.

a) Je, katika taratibu zetu si ndio kuondosha katika kujitoa kwenye sifa za Mji wa Kimataifa wa Urithi.
b) Je, ni sheria gani zinatumika kufanywa hoteli hizo, ni Zipa, Manispaa ama Mji Mkongwe wenyewe.
c) Je, nyumba hizo huuzwa ama zinakodishwa, na kama hukodishwa huchukua kipindi gani.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Spika, jitihada ya Mamlaka ya Mji Mkongwe hivi sasa ni kupunguza mahoteli katika maeneo ya Mji Mkongwe. Hivi sasa ruhusu za ujenzi wa mahoteli katika maeneo ya Mji Mkongwe hazitoki hivi hivi kiholela ni lazima kuwe na sababu ya msingi kabisa.

Mhe. Spika, suala la makaazi na maofisi. Mhe. Spika, ni kwamba hivi sasa nafikiri serikali inajitahidi sana kuondoa ofisi zake katika Mji Mkongwe, ndio maana wana *plan* ya kujenga ofisi za serikali. Ukipita sasa hivi ofisi nyingi ya serikali toka Mji Mkongwe yanajengwa.

Kwa mfano ukienda Mazizini kuna Wizara ya Sheria na Katiba pale tayari imejenga ofisi yake, Osifi ya Mwanasheria Mkuu tayari imejenga ofisi yake, na kuna mipango ya ofisi nyengine nazo kujengewa ofisi zao katika maeneo yale nje ya maeneo ya Mji Mkongwe, ili Mji Mkongwe ubakie katika sheria za urithi kama kawaida.

Suala la makaazi hatuwezi kusema watu wote wa Mji Mkongwe watoke, ujambazi utaongezeka, ni lazima baadhi ya watu wabakie katika maeneo ya Mji Mkongwe ili nako usiku kuwe kuna uhai. Sio kwamba Mji Mkongwe usiku kuwe totoro hakuna mtu yeyote hata watalii watashindwa kutembea kusema kweli.

Mhe. Spika, suala la kwamba nyumba zinazojengwa mahoteli zinauzwa au zinakodishwa. Nyengine zinamilikiwa na watu binafsi na wenyewe wanauza na nyengine zinakodishwa katika utaratibu mbali mbali wa makubaliano baina ya muhusika mwenye nyumba na yule anayetaka kutumia hiyo nyumba.

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi – Aliuliza:-

Mhe. Spika, kabla sijajibiwa swali langu nambari 64 naomba nifanye masahihisho kidogo tu. Mhe. Spika, katika sehemu inayosema 'hali haikuwa mbaya', niseme hali si mbaya. Halafu 'mvua zilinyesha' niseme mvua zinazonyesha au mvua zinanyesha vizuri. Ahsante Mhe. Spika, naomba swali langu nambari 64 lijibiwe.

Kutokana na mabadiliko ya tabia nchi, unyeshaji wa mvua hasa za masika na vuli umekuwa si wa kawaida, ijapokuwa mwaka/msimu huu hali haikuwa mbaya. Mvua zilinyesha vizuri kwenye maeneo mengi ya nchi yetu.

(a) Kwa vile wakulima weu wengi bado huitegemea sana mvua katika ukulima wao, Je wizara ya kilimo ina mpango gani wa kutoa taaluma na taarifa sahihi za upatikanaji wa mvua na matumizi ya maji hayo.
(b) Kuna ushirikiano gani kati ya wizara inayohusiana na kilimo na ile inayohusiana na Mamalaka ya Hali ya Hewa katika upatikanaji wa taarifa hizi muhimu.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili – Alijibu:-

Ahsante Mhe Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake nambari 64 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo.

Mhe. Spika, wakulima wa Zanzibar wana uzoefu mkubwa wa miongo ya hali ya hewa ya nchi yetu, yakiwemo masika, vuli, kaskazi na kipupwe. Vile vile kwa kiasi kikubwa wanajua aina ya mazao yanayozalishwa kwa kila miongo. Hata hivyo, mabadiliko ya hali ya hewa au tabia nchi yalijitokeza kuanzia mwaka 2005, yameleta mshangao kwa wakulima na wananchi kwa jumla.

Mabadiliko hayo yamesababisha mvua kutonyesha kwa wakati wa miongo kama ilivyozoeleka. Vipindi vya jua navyo vimerefuka kuliko kawaida, hali hii inaleta taathira katika mifumo ya kilimo cha mazao mbali mbali iliyozoeleka.

Mhe. Spika, kwa kuzingatia hayo Wizara ya Kilimo na Maliasili kwa kutumia taasisi zake, imekuwa ikitoa taaluma kwa wakulima juu ya mabadiliko ya hali ya hewa na mbinu za kilimo bora, ili kukabiliana na hali hiyo. Taaluma hiyo hutolewa kwa wakulima katika mikutano mbali mbali, vyombo vya habari, huduma za ushauri mashambani na skuli za wakulima.

Taaluma hii hujumuisha matumizi ya pembejeo kwa wakati muafaka, upatikanaji mbegu bora zinazostahamili ukame, matumizi ya mbegu fupi, uvunaji wa maji ya mvua na kuhifadhi unyevu wa ardhi. Mpango huu wa kutoa taaluma ya kilimo kukabiliana na mabadiliko ya hali ya hewa ni endelevu na unahusisha wakulima wote Unguja na Pemba.

Mhe. Spika, Mamlaka ya Hali ya Hewa ni taasisi ya kitaifa yenye jukumu la kutoa taarifa ya mwenendo wa hali ya hewa nchini, ili ziwafikie wananchi wote wakiwemo wakulima. Mamlaka hutoa taarifa kupitia vyombo vya habari kila siku na mbali ya taarifa hizo, pia Wizara ya Kilimo na Maliasili inashirikiana na mamlaka hiyo kwa kupata takwimu za hali ya hewa kwa vipindi mbali mbali, kwa ajili ya matayarisho ya kazi za kilimo, uandishi wa ripoti za miradi na ripoti za maendeleo. Moja kati ya vituo vikubwa vya kukusanya takwimu za hali ya hewa, kipo Kizimbani ndani ya eneo la utafiti wa kilimo. Takwimu zinazokusanywa hapa, pia hutumiwa na Wizara ya Kilimo na Maliasili na taasisi zake katika mipango yao.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, naomba nikushukuru kwa kupata nafasi hii, naomba nimuulize Mhe. Waziri swali moja la nyongeza kama ifuatavyo. Kutokana na mabadiliko hayo ya tabia nchi wakulima wengi msimu huu wamekula hasara, baada ya mpunga wao kukauka hususan wananchi wa Jimbo la Muyuni, ambapo serikali iliahidi kuwasaidia mbegu na kuwaburugia mashamba yao. Lakini hadi hivi ninavyozungumza serikali imeshindwa kufanya lolote katika hayo ambayo waliahidi.

a) Mhe. Spika, Mhe. Waziri atuambie ni kwa nini wakulima wale mpunga wao ulivyokauka na kwa kuwa wizara ilifika ikaona, kwa nini walishindwa kuwasaidia angalau mbegu pishi moja moja, ili wananchi wale waweze kulitatua tatizo hilo.

b) Hivi mpunga kama ule ulipokauka, na kwa kuwa wizara imetapakaa na mabwana shamba, taarifa ilifika lini kutoka kwa mabwana shamba mpaka hatua ile ikafikia na wananchi wakala hasara kiasi kile.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo na Mifugo: Mhe. Spika, swali la (b) naomba arudie.

Mhe. Spika: Mhe. Hija Hassan Hija rudia swali (b).

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, swali la (b) ni kwamba Wizara imekuwa ikituambia kwamba imeeneza mabwana shamba katika maeneo yote, lakini hatua ya mpunga kukauka mpaka anafika Rais hakuna taarifa ambayo ilifika kutoka kwa mabwana shamba. Inakuwaje mpaka anafika Kiongozi Mkuu lakini taarifa kutoka kwa bwana shamba haijafika ofisini kwako.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo na Mifugo: Mhe. Spika, ni kweli Muyuni ni eneo ambalo lilikabiliwa sana na hali ya hewa, mpunga ulikauka na ilikuwa ni hali mbaya. Lakini Mhe. Spika, mimi mwenyewe nilifanya ziara ya kwenda Muyuni pamoja na Mhe. Mwakilishi, nilimpigia simu tukaenda pamoja ilikuwa ni katika kipindi ambacho kama utatia kibiriti basi mpunga utawaka. Ni kweli ilikuwa hali mbaya, tukakaa pamoja tukazungumza na wakulima wa Muyuni, baada ya mazungumzo yale pamoja na wakulima wa Muyuni, alikuwepo na Mkuu wa Wilaya basi mazungumzo yale yakawa na mjadala mrefu kuhusu suala la kuburugiwa tena watu wa Muyuni.

Mhe. Spika, baadhi ya wakulima walisema tusubiri hali itakavyojitokeza, baadhi ya wakulima walisema waburugiwe upya, pakawa na mgongano mkubwa katika kufahamiana kwa kipindi hicho. Kwa bahati nzuri baada ya Mwenyezi Mungu kuteremsha rehma yake, basi mpunga ule ulichipua vizuri sana ndio kipindi alichokwenda akauona Mhe. Rais mpunga ule. Ulichipua mpunga mzuri na ambapo tarajio letu hatukufikiria kwamba itakuwa hali ile, ile ilikuwa ni kudra ya Mwenyezi Mungu kutuonesha kwamba kuna kifo na ufufuo.

Mhe. Spika, nina imani watu wa Muyuni ambao hawakupelekewa mbegu, taarifa ya kuwa hawakupelekewa mbegu hili ni suala ambalo kwa uhakika taarifa hii kwa kipindi kile ilikuwa ni kipindi cha mvua, trekta zilikuwa tayari lakini ilikuwa hata hilo trekta lenyewe haliingii kutokana na mvua ilivyokuwa nyingi. Kwa hivyo, suala la kupelekewa mbegu watu wa Muyuni hili ni suala ambalo lilikuwepo, taarifa mbayo nilikuwa nayo ni kwamba mbegu ilipelekwa.

Mhe. Spika, kuhusu suala la kuwa kuna mabwana shamba lakini taarifa ya kukauka mpunga mpaka ikafikia hatua ile na mpaka kwenda kiongozi wa kitaifa. Sio kweli, kwa sababu mimi mwenyewe nilipata taarifa mapema na nikashirikiana na Mhe. Mwakilishi.

Kuna tatizo Mhe. Spika. Tatizo lililokuwepo mabwana shamba wetu wananchi wa katika mabonde wengi hawawajui. Kwa mfano kuna Sheha mmoja ambaye alikuwa anapelekewa taarifa siku zote na bwana shamba, lakini akasema mimi bwana shamba simjui. Siku iliyokwenda kutizamwa ripoti anaambiwa hii saini ya nani. Akasema hii ni saini ya afisa mmoja wa kilimo yuko hapo. Kwa hivyo, inawezekana kwamba hawa masheha mabwana shamba hawawajui kuwafananisha, kama huyu bwana shamba au afisa wa kilimo. Lakini taarifa ya Muyuni ilifika katika Wizara kwamba mpunga wa Muyuni umekutwa na matatizo, ndio maana mimi nikaanza kufanya ziara na maafisa wangu tukaenda kuona mpunga wa Muyuni kwa hali iliyokuwa Mhe. Spika.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, tunatakiwa tukisema tuseme kwa utafiti na sio vyema kuja kupotosha umma. Kwa hivyo, naomba niweke sawa maneno ambayo nimezungumza mimi na Mhe. Naibu Waziri kwamba Wizara ndiyo iliyoahidi kupeleka mpunga Muyuni, lakini mpunga uliopelekwa ni kwamba umenunuliwa kwa umahiri na Mhe. Mwakilishi wa Muyuni, Mhe. Jaku Hashim Ayoub sio wizara. Iliyoahidi kutoa mpunga ni serikali, lakini ikashindwa na Mhe. Mwakilishi akaamua kununua mpunga kwa niaba ya wananchi wake. Kwa hivyo, naomba kuweka sawa hivyo.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili: Sikumfahamu vizuri alivyozungumza Mhe. Spika.

Mhe. Spika: Anasema mpunga ulioahidiwa na serikali haukupelekwa, isipokuwa Mwakilishi mwenyewe akanunua mpunga huo. Sasa mimi nasema una maelezo kuhusiana na hilo.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili: Mhe. Spika, nadhani hili suala nitakwenda kulifanyia utafiti Wizarani.

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Nakushukuru Mhe. Spika, na mimi kunipa nafasi hii. Mhe. Spika, katika majibu yake Mhe. Naibu Waziri alieleza kwamba wizara yake huwa ina mpango endelevu wa kujenga au kutoa elimu kwa wakulima katika mambo hayo ya kilimo na kuwashajihisha katika kujenga mabwawa kwa ajili ya kuhifadhia maji.

Mhe. Spika, mimi nataka kujua tu kwamba wizara yake labda imeweza kujenga mabwawa mangapi ya kuhifadhia maji na katika maeneo gani.

Mhe. Waziri wa Kilimo na Mifugo: Mhe. Spika, mpaka sasa hivi kuna eneo la Mwembe Mpunga sehemu moja tumeweka pale ya darasa ambapo mabonde mengi yatakwenda kusoma pale, na pale ndipo tulipoanzia kwanza. Sehemu nyengine itafuatia Cheju, hiyo ni sehemu tu ya kuanzia hapo Mwembe Mpunga Mhe. Spika.

Nam. 35

Magodoro Hospitali ya Chake Chake

(Mhe. Mjumbe aliyetaka kuuliza swali hilo hapo juu ameliondoa).

Nam. 54

Uchelewaji wa Fedha za Mikopo kwa Wanafunzi

Mhe. Jaku Hashim Ayoub – Aliuliza:-

Kwa muda mrefu wanafunzi kutoka Zanzibar wanaosoma nje ya nchi wamekuwa na kilio cha serikali kutowatumia fedha kwa muda muafaka, wakiwemo wanaosoma China, Uganda na maeneo tofauti na kuwafanya baadhi yao kufanya kazi za vibarua baada ya kusoma.

a) Kwa kuwa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kila mwaka inapitisha bajeti ya mfuko wa elimu ya juu, kwa nini wanafunzi hao hawatumiwi fedha kwa wakati.
b) Hatua ya kuwacheleweshea fedha na kusoma katika mazingira magumu wanafunzi hao wakiwemo watoto wa kike kama wakifeli au kujiingiza katika mambo yasiyofaa nani wa kulaumiwa kati ya serikali na wanafunzi.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali – Alijibu:-

Mhe. Spika, kabla sijajibu nina masuala mafupi nataka niyaeleze. Mhe. Spika, ni kweli kwamba Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu ya Zanzibar imedhamini wanafunzi 153 wanaosoma masomo mbali mbali katika vyuo vya nchi za nje. Mhe. Spika, ni vyuo vya nchi za nje. Vyuo hivyo ni Ukraine, Malaysia, Uganda, China na nyenginezo.

Mhe. Spika, kwa mujibu wa *visa* wanayopewa wanafunzi hawa, hawaruhusiki au hawaruhusiwi kufanya kazi. Kwa hivyo, kama wapo wanafunzi ambao wanaofanya kazi na tunawazungumza hapa, wakisikilikana watapata adhabu, wanaweza hata wakafukuzwa nchini.

Mhe. Spika, naomba sasa nimjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 54 lenye vifungu (a) na (b) kama hivi ifuatavyo:-

(a) Ni kweli kwamba Wizara yangu iliidhinishiwa bajeti ya Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu ya shilingi bilioni 8 mwaka wa fedha huu 2012/2013. Kwanza nataka niishukuru na niipongeze serikali kwa fedha hizo walizoziidhinisha Baraza hili la Wawakilishi kwa msaada mkubwa walioidhinisha bajeti yangu, ili kupata nyongeza ya bilioni 8 badala ya bilioni 4 kama nilizopata bajeti iliyopita.

Mhe. Spika, fedha hizi zilizoidhinishiwa Wizara yangu si kwamba zinatiwa zote kwenye bajeti ya wizara, na Wizara ya Fedha inajitahidi kama iwezekanavyo kuziingiza kwa wakati muafaka fedha zinazohitajika katika bajeti ya wizara yangu.

Katika bajeti hiyo zimeingizwa shilingi bilioni 4.3 kati ya bilioni 8 katika bajeti ya wizara, ambayo ni sawa na asilimia 75 ya bajeti yote. Kwa kiasi kikubwa asilimia 75 ya fedha hizi zimelipiwa wanafunzi wanaosoma nchi za nje kwa kukidhi gharama za chakula, malazi, malipo ya masomo na kadhalika.

Kwa hiyo, bajeti iliyobakia ya asilimia 25 italipwa kwenye mwezi wa Aprili mpaka Juni katika kipindi hichi, na pindi fedha hizo zikiingizwa wanafunzi waliobakia watalipiwa gharama zao za masomo, chakula, malazi na kadhalika.

Mhe. Spika, ni kweli kabisa wanafunzi walioko nchi za nje gharama zao za masomo ni kubwa. Kwa mfano, mwanafunzi mmoja alioko Uchina anayesoma miaka 6 udaktari anagharimu shilingi milioni 56 mwanafunzi mmoja peke yake, kwa sababu hiyo ndio maana hivi sasa tumezuia kuwapeleka wanafunzi nchi za nje kutokana na ukubwa wa bajeti yao kama wanafunzi hao masomo yao yanapatikana ndani.

(b) Kuchelewa kuwatumia fedha wanafunzi wanaosoma nchi za nje sio kisingizio cha wanafunzi hao kufeli au kufanya mambo yasiyofaa. Wizara yangu imekuwa ikifanya juhudi ya kuwafuatilia wanafunzi walioko nchi za nje katika masomo yao ama kwenda kuwatembelea moja kwa moja au kwa kutumia ofisi zetu za ubalozi zilioko huko na wala hatujagundua au kupata taarifa kwamba wanafunzi hao wanajihusisha na mambo hayo na kufanya kazi.

Mhe. Spika, nakushukuru sana.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Spika, ahsante pamoja na majibu mazuri aliyoyatoa Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, naomba kuuliza swali moja dogo la nyongeza kama hivi ifuatavyo.

Serikali ina mpango gani wa kusitisha vijana wetu kwenda kusoma nje ya nchi ukizingatia masomo yale yanapatikana ndani ya nchi hii vikiwemo visiwa vya Unguja na Tanzania Bara, ili kuokoa au kuondoa tatizo hilo lisizidi kutokea tena.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, hivyo ndivyo nilivyosema kwamba hivi sasa tumesitisha na wala hatuwapeleki tena wanafunzi wa Zanzibar kusoma nchi za nje kama hawakupata *scholarship* kwa kudhaminiwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar tumesita kutokana na gharama kubwa zinazotukabili, ikiwa masomo yale yanaweza kupatikana hapa nchini ikiwa Zanzibar au Tanzania Bara na hilo ndilo jibu ambalo nimelitoa. *(Makofi)*

Mhe. Spika, ahsante sana.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Spika, ahsante sana pamoja na majibu mazuri Mhe. Waziri, na mimi kuweza kunipa fursa hii ya kuuliza swali la nyongeza. Mhe. Waziri katika majibu yake alitamka suala la kusema kuwa si kweli kuchelewa fedha kunasababisha kufanya kazi wanafunzi au vitendo vyengine.

Je, Mhe. Waziri huoni tabu kutamka lugha hiyo kusema hivyo wakati ni kweli sababu moja ya kutopelekewa fedha wanafunzi ni kuweza kufanya kitu ambacho ni kinyume na maadili yao.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, nimesema katika jibu mama kwamba sisi wenyewe Wizara ya Elimu tunafuatilia suala la wanafunzi wetu walioko nchi za nje na nimewataja Urusi, Ukraine na kadhalika na tumebaini wanafunzi hao hawafanyi kazi na wala hawafanyi vitendo hivyo vya utovu wa nidhamu tulivyovizungumza.

Kutokana na hali hiyo, ndio maana nikasema si kweli kwamba wanafunzi hao kwa sababu hawapelekewi fedha zao kwa wakati wanafanya vitendo hivyo. Vile vile nilisema kwamba asilimia 75 ya mahitaji yao ya chakula, mavazi, masomo na kadhalika yameshalipwa yote na kilichobakia asilimia 25 yatalipwa katika *quarter* hii ya mwisho inayomaliza mwezi wa Julai. Kwa hiyo, hivyo ndivyo nilivyosema katika jibu langu mama.

HOJA ZA SERIKALI

Mswada wa Sheria ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu (Utekelezaji wa Majukumu) ya 2013

(Majadiliano Yanaendelea)

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, wiki iliyopita nilikuwa nimebakisha wachangiaji wangu wawili, ambaye mmoja amebakia dakika tano ni Mhe. Hamza Hassan Juma, basi atumie dakika tano kwa ajili ya kumaliza hotuba yake na baada ya hapo twende kwa Mhe. Asha Bakari Makame na hatimaye Mhe. Mwanasheria Mkuu.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Spika, nikushukuru kwa kunipa nafasi hii nikaweza kumalizia dakika zangu tano zilizobaki na nitajitahidi niende haraka sana.

Mhe. Spika, jengine ambalo nataka kuongezea kwenye mchango wangu kwenye kifungu cha 18 kuhusu utaratibu wa kupata ushauri elekezi. Kwa kweli hapa kidogo namuomba Mhe. Mwanasheria Mkuu kupitia kwako Mhe. Spika, wakati atakapokuja kutoa ufafanuzi anisaidie. Mhe. Spika, tunajua kwamba Mhe. Mwanasheria Mkuu atakuwa anasimamia zaidi masuala yote ya kisheria kwa upande wa serikali pamoja na wale atakaowaagiza kusimamia shughuli zote, aidha za uwakili au kesi za serikali.

Lakini hapa Zanzibar Mhe. Spika tunalo tatizo moja na tatizo hili liko zaidi katika hizi ajira binafsi. Hivi sasa ukiangalia Mhe. Spika wafanyakazi wetu wengi wanaofanya kazi katika taasisi binafsi aidha kwenye sekta ya utalii, yaani mahoteli au kwenye maeneo mengine kama vile viwandani ama sehemu nyengine, kuna tatizo kubwa sana la mikataba ya ajira.

Kwa mfano, utakuta wafanyakazi wanafanya kazi hawana mikataba ya ajira na wakati mwengine hata wale wenye mikataba ya ajira mikataba ile inakuwa ni ya *part time*, yaani ya miezi 6 au 9 ama mwaka mmoja. Kwa hiyo, hii inapelekea Zanzibar kuwa na wafanyakazi wengi wasio rasmi kitu ambacho kinashindwa kuwahakikishia hatima ya maisha yao.

Mhe. Spika, jambo ni ni vyema tukaliangalia sana, kwa sababu vyenginevyo mzigo wa wananchi kuelemea kutaka kuajiriwa ndani ya serikali utakuwa mkubwa sana. Kwa hivyo, ndio maana watu wetu kila unapowaambia nendeni katika sekta binafsi kwa sababu wanajua hawana uhakika wa hatima ya maisha yao. Sasa hili sijui atawasaidia vipi na kwa sababu ingawa sekta binafsi lakini wafanyakazi hawa bado wako chini ya Waziri anayeshughulikia ajira, kwa hiyo ina maana Mhe. Waziri anayeshughulikia masuala ya ajira kwamba hawa ni bado ni watu anatakiwa awashughulikie.

Kwa maana hiyo, sijui ushauri wa kisheria katika kuandaa mikataba ya hawa watumishi ambao wako kwenye sekta binafsi hapa sijui Mhe. Mwanasheria Mkuu atakuja kunisaidia vipi katika eneo hili. Kwa kweli ni eneo ambalo limeajiri watu wengi na pengine zaidi kuliko walioajiriwa serikalini na tukiendelea kuwaacha wanagaragara hawana uhakika wa maisha yao ya baadaye na mikataba yao ya muda na wala hawana viinua mgongo, kwa kweli itakuwa ni mzigo mkubwa sana kwa upande wa serikali, kwa sababu kila mtu atakuwa haamini ajira yoyote isipokuwa ajira ya serikali.

Jambo jengine ambalo nataka kulizungumzia kwenye kifungu cha 20 hapa kwenye *marginal* imeandikwa Maoni ya Mwanasheria Mkuu kuwa Msimamo wa Serikali. Mhe. Spika, ukiangalia kifungu cha 20 naomba kunukuu kidogo hapa.

Kifungu cha 20(1) cha mswada kinasema hivi:-

> "Ushauri wa kisheria wa Mwanasheria Mkuu uliotolewa chini ya masharti ya Sheria hii utabaki kuwa ni msimamo wa kisheria wa Serikali juu ya jambo hilo isipokuwa kama Rais ataelekeza vyenginevyo au umefanyiwa mapitio vyenginevyo na mahakama yenye mamlaka".

Mhe. Spika, hapa kidogo nataka ufafanuzi ambao kuna jambo ambalo limetokezea hivi karibuni. Mhe. Spika, tulipokuwa na Maoni ya Katiba kila mtu katakiwa kutoa maoni yake. Sasa je kupitia kifungu ina maana Maoni ya Mwanasheria Mkuu ni maoni ya serikali au yanabakia kama ni mtu mmoja mmoja, kwa sababu hapa tayari ina maana tuna-*band* kwenye sheria, ili huko baadaye inapokuja kutokezea isije ikawa tena hivi na vile, hili pia kidogo naomba kupata ufafanuzi.

Vile vile Mhe. Spika, nataka Ofisi ya Mwanasheria Mkuu ijitahidi sana kuandaa utaratibu wa kuweka kumbukumbu na hii itaweza kusaidia katika miaka ya baadaye kuja kuondoa utata kwenye mambo tofauti.

Mhe. Spika, tunao mfano hai ambao umejitokeza na ulileta utata mkubwa sana kwa wananchi wetu na hasa tulipokuwa tunazungumzia kuhusu Hati ya Muungano, ambayo inaambiwa mara sijui ipo au haipo nani alisaini na nani hakuisaini. Sasa hii itukumbushe na iliyopita si ndwele, lakini ndwele hiyo itakayokuja huko mbele.

Kwa maana hiyo, mikataba yote itakayofunga Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar, basi lazima kuwe na *archive* au sehemu ya kumbukumbu, ambapo likitokezea tatizo lolote iwe tunakwenda kwenye kumbukumbu na kuangalia, ili utata uwe haupo.

Kwa kumalizia Mhe. Spika, jambo jengine ambalo nataka kulizungmza ni kifungu cha 13 kinachozungumzia bajeti. Mhe. Spika, tunatengeneza sheria ya Kuanzisha Ofisi ya Mwanasheria Mkuu na katika kutengeza sheria ina maana tunatengeneza kitu ambacho tunakijenga uwezo wa kisheria. Kwa hivyo, tunaiomba sana serikali pamoja na Mhe. Mwanasheria Mkuu kupitia kwako Mhe. Spika, kwamba akae na watu wake aweze kuandaa bajeti ya kutosha ambayo itaweza kuwawezesha watendaji wake kufanya kazi zao vizuri.

Mhe. Spika, ofisi hii ina majukumu makubwa sana kwa serikali. Kwa hivyo, uwezekano wa kuweza kuandaa bajeti nzuri na kuweza kuwahimili katika huduma wanasheria wa serikali itaweza kusaidia wanapokwenda kutia mikataba au kusimamia mikataba ya serikali wasipate vishawishi vyengine vya nje ambavyo baadaye vitatuletea matatizo.

Baada ya hayo machache Mhe. Spika, napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi hii na naunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Asha Bakari Makame: Mhe. Spika, kabla ya yote nikushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kuchangia mswada huu ambao ni muhimu. Vile vile nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia siku hii ya leo ya mwanzo wa wiki kuwepo hapa katika hali ya usalama na afya.

Pia nichukue nafasi hii Mhe. Spika, nimpe pole sana ndugu yetu mtoto wangu kwa upande wangu mimi Mhe. Nassor Ahmed Mazrui kwa kufiwa na baba yake, namtakia kila la kheri na Mwenyezi Mungu ailaze mahala pema roho ya marehemu peponi, amina.

Mhe. Spika, kwanza kabisa pamoja na kwamba wenzangu wameshapongeza, lakini wanasema watu kuwa nyongeza haigombi. Kwa hivyo, nichukue nafasi hii nimpongeze sana Mhe. Waziri kwa jitihada ambayo anaifanya, pia nimpongeze sana Mhe. Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa jinsi mswada huu ambavyo umepangika vizuri na ni moja katika kutoa dira na miongozo katika miswada yote, ili kuweza kutekeleza wajibu wetu ipasavyo tena kwa ufanisi zaidi Mhe. Spika.

Nikianza mchango niende moja kwa moja kwenye ukurasa wa 316 kifungu cha 2(1) (d), naomba kunukuu kidogo Mhe. Spika.

Kifungu cha 2(1) (d) cha mswada kinaeleza hivi:-

> “Kwa jumla kuweka utaratibu wa uendeshaji wa shughuli za kutoa huduma za kisheria kwa Taasisi ya Utumishi wa Umma”.

Mhe. Spika, hapa ni pahala nyeti kabisa. Kwa hivyo na mimi nitilie mkazo kama wenzangu ambavyo wamechangia, kwa sababu wameshachangia watu mbali mbali, isipokuwa na mimi nimesema nitilie mkazo Mhe. Spika, ili tuhakikishe kwamba ni kweli tunasimamia ipasavyo sheria hii, kutowanyima haki wenzetu ambao wanafanya kazi ipasavyo.

Vile vile niende kwenye ukurasa wa 326 ambapo mwenzangu amechangia vizuri Mhe. Hamza Hassan Juma na ameelezea vizuri. Sasa na mimi niseme kwamba sekta binafsi kwa kweli imekaa kama haina mwenyewe, ingawa kuna Wizara ambayo inajihusisha sana, yaani Wizara ya Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika.

Lakini bado sekta hii naona kwamba na tunamuomba Mhe. Mwanasheria Mkuu kupitia kwako Mhe. Spika, katika sheria hii ahakikishe kwamba sekta binafsi zinapewa haki zake ipasavyo. Kwa mfano, tukienda kutembelea sehemu mbali mbali basi utapewa mashtaka kwenye sekta hii binafsi ambayo mengine si ya kuridhisha.

Namshukuru sana Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika anajitahidi lakini bado mambo yanafichika na wenzetu hawa wa sekta binafsi wanayaficha haya mambo, ili kuwakosesha haki zao watu wa sekta binafsi. Pia nilisema Mhe. Spika nitilie mkazo, kwa sababu pamoja na yote wenzetu wa sekta binafsi wanatusaidia sana katika maisha ya hapa na pale na wanajisaidia wao wenyewe katika kuendesha maisha yao.

Mhe. Spika, ukurasa wa 27 kifungu cha 21, naomba kunukuu kidogo Mhe. Spika.

Kifungu cha 21(1) cha mswada kinaeleza hivi:-

> "Mwanasheria Mkuu anaweza kutoa miongozo ya kina juu ya namna ambavyo kesi zilizofunguliwa na Serikali au dhidi ya Serikali zitasimamiwa".

Mhe. Spika, niseme tu kwamba suala hili nitamuomba sana Mhe. Mwanasheria Mkuu kupitia kwako Mhe. Spika, alitupie macho sana, kwa sababu kuna baadhi ya mambo ambayo yanatendeka katika serikali, lakini ni aibu serikali kushtakiwa na ikashindwa. Kwa hivyo, hii yote inatokana na mambo gani, mambo yetu ambayo hatuyapangi ipasavyo na nitalichangia hili pamoja na masuala ya mikataba.

Kwa kweli namuomba sana Mhe. Mwanasheria Mkuu kupitia kwako Mhe. Spika, kwamba mikataba ya serikali ya shughuli zetu mbali mbali ambazo tunatia saini mikataba naiomba Ofisi ya Mwanasheria Mkuu ahakikishe kwamba mikataba hii inakwenda sambamba na matakwa ya serikali.

Mhe. Spika, ni aibu mikataba mingine tunayoitia saini wakati mwengine tunayefunga naye mkataba anakimbia au hatimizi yale masharti ambayo tumekubaliana kwenye mikataba, almuradi ni mkorogo vyogo wa Juma Muhogo.

Mikataba inayotiwa saini sijui tunaitia saini ya aina gani. Kwa hivyo, namuomba sana Mhe. Mwanasheria Mkuu kupitia kwako Mhe. Spika, kutokana na mswada huu tena ni imani yangu kwamba Mhe. Mwanasheria tunavyokuelewa utendaji wako wa kazi, kuwa utasimamia ipasavyo mikataba yote iende sambamba na matakwa ya serikali na pale inapobidi basi kwa kweli isichukuliwe ikafinyangwa na kugeuzwa mambo mengine. Suala hili namuomba sana Mhe. Mwanasheria Mkuu alisimamie ipasavyo Mhe. Spika.

Nikiendelea na mchango wangu sasa niende kwenye kifungu cha 22 kuna mambo yetu hapa ya kiserikali, ambapo kifungu hiki Mhe. Spika naomba kunukuu kidogo.

Kifungu cha 22 wa mswada kinaeleza hivi:-

> "Uandaaji wa Hati ya Kisheria za Serikali".

Mhe. Spika, namuomba sana Mhe. Mwanasheria Mkuu na nitilie mkazo na wenzangu wamechangia vizuri, na kwa sababu tena nimebakia mimi nafikiri wa mwisho na itakuwa zile dondoo zote ambazo ni muhimu wenzangu wameshachangia, isipokuwa mimi nitilie mkazo tu Mhe. Spika katika uandaaji Hati za Kisheria za Serikali. Kwa kweli ni kitu muhimu sana Mhe. Spika na ni kitu ambacho kinatupa muongozo hasa namna gani ya uandalizi wa Hati za Kisheria za Serikali.

Vile vile nizungumzie suala jengine kuna wenzangu wamezungumza hapa kwamba tunayo Serikali yenye Mfumo wa Umoja wa Kitaifa na wameelezea na mimi naunga mkono kwamba nadhani tuwe na sheria maalum ambayo inaelezea hasa namna gani ya Mfumo wa Umoja wa Kitaifa. Lakini hii sijui niseme ni mara ya nne au ya tano kuiomba serikali itufanyie semina juu ya kuelimishwa sisi Wajumbe wako wa Baraza hili tukufu, kwa ajili ya kuelezwa Mfumo wa Umoja wa Kitaifa.

Kwa hivyo, sijui sasa nadhani nimsukumie Mhe. Mwanasheria Mkuu pamoja na Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria, kwa sababu miongoni mwao mmoja alikuwa ni Mjumbe Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria alikuwa ni Mjumbe. Kwa maana hiyo, naomba sana Mhe. Mwanasheria Mkuu pamoja na Waziri wa Katiba na Sheria kupitia kwako Mhe. Spika, watufanyie hii semina, kwani ni muhimu ambayo itatupa mwanga na sisi wengine tunaulizwa huko nje. Sasa kama mimi sijui sijapata semina ya kunielimisha sijui itakuwa vipi.

Mhe. Spika, nadhani washirikiane Mhe. Mwanasheria Mkuu pamoja Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria, kwa sababu tayari tumeshaanza kupitisha hizi sheria pamoja na Waziri wa Katiba na Sheria, ili watupatie semina tena sio siku moja ya kuja kupewa blaa blaa, isipokuwa tufanyiwe semina siku mbili ambazo tukiondoka pale tunajua nini tunawaelimisha na wananchi wetu.

Jambo la mwisho Mhe. Spika, naomba tujitume zaidi na nitaomba Ofisi ya Mwanasheria Mkuu pamoja na Waziri wa Katiba na Sheria, kwamba kuna haja ya kupitiwa sheria zetu zote kwa sababu hivi sasa baadhi yake zimepitwa na wakati. Kwa maana hiyo, nitaomba tujitume Wizara hii ya Katiba na Sheria pamoja na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu, ili tuhakikishe sheria zetu nyengine tunazipitia, kwa ajili ya kwenda sambamba na sheria hii ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu zioane, ili tuweze kufanya kazi zetu kwa ufanisi zaidi.

Mhe. Spika, nina imani sana kwamba kuna baadhi ya sheria zetu kuwa hatwendi sambamba na matakwa yetu ya hivi sasa. Kwa hivyo naomba sana tuangalie kidogo kidogo mpaka baadaye tunaweza kuzimaliza, ili na sisi hivi sasa twende kwa sayansi na teknolojia.

Baada ya kusema hayo Mhe. Spika na mimi niungane na wenzangu nasema naunga mkono hoja mswada huu wa sheria kwa asilimia mia moja na ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Spika, baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupa afya na kuweza kukutana hapa leo kwa ajili ya kuchangia hoja ya mswada huu naomba na mimi nikushukuru kwa kunipa fursa hii kusaidiana na wenzangu katika kuchangia hoja ya mswada huu.

Mhe. Spika, kwa vile huu mswada unaihusu ofisi yangu nitachukua muda kumsaidia Mhe. Waziri, kwanza kuweka bayana zaidi mambo yanayohusiana na mswada huu ambayo yamezungumzwa, pia kujaribu kufafanua baadhi ya hoja ambazo Waheshimiwa Wajumbe wenzetu wameeleza humu na mengine wametaka ufafanuzi.

La kwanza Mhe. Spika, wametupa dhima kubwa, kwa maana ya kwamba wameeleza sifa nyingi na imani yao kwa ofisi yetu. Mhe. Spika, mimi naomba niwahakikishie wenzangu hapa kwamba tunachukua hilo kama ni changamoto ya kufanya kazi zaidi ili kuitunza ile imani ambayo wametupa. Nitajitahidi na naamini wenzangu wamekuwepo, lakini na Mhe. Waziri na yeye ameyasikia ili kuyasimamia kutunza ile imani ambayo tumepewa.

Lakini la pili ambalo nimelizungumza sana hapa ni kuhusiana na maandalizi ya Mswada huu. Ni kweli tulijitahidi na mimi nilikuwa nawambia wenzangu kwamba Waswahili wana msemo wanasema kwamba "Mfinyanzi hulia gaeni**"** Msemo ule maana yake si kuhimiza kwamba "Mfinyazi**"** alie gaeni, lakini ni kutahadharisha wengine kwamba ikiwa wewe ni **"**mfinyanzi**"** basi usilie gaeni, ujitahidi ulie chombo kilichokuwa kizuri zaidi. Na hilo na sisi tulizingatia busara ile ambayo tumeelezwa katika Msemo huo.

Mhe. Spika: Niwaombe Waheshimiwa Wajumbe wanaotoka nje wajue kwamba mara baada ya Mhe. Mwanasheria Mkuu tunafanya majumuisho na hatimae tuwaombe Waheshimiwa Wajumbe kupitisha Mswada huu. Kwa hiyo tuelewe baada ya dakika chache kutakuwa kuna hatua hiyo.
Mhe. Mwanasheria Mkuu endelea.
Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Spika, kwa vile najua Mhe. Waziri atakuja kufanya majumuisho ya hoja pengine mahsusi, nijaribu kuangalia zile hoja za jumla na nimejaribu kutoa maelezo ya jumla kuhusiana na hoja mbali mbali. Kwanza nilizungumza sana kuhusiana na madhumuni ya Mswada huu.
Mhe. Spika, dola yoyote nguvu yake na nguzo yake ni sheria. Ndio maana mihimili miwili ya dola basi kazi yake kubwa ni kusimamia sheria. Kwanza Baraza la Wawakilishi kama chombo cha kutunga sheria. Lakini pia na Mahakama kama chombo cha usimamizi wa sheria. Kwa upande wa serikali nayo inatakiwa iwe madhubuti, iwe makini katika suala la usimamizi wa sheria. Mwega wake katika hili ni Ofisi ya Mwanasheria Mkuu.

Mhe. Spika, kwa miaka mingi tumekuwa tukienda lakini kwanza Ofisi yenyewe kuwa na mamlaka ya kisheria, kusimamia yale majukumu yaliyopewa hilo lilikuwa ni tatizo kama Waheshimiwa wengi walivyoeleza humu ndani. Lakini na kubwa ni kuhusiana na watendaji wa Ofisi hii na sio wa Ofisi hii tu lakini na watendaji wengine Wanasheria ambao wapo nje ya Ofisi hii. Kwa hali na mazingira ya sasa Mhe. Spika, wanahitaji kusema kweli wawe na uweledi wa hali ya juu, kuwa na uwezo wa hali ya juu, pia wanahitaji na usimamizi.

Wanafalsafa wanasema elimu isiyotumika kwa haki ni ujanja, elimu yoyote ni lazima itumike kwa haki. Sasa kama haikutumika kwa haki basi inakuwa sio elimu tena hiyo inakuwa ni elimu ya ujanja. Sheria ni kitu muhimu kwa hivyo lazima matumizi yake yatumike kwa uwadilifu na yatumike kwa haki. Kwa hivyo ule usimamizi ulikuwa unahitajika kwa haraka zaidi.

Jengine kuhusiana na watendaji katika sekta ya sheria ni kwamba sasa hivi hatushindani ndani ya Zanzibar wala ndani ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania, lakini tunashindana katika ulimwengu. Dunia imekuwa na utandawazi ni vizuri na watu wetu nao wao wakawa na uwezo ambao unalingana na wana sheria wengine duniani. Nadhani kwa wale waliofatilia kesi ya uchaguzi wa Kenya hivi karibuni wameona ni kwa kiasi gani kiwango cha wenzetu wanasheria wapo hapo jirani zetu Kenya, ambao sisi ndio tumeanza fani hii kuliko wao. Lakini mtu ajiulize je na wakwetu nao wanaweza kuwa na kiwango na uwezo unaofanana na ule? Maana yake kesho tutakuja kushindana na wanasheria wa Kenya.

Mhe. Spika, kwa mfano sasa hivi Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania ina mgogoro na Malawi kuhusiana na suala la mpaka. Suala ninalojiuliza je, una watu wenye uwezo unaolingana na huo. Sisi tupo kwenye Jumuia ya Afrika Mashariki, ni lazima katika kila fani tujiulize na tuweze kujenga uwezo kwa ajili ya watu wetu kwa kiwango kinacholingana na kuzidi kile cha eneo hili la Afrika Mashariki na hata dunia kwa sababu ndio tunayoifanyia kazi. Madhumuni makubwa moja ni kuhakikisha kwamba tunafika huko tunakoelekea.

Jengine Mhe. Spika, nimezungumza kuhusu suala la Naibu Mwanasheria Mkuu na hapa mambo mawili makubwa yalizungumzwa, kwanza kuhusiana sifa za Naibu Mwanasheria MKuu kwa hali ya sasa hivi ziongezwe. Baadhi ya waliozungumza walisema viwe katika kiwango cha Shahada ya Pili. Kikubwa tulichozingatia kwamba ukiangalia Katiba ya Zanzibar, sifa zilizowekwa za Mwanasheria Mkuu ni zile ambazo zimewekwa ndani ya sheria hii ambazo zinazolingana na Naibu Mwanasheria Mkuu. Tusingeweza kuweka sifa ndani ya Sheria kubwa zaidi kwa Naibu Mwanasheria Mkuu, wakati Mwanasheria Mkuu mwenyewe kwenye Katiba hazikuwekwa sifa kama hizo. Lakini ndani ya Katiba na ndani ya sheria hii kilichowekwa ni kiwango cha chini kwamba angalau katika uteuzi bila ya shaka itazingatiwa kwa kadri kama vile inavyozingatiwa kwa Mwanasheria Mkuu kwamba zile ni sifa za chini, lakini kwa kadri itakavyohitajika sifa zitakazotumika bila shaka kwenye uteuzi zaidi ni zile zilizowekwa ndani ya sheria.

Mhe. Spika, jengine lilozungumzwa ni kwamba labda awe Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi kutokana na yaliyojitokeza na hali halisi. Tunasema kwamba ni wazo zuri lakini kama ambavyo lilizungumzwa humu ndani kwamba litahitaji mazingatio wakati wa kuzingaria marekebisho ya Katiba yetu.

Jengine lilizungumzwa kwamba asiwe moga. Mimi nadhani akishakukubali kwamba yeye ni mshauri, akiwa moga labda itakuwa ni hulka yake tu. Kwa sababu kazi ya ushauri kwa mwanasheria kazi yake kubwa ni kushauri. Kazi ya kushauri hutakiwi kumshauri yule unayemshauri lile analotaka kulisikia utakuwa humshauri, hapo itakuwa unamughilibu. Unachotakiwa umshauri kile kitu ambacho wewe unakiamini na wewe uko tayari kukisimami na uwe na hakika kwamba kisheria hiki ni sahihi. Inawezekana unayemshauri hakipendi, inawezekana unayemshauri, maana katika kushauri mtu anaweze akakizingatia au asikizingatie. Lakini humshauri kitu kwa sababu unaona kwamba yeye anapenda hiki na wewe ukampeleka huko huko, hivyo utakuwa hujamsaidia kusema kweli bora abadilishe mshauri kama wanavyosema kuna hadithi moja ya mlevi alibadilisha daktari

Kuna mlevi alibadilisha daktari kwa sababu aliambiwa usivute tena sigara akasikitika, rafiki yake akamwambia wewe unapata shida ya bure, wewe nenda kwa daktari fulani. Alipokwenda kwa daktari mwengine akamwambia hilo suala unaweza ukaendelea lakini ujue hatari iko kwako wewe mwenyewe. Sasa bora umwambie lile lenye hatari mwenyewe anaweza akachagua. Kwa hivyo nakubaliana na aliyetoa wazo hilo kwamba mwanasheria anatakiwa asiwe moga katika utekelezaji wa kazi zake.

Mhe. Spika, jengine alilozungumza ni kuhusiana na suala la vitengo kwamba labda vitajwe ndani ya sheria. Mhe. Spika, Ofisi hii pamoja na kwamba ni ya miaka mingi lakini bado ni ndogo. Juhudi zinazoendelea sasa hivi za serikali na Wizara na Afisi yenyewe ni kuiimarisha. Mimi nimeondoka Ofisi ile kwa mfano mwaka 2002, kwenda kwa Mkurugenzi wa Mashtaka. Nilipoondoka wakati ule kulikuwa na wanasheria 10 lakini mimerudi mwaka 2011 miaka 9 baadaye nikakuta kuna wanasheria 9, badala ya kuongezeka wamepungua. Wakati kule nilipokwenda kuna mwanasheria mmoja ambaye ndio mie mwenyewe, nimeondoka kuna wana sheria 32. Lakini huku walikuwa wamebaki 9 na wengi wale niliokuwa nimeanza nao bahati mbaya sikuwakuta.

Mhe. Spika, na hapa sasa hivi tunasema ni vizuri kwenda kulingana na mahitaji. Huko mbele tutahitaji kitu gani na kukijengea uwezo. Ni vyema kutokana na maendeleo ya Ofisi basi vitengo na idara zizuke au zije au ziwepo kulingana na mahitaji na kadri ya ile hali ya Ofisi yenyewe itakavyofikia. Ukianza leo kwenye sheria ukisema kuwa utakuwa na idara au kutakuwa na vitengo, kwanza itakuzuia katika kuona mahitaji ya baadaye kwa sababu umeshawaweka kwenye sheria, lakini na pili itakupa kwamba ni lazima hizo idara zenyewe zianze kuanzishwa. Ndio maana nikasema kwamba tunaweza tukaanza na vitengo vikakuwa vikawa idara itakapofika wakati huo basi tutafanya hivyo. Lakini tunaona kama tukiziweka kwenye sheria sasa hivi tutakuwa kama tunajizuia yale maendeleo na mtazamo wa kuiendeleaza ofisi yenyewe.

Mhe. Spika, suala jengine ambalo limezungumzwa sana ni suala la Mikataba. Mimi kwanza niwashukuru Waheshimiwa Wajumbe kwamba wameliona hilo umuhimu wa kuisimamia mikataba ya serikali vizuri. Mhe. Spika, naomba nikiri mbele ya Baraza hili kwamba kweli kuna changamoto nyingi katika suala hili na hasara inawezekana inapatikana katika kutokusimamia bila ya shaka ni kubwa vile vile. Kwa hivyo madhumuni yetu ya kuliweka hili wazi katika sheria. Kwanza kuna suala la kuwa makini katika mapatano ndio nia yetu katika kujenga huo uwezo wa kuwa makini katika mapatano. Hii inaonesha kwamba bado kuna udhaifu huo katika mikataba yetu ya serikali.

Jengine ni lile suala la kuwa na vigezo katika masharti. Naamini Mhe. Spika, Waheshimiwa Wajumbe watakubaliana na mimi kwamba leo ukenda Benki yoyote kukopa ukifika wanakupa mkataba wao wa mkopo. Wewe kazi yako ni kujaza tu jina na kiwango unachotaka, lakini tayari umeshaandaliwa. Kwa upande wa serikali kwa sehemu kubwa tunanunua, tunafanya matumizi makubwa, tunaingia mikataba mikubwa, lakini mara nyingi yule tunayetaka kuingia nae mkataba yeye ndiye anayeleta mapendekezo ya mkataba. Hilo si jambo sahihi hata kidogo kwa kweli. Tunachotakiwa kadri inavyowezekana sisi wenyewe serikali tuwe na mikataba yetu au *Standard Form Contract* za kwetu za serikali na kama kuna mtu ambaye anataka kukatibiana na sisi, basi tuanzie kuanzia hapo. Ipo ile ya kimataifa inayojulikana basi pia tukubaliane kwamba ipi tutaifuata, kwa sababu nayo inatofautiana.

Mhe. Spika, suala ambalo tunakusudia kuliimarisha ni hilo na eneo jengine ni usimamizi katika utekelezaji wa mikataba. Katika mikataba kuna mambo mengi ambayo yanatakiwa hatua kwa hatua yaweze kusimamiwa. Kwa mfano mtu hajatekeleza inabidi kumpa taarifa kwamba bwana hili hujalitekeleza, kwa sababu utakapokuja kufungua kesi lazima uwe na kumbukumbu kwamba hili hakulitekeleza na sisi tulimpelekea *notice* kwamba muda wa kulitekeleza hili hujalitekeleza. Au kuna masharti pengine hata kabla ya kuanza mkataba tunaita (*condition precedent)* ambazo mnatakiwa mzifatilie na mfikie pahala msema hizi zimetekelezwa, sasa ndio ukataba unaanza.

Mara nyengine mkataba unaanza bila ya masharti ya awali yenyewe hayajatimizwa. Kwa hivyo ni jambo la msingi. Lakini jengine kubwa ni uwekaji wa kumbukumbu, kama ambavyo Mhe. Hamza Hassan Juma alisisitiza hivi mwisho kwamba hili ni jambo la muhimu. Nia yetu ni kuanzisha *register* la mikataba ya serikali ambapo nakala au mikataba yenyewe itakuwa mbali na kuwepo tu kwamba imeshaingia, lakini itakuwa kwenye *register* maalum na kumbukumbu zake ziwepo ili tuweze kuifatilia, Hili litasaidia kujua serikali imetumia pesa kiasi gani katika mikataba mbali mbali. Fedha nyingi za serikali zinatumika lakini bila ya kujua pengine wakati mwengine tija yake, hasara yake, na bila ya kujua namna gani tunaweza tukadai baadhi ya mambo ambayo tumekatibiana na watu ambao tumeingia kwenye mkataba. Nia yetu ni kuzisaidia katika hilo, lakini bado mimi nasema hili si jambo ambalo tukipitisha Sheria hii basi litakuwa tatizo limeondoka, lakini tuaanza hatua madhubuti za kuweza kusaidia. Bado tunakabiliwa na changamoto nyingi kwa sababu hata uhitaji wa kuweza kulisimamia hili ni jambo muhimu sana napengine litachukua muda.

Mwisho Mhe. Spika, naomba nimalizie kwa ufafanuzi wa baadhi ya mambo ambayo mahususi kidogo yaliulizwa na Waheshimiwa Wajumbe. Kwanza nianze na lile la Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa aliuliza suala la sheria kutokuwa na kifungu cha adhabu. Ni kweli lakini ukiangalia makosa mengi ya jinai ambayo yanaweza yakafanywa chini ya sheria hii yote yamekuwa *covered* vizuri chini ya sheria ya jinai. Tulizingatia hilo lakini tukaona halina haja

kurudia kifungu cha adhabu ndani ya sheria, kwa sababu sheria ya adhabu inaweza ikatumika ipasavyo katika masuala haya. Hakuhitaji kuunda kosa jengine jipya ambalo halimo katika sheria ya adhabu.

Mhe. Marina Joel Thomas aliuliza kuhusiana na suala la AG atakuwa kiongozi wa mawakili, vipi ile sheria yenyewe ya Mawakili Sura ya 98. Ni kweli kama alivyotoa muongozo wake kwamba ile sheria ni ya siku nyingi maana imetungwa mwaka 1941. Wenyewe mawakili waliwahi kuandaa rasimu na nimewasiliana nao hata juzi kwamba ile rasimu wailete tena ili tuipitie tushauriane tuweze kuwa na sheria mpya ya mawakili kwa hivyo alichosema ni kweli lakini tutashirikiana na chama cha Mawakili Zanzibar ili tuweze kuifanyia mapitio ile sheria ya Sura ya 28 ambayo ni ya muda mrefu kidogo.

Jengine alilosema ni kwamba Wanasheria kwenye hii *Government Proceedings Act* wameambiwa wanaweza wakashtakiwa kama hawatosimamia vizuri, sasa Mswada huu unawapa kinga vipi hakutokuwa na mgongano au si itabidi sheria ile ifutwe kile kifungu. Lakini ukweli Mhe. Spika, hakuna mgongano, kwa sababu sheria ile inachozungumza ni kama mtu atafanya uzembe. Hii kinga yake ni pale mtu ambapo hatokuwa amefanya uzembe. Ile inazungumzia katika kusimamia tu ile kesi lakini kinga ya humu ni katika kufanya kazi za jumla. Kwa hivyo ni sheria ambazo hazina mgongano na zinaweza zikaenda sambamba.

Mwisho ni ile hoja ambayo ameizungumza Mhe. Hamza Hassan Juma. Kwanza ni suala la ushirikishwaji Mwanasheria Mkuu katika mikataba ya kimataifa. Ni kweli hilo ni muhimu kwa sababu kuna mikataba mengine mnaweza mkafanya *reservation* ili kulinda silka zenu na maslahi yetu. Kwa utaratibu wa sasa hivi huo ushirikishwaji haupo kusema kweli. Lakini juzi siku ya Ijumaa ilikuwa tuwe na kikao kuzungumzia suala hili baina ya Serikali ya Zanzibar na Serikali ya Muungano bahati mbaya kile kikao kiliakhirishwa. Lakini suala ambalo sasa hivi limo katika kuandaliwa utaratibu maalum wa namna gani Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa ujumla wake kushirikishwa katika masuala haya pamoja na sheria tokea mwanzo mpaka mwisho.

Jengine ni suala la mkataba wa ajira. Ninachoweza kumuhakikishia kwamba Ofisi yangu itashirikiana kwa karibu na Wizara zinazohusika katika kuliangalia utaratibu na kuna mawazo ya awali ambayo yaliwahi kutolewa na Wizara hizi kwa kushirikiana na Ofisi yetu tulitakiwa kuyafanyia kazi ili kuhakikisha kwamba zile ajiwa kwa watu wetu wa Zanzibar zinalindwa kwa kuweka utaratibu maalum wa kisheria. Kwa hivyo ninaloweza kumuahidi ni hilo katika kulitekeleza suala hilo.

Mhe. Spika, la mwisho kabisa ni lile alilouliza je, maoni ya Mwanasheria Mkuu katika maoni ya Katiba ni maoni ya serikali. Kwanza naomba kumuhakikishia Mhe. Hamza kwamba Mwanasheria Mkuu hajawahi kutoa maoni mbele ya Tume ya Katiba. Ndugu Othman Masoud Othman ambaye pia ni Mwanasheria Mkuu alitoa maoni na katika kutoa maoni yale aliiambia Tume mambo mawili. Kwanza maoni yale ni yake binafsi, na haja *share* wala hajawahi kukaa na kiongozi yeyote kuyazungumza na wala hakuna kiongozi ambaye ameyaona kabla ya kuwasilisha kwenye mkutano ule. Kwa hivyo yale ni maoni yake binafsi. Bahati nzuri na serikali haijawahi kutoa maoni kuhusiana na masuala ya Katiba. Kwa hivyo naomba nimuondoe wasi wasi huo yale ni maoni ya Ndugu Othman Masoud Othman ni maoni yake binafsi na sio maoni ya serikali na hayatakuwa maoni ya serikali.

Baada ya kusema hayo Mhe. Spika, niungane na wenzangu walioomba kwamba Mswada huu upitishwe ili tuweze kuufanyia kazi na mimi naunga mkono hoja na nakushukuru sana.

Mhe. Spika: Niwaombe Waheshimiwa Wajumbe waliokuwepo nje waje tumalize kazi hii. Waheshimiwa waliokuwepo nje waingie ndani ili tumalize kazi hii. Mhe. Waziri karibu.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kufanya majumuisho ya Mswada wetu huu uliokuwepo mbele ya Baraza lako. Kwanza hatuna budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia kuwa wazima na tukafika hapa.

Pili kwa niaba yangu na kwa niaba ya Wizara yangu naomba nimpe mkono wa pole Mhe. Nassor Mazrui kwa kuondokewa na Mzee wake. Kwa kweli huu ni msiba wetu sote pamoja na tunamuombea Mwenyezi Mungu ailaze roho ya marehemu katika mahala pema Peponi.

Suala jengine ni kwamba napenda sana niwashukuru wachangiaji wote ambao walishiriki katika kuuchangia Mswada huu. Wachangiaji walikuwa ni 14 naomba niwataje kama hivi ifuatavyo:

1) Mhe. Wanu Hafidh Ameir
2) Mhe. Abdalla Juma Abdalla
3) Mhe. Fatma Mbarouk Said
4) Mhe. Mgeni Hassan Juma
5) Mhe. Hija Hassan Hija
6) Mhe. Ismail Jussa Ladhu
7) Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa
8) Mhe. Hassan Hamad Omar
9) Mhe. Salmin Awadh Salmin
10) Mhe. Ali Mzee Ali
11) Mhe. Marina Joel Thomas
12) Mhe. Hamza Hassan Juma
13) Mhe. Asha Bakari Makame
14) Mhe. Mwanasheria Mkuu

Naomba nitoe shukurani zangu za dhati kwa wachangiaji hao na wale wengine ambao hawakupata nafasi ya kuchangia.
Mhe. Spika, michango ambayo imetolewa na Waheshimiwa Wajumbe mimi nimeigawa katika sehemu tatu. Sehemu ya Kwanza ni kwamba wajumbe wengi na kwamba takriban wote walitupa pongezi Waziri na Mwanasheria Mkuu. Napenda kwa dhati kabisa na wao niwashukuru, nizipokee pongezi hizo kwa niaba yangu na kwa niaba ya Mwanasheria Mkuu.

Lakini zaidi nawambia kwamba pongezi hizi si zangu wala si za Mwanasheria Mkuu lakini ni za Ofisi ya Mwanasheria Mkuu pamoja na Wizara yangu yaani wafanyakazi wa Wizara yangu. Kwa hivyo kwa niaba yao tunasema asanteni sana na tunapokea pongezi hizo. Ingawa kama alivyosema Mwanasheria Mkuu kwamba hii ni changamoto ambayo iweze kutufanya sisi kwamba hapa tulipofika tuzidishe kasi ili tuweze kuongeza hatua zaidi. Kwa maana hiyo tunaomba miongozo yenu hasa Kamati ya Katiba na Sheria pamoja na Wajumbe wa Baraza hili kwa ujumla ili tuweze kwenda mbele katika hatua nyengine kubwa zaidi.

Mhe. Spika, suala jengine kubwa ambalo Mhe. Mwanasheria Mkuu amelizungumza ni suala la kifungu cha 14 (h) ambacho kinazungumzia umuhimu wa mikataba ya serikali katika wizara mbali mbali ni kwamba lazima iongekane na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu. Hili ni jambo muhimu Mhe. Spika, kwa sababu tumeshuhudia katika kipindi hichi kifupi kwamba serikali imeingizwa katika hasara kubwa sana kwa kuingia katika mikataba iliyiokuwa haipitii katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu.

Mhe. Spika, labda niwambie wajumbe kwamba hata Wizara yangu ya Katiba na Sheria ilivyo kama kuna makataba wowote ambao tunataka kuufunga baina ya wizara yetu na mtu wa nje, mkataba ule ni lazima tuupeleke Ofisi ya Mwanasheria Mkuu kwa kupata idhini yake. Huo ndio utaratibu na hivyo ndivyo tunavyofanya. Haina maana kwamba Ofisi yangu ni ya Wizara ya Katiba na Sheria pengine waziri anajua sheria kidogo, pengine Katibu Mkuu anajua sheria kidogo, kwa hivyo tukasema basi tufanye kila kitu sisi. Kwa hivyo ningeliwaomba Waheshimiwa Mawaziri wote katika Mawizara yote basi utaratibu huo ambao unafuatwa na Wizara ya Katiba na Sheria basi ufanyike kwa Wizara zote na katika mashirika yote. Mkataba wowote ule ambao uta – *involve* baina ya serikali na watu wengine basi ni lazima upitie kwa Mwanasheria Mkuu.

Mhe. Spika, sehemu ya pili ya michango ni michango ambayo ilikuwa inataka ufafanuzi na michango hiyo nashukuru baadhi ya ufafanuzi Mhe. Mwanasheria Mkuu ameshaitoa. Lakini mimi ningependa niseme yafuatayo tu. Mhe. Abdalla Juma alizungumza sana kuhusu kifungu cha tano yaani kwanini hakikuanzishwa, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu katika sheria hii.
Kwa kweli Mwanasheria Mkuu ametajwa katika Katiba, kifungu cha 55(1) pamoja na sifa zake. Kwa hivyo isingelikuwa vizuri tena kuirudia tena katika sheria. Lakini ukilinganisha na yale maandiko ambayo yamewekwa katika kifungucha (6) kuanzishwa Ofisi na Naibu Mwanasheria Mkuu, ndani ya Katiba hamna kwa hivyo ndio maana hapa tukasema tuiweke hapa ili kuwe na uhakika kwamba kutakuwa na Mwanasheria Mkuu kama ilianzishwa katika Katiba lakini pia kutakuwa na Naibu Mwanasheria Mkuu kama ilivyoanzishwa katika sheria inayohusika.

Suala la sifa za Naibu Mwanasheria Mkuu ninafikiri alieleza kwa kirefu Mhe. Mwanasheria Mkuu na haina haja tena kulizungumza.

Mhe. Spika, baadhi ya maneno ambayo Mhe. Abdalla Juma alizungumza kwa mfano marekebisho yale maneno ya uelekevu, hayo tunayakubali hatuna matatizo na wakati wa kuandika huu mswada vizuri angalizo lake tutalichukua kwa makini.

Mhe. Fatma Mbarouk naye alizungumzia hasa katika kifungu cha 8(3) na alisema kwamba kifungu cha 8(3) hili suala la Idara na suala la Vitengo, ninafikiri Mwanasheria Mkuu alilizungumza kwamba ninapozungumzia Idara kwa hivyo hili ni suala ambalo limezungumzwa katika sheria ya utumishi wa umma namba 2 ya mwaka 2011, na unapokuwa na Idara basi lazima uwe na Mkurugenzi ambaye Mkurugenzi huyo kwa mujibu wa sheria ile ni Mamlaka ya Rais ambaye anaweza kuteua, lakini unapokuwa na vitengo basi ile ni mamlaka ya Mkuu wa Idara. Na hatuwezi moja kwa moja kuiweka katika sheria kwa sababu hivi sasa tunaanza kukiunda hichi chombo. Kwa hivyo unapoweka moja kwa moja katika Katiba ina maana lazima katika sheria, sheria hii ikipita basi lazima tuanzishe Idara. Pengine itakuwa bado wakati wa kuanzisha Idara haijafika kwa sababu ya watu, pengine kwa sababu ya *volume* ya ile kazi, kwa hivyo ndio tukasema kwamba ni vyema tu tukaweka maneno ambayo yanaweza yakaturuhusu kufanya hivyo hapo baadae.

Mhe. Bi. Mgeni ninamshukuru alizungumza lakini suala lake kubwa yeye lilikuwa suala la Naibu Mwanasheria Mkuu kwamba zile sifa za kuwa Naibu Mwanasheria Mkuu ziongezwe, lakini ninafikiri hili limeshapata jibu kama alivyojibu Mhe. Mwanasheria Mkuu kwamba uanzishaji wa Mwanasheria Mkuu au uteuzi wa Mwanasheria Mkuu umo katika Katiba na zile sifa zilizowekwa zile ndio za chini kabisa, inategemea mazingira yalivyo na mtu gani ambaye anaonekana kwamba anafaa.

Mhe. Spika, cha kutizama hapa ni kwamba moja katika sifa zile ni kwamba lazima mtu yule awe ameshatumikia katika shughuli zile angalau kwa miaka 7. Sasa miaka 7 kwa kweli ni muda mrefu wa kumfanya mtu yule awe ni mzoefu na anaweza kufanya shughuli hizo. Na hapa Mhe. Spika, napenda nizungumzie suala ambalo alilizungumzia Mhe. Hija, Mhe. Hija alizungumza mambo 2.

Kwanza alisema kwamba alishukuru kwamba lile suala la Mwanasheria Mkuu limo kikatiba kama inavyosema kifungu cha 55, lakini yeye akashauri kwamba *accounting officer* ni vizuri awe Mwanasheria Mkuu na asiwe Naibu Mwanasheria Mkuu. Mhe. Spika, napenda tu nimfahamishe Mhe. Hija pamoja na Wajumbe kwamba Mwanasheria Mkuu isingelikuwa vizuri kumfanya kwamba yeye ndie *accounting officer* kwa sababu mbili muhimu.

Kwanza ukitizama uteuzi wa Mwanasheria Mkuu ni uteuzi wa kisiasa, lakini pia katika kifungu cha 43(3) cha Katiba Mwanasheria Mkuu ana mamlaka au zile nguvu zake ni sawa sawa na *cabinet*. Kwa hivyo unapomfanya huyu kuwa ni *accounting officer* ninafikiri hiyo itakuwa kidogo ni tatizo lakini tumfanye hasa yule mtendaji ambaye ni Naibu Mwanasheria Mkuu ambaye majukumu yake Naibu Mwanasheria Mkuu ni ya kila siku, kazi zake pamoja na za utawala, kwa hivyo huyu ndio anaweza akawa ndio *accounting officer* na huu ndio utaratibu unaofanywa katika maeneo ya nchi nyingi zile. Kwa hivyo ni vizuri kwamba na sisi tukafuata utaratibu huu huu. Lakini tukimuweka Mwanasheria Mkuu kwamba yeye ndiye *accounting officer* itakuwa tunakwenda nje kidogo kumfanya kwamba yeye kama ni kiongozi mkuu wa ofisi na pia ni kiongozi wa kisiasa kwa upande mmoja tukamfanya kwamba ni *accounting officer*. Kwa hivyo ndio maana pendekezo letu tukasema kwamba Naibu Mwanasheria Mkuu awe ndio *accounting officer*.

Mhe. Spika, Mhe. Jussa yeye tunamshukuru kwa kutupa pongezi nyingi lakini la pili alisema kwamba hivi vitengo ni bora navyo tukavitaja ndani ya sheria. Sisi tulihisi kwamba kwa wakati huu haina haja kuvitaja, kwa sababu unapokitaja ndani ya sheria na sheria hii ikapita kwa hivyo lazima tukianzishe, pengine wakati wa kukianzisha bado. Lakini hapa tumesema tunaweza kuanzisha pale ambapo haja ipo. Lakini Mhe. Spika, naomba tutizame kifungu cha 8(1) 8(2) 8(3) na 14(1) (a) na (g) (c) na (e) d, h, na m hivi vyote ukivitizama vinaanzisha hasa hivi vitengo au vimetoa muelekeo wa kuwa na vitengo kama hivi.

Kwa mfano kifungu cha 14(a) kwa mfano kinasema kuiwakilisha serikali na taasisi nyengine za umma katika kesi za madai, mashauri ya kupatanishwa na mashauri mengine ya kimadai. Kwa hivyo utaona *directly* hii ni kwamba kitengo hiki au kutakuwa na kitengo ambacho kinazungumzia masuala ya madai. Kwa hivyo hapo baadae tunaweza tukasema Idara ya Madai au Kurugenzi ya madai au kitengo cha madai wakati ambapo unaruhusu.

(c) Kwa mfano kuanzisha kufanyia mapitio ya sera na taratibu zinazohusiana na uandishi wa sheria na uandishi wa hati zinazokuwa za kisheria. Kwa hivyo hapa *directly* ni kwamba tunaambiwa kuwe na kitengo kinachozungumzia masuala ya *legislative drafting* na mambo kama hayo. Kwa hivyo Mhe. Spika, mimi nahisi kifungu cha 14 kinaelezea wazi ule muelekeo wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu utakuwa umegawika katika sehemu ipi na ipi.

Mhe. Spika, Mhe. Jussa pia alizungumzia suala la kifungu cha 20 mimi ninamshukuru kwa maelezo yake ambayo alitoa na hayo yamesaidia katika kuwaelimisha Waheshimiwa Wajumbe lakini pia alizungumzia suala la Mwanasheria Mkuu na Mkurugenzi wa Mashtaka alitaka kujua uhusiano huu uliopo utakuwa ni uhusiano gani. Kwa vile Idara zote hizi za Mwanasheria Mkuu na Mkurugenzi wa Mashtaka ni Idara ambazo ni *independent* zinajitegemea wenyewe, kwa hivyo si kwamba zitaingiliana katika shughuli zao, isipokuwa tulichosema hapa ni katika mashirikiano ya shughuli zetu. Kwa sababu zote hizi ni Idara za Serikali na ukitizama utaona kwamba Ofisi ya Mwanasheria Mkuu mara nyingi inahusiana na mambo *civil* na Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka mara nyingi inahusiana na mambo ya *criminal*.
Kwa hivyo hata wale wanasheria utaona wata-*base* sana katika mambo ya *criminal* na huku mambo ya *civil*. Lakini kwa sababu tunasema hawa ni wanasheria wetu wote si vibaya na wao kuwashirikisha kwa baadhi ya mambo ili wapate ujuzi. Kwa sababu mwanasheria mzuri ni yule ambaye anajua au *at least* ana uelewa wa maeneo yote ya *criminal* na *civil*. Kwa hivyo haya ni mashauriano na mashirikiano na sio kuingiliana katika shughuli zao za kazi zinazohusu.

Mhe. Mahmoud ninafikiri jibu alijibiwa na Mhe. Mwanasheria Mkuu sina haja ya kulizungumza tena na Mhe. Hassan tunamshukuru kwa maelekezo yake mazuri na *inshaallah* tutayafanyia kazi.

Mhe. Salmin pia naye ninamshukuru na hapa alizungumza mambo mawili; la pili naomba nilizungumze mwisho pamoja na suala la Mhe. Ali Mzee, lakini la kwanza lile la kusema kwamba *circular* zitolewe juu ya utaratibu wa kuandika sheria na mambo kama hayo mimi nakubaliana nae na utaratibu huo ndio tuliokusudia hasa na ndio maana katika hii sheria tukasema kwamba Mwanasheria Mkuu atatoa utaratibu maalum wa namna gani ya uandishi wa sheria pamoja na mambo kama haya.

Suala moja ambalo ningependa niseme ni kwamba pale ambapo Mwanasheria Mkuu kwa bahati mbaya hawezi kufanya kazi zake ama amesafiri au ni mgonjwa au ana dharura nyengine tulisema kwamba kazi hizo zitafanywa na Naibu Mwanasheria Mkuu. Lakini baadhi ya Wajumbe walisema kwamba tuweke muda yaani muda gani. Kwa mfano tuseme Mwanasheria Mkuu ni mgonjwa au hayupo tuseme ikifika baada ya wiki mbili ndio pengine Naibu Mwanasheria Mkuu achukue nafasi. Mimi nafikiri hivyo haitokuwa barabara.

Kwa sababu lengo hapa ni kuziba lile pengo la Mwanasheria Mkuu wakati ule hayupo na lile pengo linaanza pale anapoondoka kama anakwenda kwa mfano safari ya kusoma kuanzia kesho kwa hivyo lile pengo litaanza kesho. Hatuwezi kusema Naibu Mwanasheria Mkuu atafanya kazi ya Mwanasheria Mkuu baada ya wiki moja, kwa hivyo itakuwa ile wiki moja hapana mtu pale lakini lengo ni kujaza ile nafasi. Kwa hivyo hapa Mhe. Spika, tulihisi kwamba hakuna haja ya kuweka muda aina hiyo.

Lakini la pili je, kuna uwezekano wa kwamba Naibu Mwanasheira Mkuu, Mwanasheria Mkuu, Mwanasheria Mkuu hayupo na pengine Baraza lipo na tumeshasema huku kwamba Naibu Mwanasheria Mkuu ndie atashika nafasi ya Mwanasheria Mkuu sasa Baraza la Wawakilishi lipo au Baraza la Mapinduzi lipo kwa sababu Mwanasheria Mkuu anaingia katika Baraza la Mapinduzi wanaingia katika Baraza la Wawakilishi, hiyo Mhe. Spika kisheria haiwezekani. Kwa sababu ile ni nafasi ya Mwanasheria Mkuu kikatiba kwa hivyo kwa nafasi ya Mwanasheria Mkuu kikatiba atakuwa ni yule yule Mwanasheria Mkuu wa kikatiba, mpaka hapo ambapo Mwanasheria Mkuu yule ataondolewa basi katiba vile vile imesema itakuwa nafasi yake hiyo imeshamalizika. Kwa hivyo kwa nafasi kama hizo hawezi kuingia, isipokuwa anaweza kuitwa kwa kutoa ushauri tu katika Baraza la Mapinduzi, anaweza akaitwa akaalikwa na katika Baraza la Wawakilishi anaweza akaalikwa lakini si humu ndani, itakuwa ni huko nje akatoa ushauri wake halafu baadae kikao kikaendelea.

Mhe. Spika, Mhe. Ali Mzee ninamshukuru sana kwa maelezo yake lakini napenda haya niyazungumze mwisho maelezo yake yote pamoja na yale mawazo mengine aliyotoa Mhe. Salmin. Mhe. Marina na yeye ninamshukuru alitaka kupata ufafanuzi kuhusu kifungu cha 4(2) akasema ni uhuru gani huo aliokuwa haingiliwi. Kifungu cha 4(2) Mhe. Spika, kinasema kama inavyofuata hivi.

Kwamba kunaanzishwa Ofisi itakayojulikana kama Ofisi ya Mwanasheria Mkuu Ofisi itakuwa taasisi huru na yenye mamlaka ya kujiendesha ndani ya utumishi wa umma Zanzibar. Sasa alitaka kujua taasisi huru maana yake ni nini? Taasisi huru maana yake ni taasisi ambayo ni *independent* haiwezi kuingiliwa na ndio maana tukasema ushauri wa Mwanasheria Mkuu utakuwa ni *final* kwa mambo yote ya serikali yanayohusiana na sheria. Isipokuwa pale ambapo Rais ataamua vyenginevyo. Kwa hivyo ni Rais tu ambaye anaweza aka-*over rule* maamuzi ya Mwanasheria Mkuu lakini kwa mambo mengine yote yanayohusiana na sheria basi maamuzi ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu hayo ndio yataheshimiwa kwa mujibu wa sheria hii ndio nikasema lazima iheshimiwe.

Katika kifungu cha 5(2) vile vile alisema Mhe. Marina kwamba Mwanasheria Mkuu atatekeleza kazi za jumla na maalum na kutumia uwezo wake aliopewa na Katiba, sheria hii na sheria nyengine yoyote. Lakini alisema Mwanasheria Mkuu kwa sababu ya wadhifa wake atakua kiongozi wa mawakili na atapewa nafasi ya kutangulia mahakamni katika mashauri yoyote anapohudhuria. Mhe. Marina alitaka kujua hii nafasi ya kutangulia ni ipi ni namna gani. Nafasi ya kutangulia katika sheria ni yule mtu ambaye ndio kama shekhe wa sheria au mkubwa wa sheria katika suala lile.

Kwa mfano hata msikitini au kwenye kanisa, kwenye kanisa atapokuja Padri basi sote tulioko huku tutaondoka tutampisha Padri kuendesha zile shughuli sawa sawa na msikitini, sote tulioko huku tutaondoka tutampisha shekhe ili aendelee na suala hilo. Kwa sababu ile heshima ambayo anapewa kutokana na nafasi yake aliyopewa kikatiba. Sasa tunaposema kwamba Mwanasheria Mkuu anapohudhuria mahkamani atapewa nafasi ya utangulizi ni kwamba kama kuna kesi na kuna wanasheria wa serikali ndio wanaoendesha kesi, sasa kutakuwa na kiongozi anaendesha kesi ile katika ile wanasheria lakini kwa bahati nzuri ikiwa mwanasheria anakwenda na yeye katika kesi ile, kwa hivyo yeye ndie atayepewa nafasi ya mwanzo katika shughuli zile na baadae watafuatia wale wengine. Hii ndio maana yake Mhe. Marina Joel.

Baada ya hapo Mhe. Hamza ninafikiri alipata majibu na Mhe. Mwanasheria Mkuu kwa hivyo sina haja ya kurejea tena lakini Mhe. Asha Bakari na yeye ninamshukuru kwa maelezo yake na alizungumzia kuhusu kifungu 22 ni kweli kuwa tunazipitia hizi sheria lakini ningelipenda niseme tu kwamba kuna *law review commission* ambayo hii iliyopewa jukumu la kupitia hizi sheria, hizi sheria ni nyingi kwa sababu ukitizama sheria zote tulizonazo kwa kweli ni za zamani sana, sasa kila moja inamshinda mwenzake. Kwa hivyo ni jukumu letu sisi kama kuna sheria ambayo tunahisi ni muhimu zaidi basi tunaweza tukawaandikia wale *law review commission* au hata ukapitia kwetu na sisi tutaipeleka kule ili iweze kupitiwa. Hivi sasa *law review commission* wameshashughulikia baadhi ya sheria zikiwemo sheria ya ushahidi ambayo ni ya zamani sana, sheria hii ya vileo ambayo nayo ilikuwa na matatizo makubwa na sheria nyengine ambazo wanazo wanaendelea nazo. Kwa hivyo tunayo Idara ambayo inashughulikia masuala haya.

Baada ya hayo Mhe. Spika, sasa naomba nijibu na suala moja ambalo lilibakia. Mhe. Ali Mzee alizungumzia na hapa nazungumzia Mhe. Salmin Awadh, Mhe. Ali Mzee na Mhe. Asha Bakari. Mhe. Ali Mzee alizungumzia mambo mawili. La kwanza alinivunja moyo kidogo aliposema kwamba hatoandika kitabu cha Baraza la Wawakilishi. Mimi nafikiri ninavyomjua Mhe. Ali Mzee atabadilisha uamuzi wake na sisi tungelimuomba aandike kitabu cha Baraza la Wawakilishi kwa sababu ninajua historia anayo kubwa katika masuala haya.

Lakini ningelimuomba tu katika kuandika kitabu hiki asije akawa kama Mhe. Aboud Talib maana yake Mhe. Aboud Talib wakati wa miaka 10 ya Sherehe za Baraza la Wawakilishi waliandika hiki kitabu lakini kwa kweli alipotosha. Nakuomba ukiandika kitabu hicho usipotoshe. Alipotosha kwa sababu waliandika kile kitabu na akapiga picha zile wakasema alokuwa Spika wa mwanzo wakamuweka uzuri, lakini hakuna katika 1980 mpaka miaka kumi ile mpaka 1990 hakuna aliyekuwa Katibu kwa mujibu wa kile kitabu. Kuna Spika wa mwanzo tu hakuna Katibu wa mwanzo ambacho si kweli, sasa usije ukapotosha kama hivyo.

Lakini la pili Mhe. Spika, ninalotaka kuzungumza ni suala hili la kusema kwamba kuwe na sheria maalum kuhusu yale yanayotaka kuelezwa kwa pamoja hasa katika mfumo huu wa serikali ya pamoja. Mimi nakubaliana nayo sana na suala hili yote haya yamo kwenye ripoti ya ziara ya mafunzo ya Uingereza na Ujerumani ambayo ilielezea kwa urefu sana. Ripoti hii nafikiri ilipelekwa serikalini na pengine hata Baraza la Wawakilishi ipo, ripoti hii kwa bahati iliandikwa na watu 9 akiwemo yeye Mhe. Ali Mzee, Mhe. Abdalla Ali Abdalla, Mhe. Mazrui, Mhe. Zakiya, Mhe. Abubakar na wengine waliokwenda ni Mhe. Ibrahim Mzee aliyekuwa Katibu, Mdungi Makame Msaidizi wake, Abdulhamid Yahya Mzee ambaye ni Katibu Mkuu Kiongozi, Khamis Mussa Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha na

Said Hassan ambaye hivi sasa ni Mwanasheria Mkuu. Ripoti ile ni nzuri tu na katika ripoti ile kuna viambatanisho, kimoja ni kiambatanisho ambacho ni azimio la Baraza la tarehe 28/1/2010 ambalo lilitolewa na Mwakilishi wa Mgogoni na kuungwa mkono na Wawakilishi wote.

Azimio hilo lilikuwa na mambo kumi na mbili baada ya kurekebishwa na Baraza na katika jambo la kumi lilisema kwamba kutakuwa na Kamati au ili-*propose* kuundwe kamati ya kusimamia utekelezaji wa masuala haya. Humu mimi nafikiri tukiipata ile ripoti tukiyaona hayo maazimio na tukipata yale yote ambayo yaliwekwa katika ripoti ile naamini inaweza ikatusaidia sana katika shughuli zetu. Basi si vibaya ripoti ile pengine kwa ridhaa ya Baraza ikagaiwa kwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu Mhe. Spika, ili waizingatie na kuifanyia kazi hiyo na mengi ya kuendeleza katika suala hili la serikali ya umoja wa kitaifa na umoja wetu, hilo ndio ninaloweza kusema katika suala hili Mhe. Spika.

Na suala la semina ambalo lilizungumzwa mimi nafikiri hili haliko sana katika Wizara ya Katiba na Sheria na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu, lakini kwa sababu hili ni jambo la serikali mimi nahisi Wawakilishi wana haki ya kufanya hivyo kwa kupitia pengine Ofisi ya Spika na Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais tungekubaliana tukafanya hilo ambalo litasaidia Wajumbe kuelimika na kujua hasa tunachotakiwa kutokana na ripoti ile na kutokana na utaratibu huo, na hapo ndio lile suala zima la kutunga sheria litakuja baada ya kufahamishana katika misingi hiyo.

Mheshimiwa baada ya kusema hayo napenda tena niwashukuru Wajumbe kwa maelekezo yao na yote tumeyachukua na tutaifanyia kazi sheria hii ili tuweze kuendeleza taifa letu. Baada ya hapo Mhe. Spika, naomba kutoa hoja.

(*Hoja ilitolewa iamuliwe)*
(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Spika, sasa naomba kutoa taarifa kwamba Baraza lako tukufu likae kama Kamati ya kutunga sheria ili kuupitia mswada kifungu baada ya kifungu.

KAMATI YA KUTUNGA SHERIA

Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Ofisi ya Mwanashera Mkuu Na Kuweka Utekelezaji wa Majukumu mwaka 2013

Sehemu ya Kwanza

Masharti ya Awali

Kifungu cha 1 Jina fupi na Kuanza Kutumika
Kifungu cha 2 Matumizi pamoja na marekebisho yake
Kifungu cha 3 Tafsiri pamoja na marekebisho yake
Kifungu cha 4 Kuanzishwa kwa Ofisi pamoja na marekebisho yake
Kifungu cha 5 Mwanasheria Mkuu

Mhe. Marina Joel Thomas: Mhe. Spika, kifungu namba 5 ambacho kinaeleza kuwa Mwanasheria Mkuu atakuwa kiongzi wa Mawakili. Suala langu nilimuuliza Mhe. Waziri nilitaka kujua hao mawakili ni wa binafsi au wa serikali, atakuwa ni kiongozi wa mawakili gani, alivyonijibu bado sijaridhika nalo.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Hii ni sheria ya serikali na tunazungumzia wanasheria wa serikali kwa hivyo watakuwa mawakili wa serikali.

Kifungu cha 5 Mwanasheria Mkuu
Kifungu cha 6 Uteuzi wa Naibu Mwanasheria Mkuu
Kifungu cha 7 Kazi za Naibu Mwanasheria Mkuu

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Mhe. Mwenyekiti nilipokuwa nikichangia kifungu hiki cha saba na nikazungumzia zaidi kifungu cha 7(2) ambapo mswada unazungumzia juu ya Mwanasheria Mkuu kuweza kutekeleza kazi zake na kutumia uwezo wa Mwanasheria Mkuu, lakini pia nikazumgumzia juu ya kwamba ili kuondosha masharti ya kifungu hiki hayatatafsiriwa kuwa yanamruhusu Naibu Mwanasheria Mkuu kumuwakilisha Mwanasheria Mkuu katika vyombo ambavyo Ujumbe wa mwanasheria mkuu katika vyombo hivyo umewekwa na Katiba. Kwa hivyo ninazungumzia zaidi huu uwezo ambao umewekwa kwa mujibu wa Katiba ambapo Mhe. Waziri wa Sheria alipokuwa anatoa ufafanuzi alielezea zaidi katika eneo hili ambapo Naibu Mwanasheria Mkuu hawezi kuingia katika chombo hiki kwa sababu ya katiba kuwa haikumruhusu.

Mimi nilipokuwa nikieleza *concern* yangu nilisema kwamba, pamoja na kwamba Katiba imezuia na imemtaja Mwanasheria Mkuu kwamba yeye atakuwa ni Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi na kaeleza kwamba, Mwanasheria Mkuu akubali tutakapofanya marekebisho ya katiba ili katiba sasa imruhusu na Naibu Mwanasheria Mkuu naye awe Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi. Kwa maana hiyo katiba nayo sasa itamke wazi kwamba Mwanasheria Mkuu na Naibu Mwanasheria Mkuu watakuwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi ili waweze kusaidiana katika shughuli hii ngumu na kubwa. Mhe. Mwenyekiti, zaidi ukizingatia hata mawaziri wanao wasaidizi wao manaibu mawaziri wanawasaidia wakati ule wanapofanya kazi. Pia nilieleza *practice* ambayo iko *live* tumeiona juu ya tukio kama hili la kutokuweza kufanya kazi kwa Mwanasheria Mkuu na hatimaye tukawa tuko *dilemma* hatujui tufanye nini.

Sasa kwa kuwa madaraka au vyeo hivi ni sisi wenyewe tunajipangia hatupangiwi na mtu, nilitaka Mhe. Waziri basi akubaliane na *concern* yangu hii kwamba, atakapofanya marekebisho ya katiba huko mbele basi jambo hili liweze kukubaliwa na kusiwe na kikwazo cha Naibu Mwanasheria Mkuu kuwa naye ni Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi kutokana na sababu hizo ambazo nimetangulia kuzisema.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Mwenyekiti, maelezo ya Mhe. Salmin Awadh ni sawa anayo mantiki yake mwenyewe binafsi, lakini hapa kuna mambo mawili ambayo napenda tuyatizame. Kwanza uingiaji wa Mwanasheria Mkuu katika Baraza ni katika nafasi zile ambazo si za uchaguzi na hii imewekwa moja moja kwa nafasi hizo. Sasa unaposema kwamba aingie na Naibu Mwanasheria Mkuu kwa misingi hiyo kwanza hilo ni suala ambalo mimi binafsi siwezi kuamu, ni suala la kiserikali na la ki-*policy*.

La pili ni kwamba ile mantiki hasa ya kusema kwamba awe na msaidizi wake akatoa mifano ya kwamba mawaziri kuna manaibu, lakini mfano huo haukuupeleka mbele kuna mawaziri ambao hawana manaibu kwa mfano Waziri wa Katiba na Sheria. Sasa hiyo si mantiki kubwa sana, lakini ninachopenda niseme ni kwamba bado sioni haja kwamba kuna ulazima kwa Naibu Mwanasheria Mkuu kuingia katika Baraza wakati Mwanasheria Mkuu yupo, na pale ambapo hatakuwepo kwa dharura basi *Cabinet* inafanya kazi *as a team work*, wana- *collective responsibility* atakuwepo Waziri wa Katiba na Sheria, atakuwepo pengine Mnadhim katika upande wa serikali na mawaziri wengine, hao wote wana wajibu wa kujibu hoja ile ambayo italetwa inayohusiana na mambo ya sheria.

Kwa hivyo, kwa mantiki hiyo Mhe. Mwenyekiti, nahisi kwamba bado hakuna haja ya kufanya Naibu Mwanasheria Mkuu awe na yeye ni Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi, na huu ndio utaratibu mwingi uliopo katika nchi nyingi za *Commonwealth*, Mwanasheria Mkuu tu ndiye anayeruhusiwa kuingia katika Bunge la kutunga sheria, wale manaibu wanakuwepo lakini wanakuwa nje ya lile bunge lenyewe na wanapohitajiwa misaada fulani basi wanatoa ushauri wao kwa njia hizi. Nakushukuru Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Mhe. Mwenyekiti, mimi nilikuwa nasikiliza mawazo ya Waziri wa Sheria juu ya hoja yangu hii. Lakini kinachoonekana kwamba ametoka ndani ya Bunge hili amekwenda kwenye mabunge mengine ya nchi za *Common Wealth*. Lakini mimi ninachotaka kusema kwamba kila wakati si lazima tuwaige watu wengine na sisi tufike pahala tuanzishe kitu watu watuige ili kuona kwamba Wazanzibari nao wamepitisha kitu cha msingi.

Hili suala la Mawaziri na Manaibu Mawaziri ni kama nilivyotangulia kusema kwamba mawaziri na manaibu mawaziri kwa *collective responsibility*, kwa hivyo waziri mmoja anapokuwa hayupo waziri mwengine anaweza akajibu kwa niaba ya serikali. lakini Mwanasheria yeye katika chombo hiki anatakiwa atoe *fat*-wa za kisheria. Bahati nzuri leo tunae Waziri wa Katiba na Sheria ambaye ni mwanasheria, lakini kipindi cha nyuma kilichopita mawaziri wetu wa sheria walikuwa si wanasheria na hata Rais hafungiki na hilo, leo Mhe. Abubakar Waziri wa Katiba na sheria, kesho akawa Waziri wa Afya hilo linakuwa halipingiki.

Kwa maana hiyo, tunaweza kuwa hatuna mshauri wa kisheria ndani ya chombo hiki, hatuzungumzii suala la kutoa au kujibu hoja tunazungumzia suala la Baraza hili kupata mshauri wa kisheria pale ambapo patatokea tatizo la kisheria na kutakiwa kutolewa ufafanuzi.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, naomba tuendelee.

Kifungu 7 Kazi za Naibu Mwanashieri Mkuu
Kifungu 8 Muundo wa Ofisi
Kifungu 9 Ajira ya Watumishi
Kifungu 10 Mawakili wa Serikali, Maafisa wa Sheria na Makarani wa Sheria
Kifungu 11 Kupangiwa kazi Mawakili wa serikali na Maafisa wa Sheria
Kifungu 12 Kuongezewa ujuzi

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, buti yangu hii si ya ukaidi isipokuwa ya kutaka ufafanuzi zaidi ili nielewe na wananchi wetu vile vile waweze kuelewa.
Mhe. Mwenyekiti, katika hii hoja ya kuongeza ujuzi ambayo niliizungumza juzi siku ya Ijumaa nilikuwa zaidi nataka nipate ufafanuzi. Mhe. Mwenyekiti, sasa hivi katika nchi yetu kufikia malengo ya *millennium Vision 2020* kuna harakati nyingi za kiuchumi, moja katika eneo ambalo tunajaribu kuliangalia sasa hivi ni eneo la kiuchumi katika sekta ya mafuta na gesi. Sasa hapa Mhe. Mwenyekiti, katika hiki kifungu cha 12 kinachozungumzia kuongeza ujuzi sasa je, sijui hapa labda Mwansheria au Mhe. Waziri wa Sheria anisaidie. Kwa mfano, tukija tukifanikiwa kuwa na uzalishaji wa aidha gesi au mafuta wanasheria wetu tuliokuwa nao wanaweza kuwa na uwezo wa kuweza kuingia mikataba mbali mbali na kusimamia zaidi hii rasilimali ili wasaidie wananchi au itabidi kuna wanasheria maalum ambao wanatakiwa waliobobea katika sekta hii.

Sasa hapa hoja yangu je, hawa wanasheria wetu wanaweza wakawa wanasheria katika eneo lolote au wanatakiwa katika maeneo maalum wawe na taaluma fulani hasa katika hii sekta ambayo naizungumza hapa. Kidogo nilikuwa nahitaji ufafanuzi ahsante.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Mwenyekiti, kama tulivyosema hapa kwamba wanasheria wetu itahitaji tuwaongezee ujuzi, lakini ujuzi huu ni kwamba hapa walipo hivi sasa wanazo wengine *degree* moja, mbili, lakini kwa shughuli kama hizi ni lazima uwe na watu ambao wamesomea kitu kimoja *specific.* Kwa mifano ambayo nimetoa suala la *mineral*, suala la mafuta *petroleum* hizo wako wanasheria hivi sasa wanao ujuzi wa *petroleum law* na *oil*, lakini kusema kwamba tutawaongezea ni vyema.

Kwa mfano, hata mafuta leo tukisema tuwe na suala hili la uchimbaji wa mafuta wanasheria hao wapo, lakini tulisema kwamba hii haitoshi kwa sababu suala hili pana, hivyo lazima tuwapate wanasheria wetu hawa ambao tutawapa ujuzi zaidi katika masuala mbali mbali, sio ya mafuta tu, lakini ya mikataba na mengine kama mambo ya ushahidi na kila ukimuongezea ujuzi ndio na sisi idara yetu inazidi kuwa idara nzuri na yenye uwezo zaidi. Kwa hivyo hayo Mhe. Mwakilishi tutajitahidi na tunaendelea kuyafanya kama tulivyosema.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nashukuru kwa kupata ufafanuzi huo na ninashukuru zaidi kwamba hata hiyo rasilimali ikipatikana kesho basi wanasheria tutakuwa nao. Lakini kitu ambacho nakiomba ni kwamba waboreshewe maslahi yao ili na hao tisa waliobakia wasije wakababakia saba. Ahsante.

Kifungu 12 Kuongeza Ujuzi na kutambulika
Kifungu 13 Bajeti na fedha za ofisi

SEHEMU YA TATU

Udhibiti na Utendaji Kazi na Utekelezaji Majukumu
Ofisi ya Mwanasheria Mkuu

Kifungu 14 Kazi za Ofisi
Kifungu 15 Haki ya Kufanya kazi kisheria na haki ya kusikilizwa
Kifungu 16 Uwezo wa Mwanasheria Mkuu na Ofisi
Kifungu 17 Mambo yanayohitaji uthibitisho wa Mwanasheria|Mkuu

Kifungu 18 Utaratibu wa kupata ushauri elekezi
Kifungu 19 Masharti ya kuhusiana na Mawakili wa Serikali na Maafisa wa Sheria Serikalini.
Kifungu 20 Maoni ya Mwanasheria Mkuu kwa msimamo wa Serikali
Kifungu 21 Usimamizi wa Kesi
Kifungu 22 Uandaaji haki za kisheria za serikali.
Kifungu 23 Uandishi wa Sheria
Kifungu 24 Usimamizi wa Mikataba

SEHEMU YA NNE

Kanuni za Maadili kwa Mawakili wa Serikali na Maafisa wa Sheria

Kifungu 25 Kanuni za Maadili
Kifungu 26 Adhabu kwa kukiuka kanuni za maadili pamoja na marekebisyo yake.
Kifungu 27 Tathmini za utendaji

SEHEMU YA TANO

Masharti ya Jumla

Kifungu 28 Kinga ya Maafisa
Kifungu 29 Mashirikiano na Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka
Kifungu 30 Mwanasheria Mkuu kuwa mchukuaji viapo.
Kifungu 31 Uwezo wa Waziri kutunga kanuni
Kifungu 32 Masharti ya mpito na kubakisha.

(Baraza lilirudia)

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Spika, ilivyokuwa Kamati ya Kutunga Sheria imeupitia mswada wangu kifungu kwa kifungu na kuukubali pamoja na marekebisho yake sasa naliomba Baraza lako tukufu likubali. Naomba kutoa hoja.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, maji na Nishati: Mhe. Spika, naafiki.

Mhe. Spika: Niwahoji Waheshimiwa Wajumbe wale wanaokubaliana na mswada pamoja na marekebisho yake wanyanyue mikono. Wanaokataa, waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mswada wa Sheria ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu (Utekelezaji wa Majukumu) ya 2013

(Kusomwa kwa mara ya tatu)

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Spika, naomba kutoa hoja kuwa Mswada wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu utekelezaji wa Majukumu ya mwaka 2013 usomwe kwa mara ya tatu.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe niwahoji wanaokubaliana na mswada katika kusomwa mara ya tatu wanyanyue mikono. Wanaokataa, waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

(Mswada wa Sheria ya Serikali ulisomwa mara ya tatu na kupitishwa)

Mswada wa Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti wa Matumizi ya Huduma ya Maji na Nishati Zanzibar ya mwaka 2013

(Kusomwa kwa mara ya Pili)

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe katika Mswada huu tulimaliza majadiliano na kazi iliyokuwa imebaki ilikuwa ni kupata semina. Ka hiyo imefanyika na mara baada ya semina ni kumuomba Mhe. Waziri kuja kufanya majumuisho. Basi ni wakati muwafaka sasa na naomba nimkaribishe Mhe. Waziri wa Ardhi, Makazi, Maji na Nishati ili kutoa majumuisho.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Spika, kwanza napenda kuchukua nafasi hii kukushukuru kwa kunikaribisha tena mbele ya Baraza hili tukufu kufanya majumuisho ya michango ya Wajumbe mbali mbali ambao walichangia katika wizara yangu wakati nilipowasilisha mswada huu nilipousoma mara ya pili.

Mhe. Spika, mswada umekwenda kwenye semina kama walivyoomba Waheshimiwa Wajumbe na kwa kweli semina ilikuwa ina shokomzoba nzuri sana kwa hivyo ilifanyika vizuri na nategemea tumeondoka pale tumeelewana vizuri kabisa kwenye masuala mbali mbali. Kwa hivyo, Mhe. Spika, kwanza napenda kuwatambua wale wote ambao walichangia kwenye mswada wangu kama hivi ifuatavyo:

1. Mhe. Marina Joel Thomas
2. Mhe. Makame Mshimba Mbarouk
3. Mhe. Abdalla Juma Abdalla
4. Mhe. Fatma Mbarouk Said
5. Mhe. Ali Salum Haji
6. Mhe. Salmin Awadh Salmin
7. Mhe. Asha Bakari Makame
8. Mhe. Hassan Hamad Omar
9. Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa
10. Mhe. Ismail Jussa Ladhu
11. Mhe. Abdi Mossi Kombo
12. Mhe. Mohammed Haji Khalid
13. Mhe. Mohammed Mbwana Hamad
14. Mhe. Saleh Nassor Juma
15. Mhe. Hamza Hassan juma
16. Mhe. Omar Ali Shehe
17. Mhe. Mussa Ali Hassan
18. Mhe. Hija Hassan Hija
19. Mhe. Jaku Hashim Ayoub
20. Mhe. Panya Ali Abdalla
21. Mhe. Mwanasheria Mkuu wa Serikali

Mhe. Spika, michango yao ilikuwa mizuri sana na baadhi ya hoja walizouliza zilipata majibu kwenye semina ile, kwa hivyo inaelekea tuliondoka vizuri pale na sasa labda niguseguse baadhi ya sehemu kidogo ambazo Waheshimiwa walizichangia.

Mhe. Marina Joel alitoa ushauri mzuri tu kwa niaba ya kamati yake ambao wa kutekelezwa na ofisi yangu. Mheshimiwa hilo tutajitahidi tutalitekeleza.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk yeye alitoa ushauri juu ya mamlaka kuwa huru iwe na maamuzi yake isiingiliwe na chombo chengine. Tunakubaliana na ushauri huo Mheshimiwa Spika.

Mhe. Abdalla Juma yeye alizungumza habari ya lugha na katika kuuandika vizuri mswada huu tutatizama lugha zikae vizuri kabisa ili ilingane katika maana tuliyoikusudia.

Hoja nyengine ilikuwa juu ya kifungu 10(1) juu ya leseni ya kuzalisha maji na mafuta ambayo haijatajwa. Majibu ya hoja ni kwamba kifungu cha 3(b) ni kwamba kinahusika uzalishaji, kwa hiyo leseni ya uzalishaji inapatikana katika kifungu hiki. Suala la mafuta kama tulivyozungumza juzi kwenye semina ni kwamba, kutakuwa na sheria yake maalum ambayo inasimamia utafutaji na uchimbaji wa uzalishaji mafuta *petroleum exploration production*.

Hoja ya kifungu cha 37 ambacho kifungu hiki kinalinda ushindani wa kibiashara, maadili, usalama na kuzuia kunufaika kwa mtumiaji anayepata taarifa hizo kuzitumia vibaya au kwa manufaa yake binafsi.

Hoja ya Kifungu 53 Mhe. Spika, baada ya kufanya utafiti juu ya hoja hii kifungu hiki sasa kitasomeka kuwa, ‘ikitokea mgogoro au mgongano, sheria za sekta husika zitatumika kwa vile sheria za sekta hizo ndizo zinazofanya kuwa kila sheria za sekta zinazohusika. Kwa sababu hii ikigongana na sheria ya ZAWA au sheria ya ZECO sheria itakayofanya kazi itakuwa ni hii ambayo tunaipitisha katika Baraza hili.

Mhe. Fatma Mbarouk Said yeye alizungumzia juu ya taarifa siri kuwekwa adhabu. Adhabu ipo katika kifungu cha 57(1). Hoja ya 58 kudhibiti viwango anahitaji ufafanuzi. Majibu ya kifungu hiki imekusudiwa kuwa viwango vya bei na si viwango vya ubora.

Mhe. Ali Salum Haji yeye alizungumzia kifungu cha 18 kiangaliwe zaidi. Majibu ushauri umepokelewa bila shaka. Hoja ya kifungu cha 28 kuongezwa kwa mujibu wa sheria za fedha, majibu ya hoja yamekubaliwa na hoja ya kifungu cha 40(3) maneno ‘amri nyengine’ anaona inafaa yatolewe ushauri umepokelewa. Kifungu hiki kinaonesha kwamba mamlaka ndio yenye jukumu la kutoa leseni ya mafuta, hivyo basi kutoa, kufuta au kupitia vibali itakuwa ni kazi ya mamlaka.

Hoja yake nyengine je, mamlaka itasimamia viwango vya bei? Mamlaka itatoa bei elekezi kwa taasisi au mtu anayetoa huduma za nishati na maji. Hoja ya kifungu cha 10 kinahitaji maelezo zaidi ina maana yakusafirisha umeme ndio maana yake kifungu cha 10(d).

Mhe. Salmin Awadh Salmin sifa za uteuzi wa Mkurugenzi kwa Mkurugenzi zipo nyingiwigo mpana amependekeza fani ya sheria na biashara zitolewe. Majibu ni kwamba uzoefu unaonesha kwamba, Mamlaka si lazima zisiwe na Mkurugenzi Mkuu mwenye sifa za shughuli za mamlaka husika. Kwa mfano, India Mamlaka ya Udhibiti inaongozwa na Mkurugenzi Mkuu ambae ana fani ya biashara. Hii inatupa wigo mpana wakumpata huyu Mkurugenzi ikiwa mwenye sifa moja itakosekana basi ya pili itatumika, ikiwa ya pili itakosekana ya tatu itatumika, ya tatu ikikosekana ya nne tutatumia, hivyo ndivyo tunavyofanya uteuzi katika kujaza nafasi zetu mbali mbali.

Hoja ya nane kunahitaji ufafanuzi. Majibu ya hoja usambazaji unahusisha uingizaji wa mafuta kutoka *deport* kwenda kwenye vituo vya petrol. Kifungu cha 21 kwa nini akaingia Waziri wa Fedha? Majibu ya hoja ni kwamba, kwa mujibu wa sheria ya Mtaji wa Umma Nam. 4 ya 202 ndio inayohusika na suala hilo la kumuweka Waziri wa Fedha.

Kifungu nambari 22(1) (a) - (d) Mhe. Spika, majibu ya hoja imekubaliwa. Kifungu nambari 31 Baraza la Wawakilishi watumiaji wa kifungu hiki hawajapewa uzito unaostahiki, majibu ya hoja ushauri umepokelewa.

Mhe. Asha Balari Makame sera ya nishati kuwa haijapitishwa na Baraza la Wawakilishi. Mhe. Spika, kwa kumbukumbu Mhe. Mjumbe Sera ya Nishati imeletwa katika Baraza hili mwezi Januari mwaka 2010 na kupata Baraka za Baraza hili.

Mhe. Mahmoud Mohammed Mussa hoja katika sheria hii hakuna utaratibu wa wanaochimba visima na utaratibu gani kuhusu kuchimba visima. Mhe. Spika, taratibu zote kuhusu uchimbaji wa visima ni sheria ya maji na sio ZURA. Sheria ya Maji kule inaeleza masuala hayo.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu hoja yake ni ya kifungu 22 ufafanuzi kuhusu 3% ya EWURA italipwa ZURA? Mheshimiwa ZECO hawalipi 3% kwa EWURA, mamlaka hii haifanyi kazi zake Zanzibar hivyo suala la mchango wa ZECO kwa ZURA utaletwa kwenye kanuni.

Mhe. Jussa pia alipendekeza jambo maana yake yeye alizungumza halafu pia akaleta michango kwa maandishi. Hapa ni kwamba yeye kifungu kimoja ambacho Mhe. Mwanasheria Mkuu alifanyia marekebisho kile cha mwisho cha 53 yale maneno ya mwisho Mhe. Mwanasheria Mkuu aliyaondoa ambapo ndio ilikuwa hoja ya Mhe. Jussa.

Pili, ilikuwa katika kifungu cha 9(f) ambayo ilikuwa kutunga kanuni na kuweka miongozo kwa sekta zinazoshughulikia huduma. Sasa hapa Mhe. Jussa alipendekeza kwamba kanuni na miongozo iwe kwa mujibu wa sheria hii, yaanihapa tuongeze maneno "kwa mujibu wa sheria hii".

Mhe. Mohammed Haji Khalid yeye alisema taasisi haina haja ya kuwa na msaidizi Mkurugenzi Mkuu. Majibu ya hoja kama ilivyofafanuliwa na Mwanasheria Mkuu kuwa serikali hii imeweka hakiba ikitokea haja ya kuwepo itakuwa hakuna haja ya kurekebisha sheria. Hoja ya kwamba kutakuwa na mgongano na mamlaka nyengine.

Mhe. Spika, yeye alitaka kujua suala la ushindani hizi taasisi mbili yaani ZECO na ZAWA zitashindana na nani? Mhe. Spika, mgombano utakuwa haupo kwa sababu kuna kifungu cha 53 tushazungumzia mgongano na sasa kwa sababu yeye anafikiria ZECO na ZAWA peke yake, lakini hii sheria inaruhusu kama alivyojibu Mwanasheria Mkuu watu wengine binafsi wakitokea kuanzisha taasisi zenye kutoa huduma hizi hapo ndipo ZAWA na ZECO watakapopata huo ushindani ambao unatakiwa. Mswada huu unaandaa mazingira ya kiushindani katika huduma kama alivyofafanua Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Muundo wa Bodi haujajitokeza katika sheria. Majibu ya hoja ni kwamba muundo wa bodi upo katika kifungu cha sita cha sheria hii.

Mhe. Hamza Hassan Juma tafsiri ya neno 'Mtu' anataka ufafanuzi. Kwenye semina juzi ufafanuzi wa mtu kibaolojia na mtu kisheria imefafanuliwa. Mtu kibaolojia maana yake ni mwanadamu na mtu kisheria hapa ina maana kampuni au taasisi iliyoanzishwa kisheria.
Kwenye eneo la huduma suala la gesi halijazungumzwa ikiwa ni sehemu ya nishati. Nishati kwa sheria hii maana yake inajumuisha umeme, mafuta na gesi na nishati nyengine zozote ambazo huzalisha umeme. Maelezo haya yamo katika karatasi ya marekebisho ya mswada wa ZURA ambayo Wajumbe wamepatiwa. Hata hivyo, kitaaluma tunapozungumzia mafuta *petroleum* maana yake ni mafuta na gesi. Kwa hivyo, ikitajwa *petroleum* basi zimetajwa zote mbili mafuta na gesi.

Hoja ya kifungu cha 3 kuwa huduma ya maji haipo itadhibitiwa vipi. Je, ZAWA akishindwa kutoa huduma ikikosa leseni ZURA atachukua hatua gani? Mhe. Spika, kama nilivyojibu juzi pale kwenye Baraza ni kwamba, serikali inajitahidi kuona kwamba huduma ya maji inapatikana kwa ukamilifu katika visiwa vyetu vya Unguja na Pemba. Kwa muhtasari ni kwamba, kwa upande wa Mkoa wa Mjini Magharibi naongeza miradi mikubwa na midogo midogo itapelekea kuongezeka kwa vianzio vya maji ili iweze kuwiana na mahitaji kwa wakati husika. Miongoni mwa miradi mikubwa ni ule mradi wa ukarabati miundombinu ADF12 unaofadhiliwa na Benki ya Maendeleo ya Afrika wenye thamani ya jumla ya US$ 21 milioni ambao utekelezaji wake utahusisha uchimbaji wa visima kumi vipya.

Halafu kuna na mradi wa uchimbaji visima 9 chini ya ufadhili wa serikali na ikiwa *Ras-el-Khaima* watathibitisha basi kwa Mkoa wa Mjini utapata visima vya ziada 15. Wizara kupitia mamlaka imepanga kuongeza mikakati maalum ya kupunguza idadi ya mabomba chakavu katika maeneo ya mjini kupitia mradi wa ukarabati miundombinu ADF12 kama nilivyokwisha kutaja mwanzo kwa maeneo ya Mji Mkongwe na sambamba na juhudi ya serikali ya kupitia wahisani wengine kwa miradi ya Mbweleo na Fumba.

Katika kukabiliana na kasi ya maji inayotokana na mabadiliko ya tabia nchi, serikali kupitia Mamlaka ya Maji imeanza na hatua za uchimbaji wa visima 9 katika eneo la Mkoa wa Mjini Magharibi zenye lengo la kuziba upungufu wa chemchem zetu mbili za Mwanyanya na Mtopepo.

Kwa upande wa Kusini Unguja katika jitihada za kuongeza vianzio vya maji, Mkoa wa Kusini Unguja ili iweze kuwiana na mahitaji kwa wakati husika kwa miradi mikubwa ni ule mradi wa maji safi na mazingira chini ya

ufadhili wa Benki ya Maendeleo ya Afrika unaohusisha na uchimbaji wa visima 6 na matangi makubwa 2 katika maeneo ya Machui na Mkorogo.

Mradi wa uchimbaji wa visima kutoka kwa ufadhili wa Jamhuri ya Watu wa China utakuwepo vile vile na ikiwa Ras el Khaima pia watathibitisha basi Mkoa wa Kusini utapata visima vyengine 14. Kwa upande wa Mkoa wa Kaskazini Unguja katika jitihada za kuongeza vianzio vya maji Mkoa wa Kaskazini ili viweze kuwiana na mahitaji kwa wakati husika, miongoni mwa mradi mkubwa ni ule mradi wa maji na mazingira chini ya ufadhili wa Benki ya Maendeleo ya Afrika unaohusisha na visima 4 na ujenzi wa matangi makubwa mawili katika maeneo ya Kwaishange Mkwajuni na Kindagoni, Fukuchani, mradi wa uchimbaji wa visima kutoka kwa wafadhili wa Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China pia utasaidia katika suala hilo na ikiwa Ras el Khaima nayo watathibitisha basi visima 8 vitaongezeka katika Mkoa wa Kaskazini Unguja.

Halafu Wizara kupitia Mamlaka inataka kuendeleza mkakati maalum wa kupunguza idadi ya mabomba chakavu katika vijiji vya maeneo ya mkoa huu kama ile ya mradi wa Mfenesini, Bumbwini Accra, Mkwajuni, Kaeshangwe na Matemwe pamoja na Chaani Kubwa, huu Accra ni jina la mradi ambao utashughulikia masuala ya kushughulikia mabomba hayo.

Mhe. Spika, kwa upande wa Mkoa wa Kaskazini Pemba. Katika mkoa huu wizara yangu imeweka mkakati wa kutengeneza miradi mbali mbali ili kuhakikisha kwamba huduma ya maji zinafikia maeneo hayo kwa kutumia fedha za ndani na washirika wa maendeleo.

Miongoni mwa mikakati hiyo ni utekelezaji wa mradi wa maji na usafi wa mazingira wa ADB ambao unaendelea hivi sasa kwa kazi ya ujenzi wa mji Wete pamoja na vijiji vya Kambini, Mchangamdogo, Shangafu, Piki, Bahanasa na Kisiwani. Kwa upande wa Wete mjini mradi utajenga matangi mawili, uchimbaji wa visima 8 vya maji na kwa upande wa vijijini mradi utajenga matangi 2 hapa Bahanasa.

Ikiwa Ras el Khaima watathibitisha basi matangi 5 yatajengwa katika mkoa huu pamoja na visima 4 katika mkoa huu.

Na mwisho Mkoa wa Kusini Pemba ni kwamba katika mkoa huu wizara yangu imeweka mkakati wa kutekeleza miradi mbali mbali ili kuhakikisha huduma ya maji inayafikia maeneo hayo kwa kutumia fedha za ndani na washirika wa maendeleo. Miongoni mwa mikakati hiyo ni utekelezaji wa mradi wa maji safi wa mazingira ambao unaendelea hivi sasa kwa ujenzi katika mji wa Chake-Chake na Mkoani pamoja na vijiji vya Wambaa, Ndagoni, Mizingani na Vitongoji, kwa upande wa mjini utajenga matangi manne ambayo matangi mawili yatajengwa katika kila mji.

Uchimbaji wa visima 6 vya uzalishaji maji kwa upande wa Chake-Chake ni visima vinne vya uzalishaji maji katika mji wa Mkoani. Kwa upande wa vijiji mradi utajenga matangi matano ambapo matangi mawili yatajengwa Vitongoji na tangi moja katika eneo la Wambaa, Mzingani na Ndagoni.

Mhe. Spika, hizi ni jitihada za serikali katika kuhakikisha kwamba maji yanapatikana katika maeneo mbali mbali na Mungu atujaalie tufanikiwe katika kutekeleza mikakati hii ili tuondoe tatizo la maji katika mji wetu.
Mhe. Hamza aliomba ufafanuzi wa vifungu ambapo ninafikiri jana ulifanyika ufafanuzi huo katika semina yetu mbali mbali.

Mhe. Spika, kuna Mhe. Omar Ali Shehe ambaye alitaka hoja kwamba kwa sheria hii ni agizo la Baraza la Wawakilishi ambalo limetolewa katika Tume ya Kuchunguza Shirika la Umeme. Ufafanuzi wa hoja kuanza kwa kutayarishwa kwa sheria hii, kulianza kabla ya Baraza kutoa agizo hilo wakati agizo linatolewa tayari mswada huu ulikuwa umeshafika katika vikao vya Makatibu Wakuu na ulikuwa tayari kwa ajili ya kufanyiwa kazi kuletwa katika Baraza la Wawakilishi.

Haina maana kwamba hoja ya Kamati imepuuzwa lakini huu ulitangulia kabla ya kuchomoza hiyo hoja ya Kamati. Kifungu cha 3 amesema kiweke fani ya ufundi ya utawala na nyengine zitolewe. Mheshimiwa huu ushauri tumeupokea lakini kama nilivyosema ukiwa na maeneo mengi ya kuchagua, maana yake ndio itakuwa rahisi kumpata Mkurugenzi wa kusimamia masuala haya.

Kifungu cha 7 sifa za Mwenyekiti. Majibu wa hoja ushauri umepokelewa lakini mara nyingi Mkurugenzi anakuwa ni mtu mzima kwa sababu anakuwa ni lazima awe na uzoefu wa kazi yenyewe, lazima awe ameshafanya kazi katika maeneo mbali mbali na hasa ya Utawala.

Vikao vya dharura viwekwe idadi kuondosha bodi. Hii itakuja kuamulia kwenye kanuni. Ni kweli tusiruhusu vikao vya dharura kufanyika ovyo ovyo vitakuwa ni vingi sana lakini kwenye kanuni ni lazima iwekwe angalau kwa mwaka wanaruhusiwa wafanya vikao vya dharura vingapi.

Mhe. Hija alitaka kujua ni wafanyakazi wangapi wamesomeshwa kupitia ufadhili wa Jumuiya ya Raslihema. Majibu ya hoja kifungu cha 3 kiongozwe maneno kwa kushirikiana na Afisi ya Mwanasheria Mkuu. Mhe. Spika, tunao mpango wa kusomesha watu katika masuala mbali mbali ya *Ras-el khaima* na mpaka hivi sasa...

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wanadhimu watanisaidia kuwaita Waheshimiwa Wajumbe waingie ndani. Mnadhimu mmoja anatoka ndani na wa pili atafanya hivyo hivyo.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Spika, mpaka sasa hivi watu watu tumewashawapeleka *Ras-el khema* kusoma lakini malengo yetu angalau tupate watu kumi tukasome elimu mbali mbali huko *Ras-el khaima*.

Mhe. Spika, pamoja na wajumbe wengine waliochangia naomba kuwashukuru Wajumbe wote katika michango yao mbali mbali kwenye sheria hii na mategemeo yetu tutakwenda kuifanyia kazi na inshaallah Mwenyezi Mungu akipenda itakuwa ni sheria nzuri na ni sheria itakayolinda kabisa mambo yetu haya ya kudhibiti masuala ya maji, umeme na mambo mengineyo.

Nafikiri haya malalamiko yanayotoka Baraza la Wawakilishi yamekuwa marefu sana kuhusu matatizo ya maji, na wakati mwengine maji machafu, wakati mwengine huduma ya maji haipatikani vizuri. Sasa haya yote tunaunda chombo sasa, huyu ndio mtu wa kupokea malalamiko yote yanayozungumzwa katika Baraza hili, hiki chombo cha ZURA.

Baada ya hayo Mhe. Spika, naomba kutoa hoja.

(Hoja imetolewa iamuliwe
(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

KAMATI YA KUTUNGA SHERIA

Sehemu ya Kwanza
Utangulizi

Kifungu 1 Jina fupi na kuanza kutumika
Kifungu 2 Ufafanuzi pamoja na marekebisho yake

Sehemu Ya Pili
Muundo Na Utawala Wa Mamlaka

Kifungu 3 Kuanzishwa kwa Mamlaka
Kifungu 4 Muundo pamoja na marekebisho yake
Kifungu 5 Kuanzishwa kwa Bodi
Kifungu 6 Muundo na Muda wa Bodi pamoja na marekebisho yake
Kifungu 7 Sifa za Mwenyekiti
Kifungu 8 Uwezo Maalum wa Mamlaka katika sekta ya petrol pamoja na marekebisho yake
Kifungu 9 Kazi za Mamlaka pamoja na marekebisho yake
Kifungu 10 Leseni
Kifungu 11 Uwezo wa jumla wa Mamlaka
Kifungu 12 Viwango na ada
Kifungu 13 Majukumu ya Bodi pamoja na marekebisho yake

Kifungu 14 Uwezo wa Bodi
Kifungu 15 Kumalizika muda
Kifungu 16 Katibu
Kifungu 17 Vikao vya kawaida
Kifungu 18 Vikao vya dharura
Kifungu 19 Akidi
Kifungu 20 Shughuli za Bodi pamoja na marekebisho yake
Kifungu 21 Maslahi

Sehemu yaTatu
Vifungu Vya Fedha

Kifungu 22 Fedha za Mamlaka
Kifungu 23 Bajeti
Kifungu 24 Hesabu na Ukaguzi
Kifungu 25 Ripoti ya mwaka

Sehemu ya Nne
Uwajibikaji wa Mamlaka

Kifungu 26 Kutunza daftari la umma
Kifungu 27 Uwazi
Kifungu 28 Kanuni za maadili ya utedaji
Kifungu 29 Siri
Kifungu 30 Mgongano wa maslahi
Kifungu 31 Baraza la kuwakilisha wateja pamoja na marekebisho yake
Kifungu 32 Majukumu na uwezo wa Baraza
Kifungu 33 Fedha za Baraza
Kifungu 34 Mikutano ya umma
Kifungu 35 Ushindani

Sehemu ya Tano
Utatuzi Wa Migogoro

Kifungu 36 Malalamiko

Sehemu ya Sita
Makosa na Adhabu

Kifungu 37 Kutoa taarifa
Kifungu 38 Taarifa za utafiti
Kifungu 39 Makosa yaliyochanganywa
Kifungu 40 Makosa ya jumla

Sehemu ya Saba
Rufaa

Kifungu 41 Kurejewa kwa hesabu
Kifungu 42 Upya
Kifungu 43 Rufaa

Sehemu ya Nane
Masharti Mengineyo

Kifungu 44 Uwezo wa Waziri

Kifungu 45 Mipango na Uwekezaji
Kifungu 46 Huduma zinazodhibitiwa na zinazohitaji leseni
Kifungu 47 Kinga dhidi ya kushtakiwa
Kifungu 48 Kanuni
Kifungu 49 Maazimio
Kifungu 50 Mwenendo
Kifungu 51 Kufuta Sheria za kisekta
Kifungu 52 Kubakisha
Kifungu 53 Sheria itakayotumika pamoja na marekebisho yake

(Baraza lilirudia)

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Spika, ilivyokuwa Kamati ya Kutunga Sheria imepitia mswada wangu kifungu baada kwa kifungu na kukubali pamoja na marekesho yake, sasa naliomba Baraza lako tukufu liikubali. Naomba kutoa hoja.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mswada wa Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti wa Matumizi ya Huduma ya Maji na Nishati Zanzibar 2013

(Kusomwa kwa mara ya Tatu)

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Spika, naomba kutoa hoja kwamba Mswada wa Mamlaka ya Kudhibiti Huduma ya Maji na Nishati Zanzibar 2013 usomwe kwa mara ya tatu.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Spika naafiki

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

(*Muswada wa sheria ya serikali ulisomwa mara ya tatu na kupitishwa)*

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe niwashukuru tena kwa kazi nzuri muliyoifanya asubuhi hii kwa mpigo kwa kupitisha miswada miwili, basi tunaendelea.

Mswada wa Sheria ya Kurekebisha Sheria mbali mbali na mambo mengine yanayohusiana na hayo

(Kusomwa kwa mara ya Pili)

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Spika, kwanza naomba kuchukua fursa hii kukushukuru kwa kunipa fursa hii ya kuwasilisha hoja ya mswada huu wa marekebisho mbali mbali na mambo yanayohusiano na hayo.

Pili naomba kuchukua fursa hii kuishukuru Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala kwa mashirikiano na miongozo waliyotupa katika kujadili mswada juu kwenye ngazi ya kamati ambayo yamesaidia sana kuufanya mswada huu kuwe mzuri zaidi.

Mhe. Spika, mswada huu unakusudia kurekebisha sheria nne zifuatazo.

1. Sheria ya Mahakama ya Kazi Nam. 2 ya 1994,

2. Sheria ya Udhibiti wa kodi za nyumba Nam. 3 ya 1987,

3. Sheria ya Mahakama Kuu Nam. 2 ya mwaka 1985

4. Sheria ya Shirika la Biashara ya Taifa (ZSTC)

Mhe. Spika, sheria mbili za Mahakama na udhibiti wa kodi za nyumba zinarekebishwa ili kwenda sambamba na mageuzi ya utendaji wa Mahakama. Katika juhudi hizo Mahakama inakusudia kuimarisha utendaji kwa kuanzisha baadhi ya divisheni za Mahakama Kuu na Mahakama maalum (Tribunal) ili kushughulikia kesi na mashauri maalum.

Mhe. Spika, kwa vile divisheni ya Mahakama maalum zitakuwa ni sehemu ya utandaji wa kawaida ya Mahakama. Imeonekana haja ya Majaji dhamana wa Mahakama hizo na wenyeviti na makamo wao wa hizo Mahakama maalum kupangiwa kazi kwa utaratibu wa ki-Mahakama badala ya kuwa chini ya uteuzi wa Rais ili kurahisha utendaji.

Mhe. Spika, uteuzi wa wakuu hao unapofanywa na Rais, divisheni hizo zinaonekana kama ni vyombo nje ya Mahakama.
Aidha inapotokea dharura uteuzi wa kaimu viongozi hao unachukua muda mrefu bila ya sababu maalum.

Mhe. Spika, kwa sababu hizo iwapo marekebisho haya yatapitishwa na mamlaka ya uteuzi yatarudi mikononi mwa Jaji Mkuu kwa kushauriana na Tume ya Utumishi ya Mahakama.

Mhe. Spika, sheria nyengine itakayorekebishwa ni Sheria ya Shirika la Biashara ya Taifa. Madhumuni ya marekebisho hayo ni kuufanya muundo wa bodi wa Shirika la Taifa la Biashara (ZSTC) uende sambamba na sheria za mitaji ya umma Nam. 4 ya mwaka 2002 ambao unaweka masharti ya msingi ya kuzingatiwa katika muundo wa mashirika ya umma.
Mhe. Spika, mswada huu umegawika katika sehemu nne.

Sehemu ya kwanza inahusiana na jina fupi na kuanza kutumika kwa sheria ambazo zinafanyiwa marekebisho hayo. Sehemu ya pili inahusiana na marekebisho ya sheria ya Mahakama ya Kazi Nam. 2 ya 1994 na sehemu ya tatu inahusiana na marekebisho ya sheria ya udhibiti wa kodi za nyumba, marekebisho Nam. 3 ya mwaka 1987 na sehemu ya nne inahusiana na marekebisho ya sheria ya Mahakama Kuu Nam.2 ya 1985.

Sehemu ya tano inahusiana na marekebisho ya sheria ya Shirika la Biashara la Taifa Nam. 11 ya mwaka 2011 ambapo kama nilivyotangulia kusema kwamba yanahusiana zaidi na muundo wa bodi ili uendane sambamba na sheria ya mitaji ya umma.
Mhe. Spika, ninaamini Waheshimiwa Wajumbe watakubaliana na mimi kwamba marekebisho haya ni muhimu kwa ajili ya kuimarisha usimamizi wa sheria chini ya Mahakama na pia kwa ajili ya utendaji wa Shirika la Taifa la Biashara (ZSTC) ambalo tumelipa kazi muhimu ya kusimamia mbali ya zao la karafuu lakini na mazao mengine ya kilimo kwa ajili ya kuleta ufanisi.

Kwa hivyo Mhe. Spika, nimalizie kwa kuwaomba Waheshimiwa Wajumbe wayapitie marekebisho haya na baadae waunge mkono hoja tuweze kufanya marekebisho ili tuweze kuleta ufanisi katika utendaji wa taasisi hizo ambazo zimetajwa kwenye mswada huu.

Baada ya kusema hayo Mhe. Spika, naomba kutoa hoja.

(Hoja imetolewa iamuliwe)

Mhe. Ali Abdalla Ali (Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala): Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba niwasilishe hotuba ya maoni ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala kuhusu mswada wa Sheria ya marekebisho mbali mbali na mambo mengine yanayohusiana na hayo.
Mhe. Spika, sifa njema zinamstahikia Mwenyezi Mungu ambaye ametujaalia kuwa hapa tukiwa na afya njema na kunipa nguvu za kusimama mbele ya Baraza lako tukufu kuwasilisha hotuba ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala kuhusu mswada wa marekebisho wa sheria mbali mbali na mambo yanayohusiana na hayo.

Mhe. Spika, kwa niaba ya kamati naomba nikushukuru wewe binafsi kwa kuniruhusu kusimama mbele ya Baraza lako tukufu niwasilishe taarifa ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala juu ya mswada huu muhimu.

Mhe. Spika, aidha ninampongeza Mwanasheria Mkuu na watendaji wake wote wa afisi hii kwa mashirikiano makubwa waliyotupa wakati tukiujadili mswada huu.

Mhe. Spika, kwa mujibu wa kanuni wa Baraza la Wawakilishi toleo la mwaka 2012 kifungu cha 83(5) ambacho kinasomeka kama ifuatavyo, "Kamati inayopelekewa mswada kwa mujibu wa kanuni hii inaweza kuwaalika mtu yeyote afike kutoa maoni yake mbele ya kamati hiyo kwa lengo la kusaidia na kuchambua mswada huo kama inavyohusika".

Kwa ujumla vifungu hivi vinatoa fursa kwa aliyealikwa au mdau wa sekta husika katika kutoa maoni yao yanayohusiana huu husika. Kamati ilifanya hivyo kama kanuni ilivyoelekeza ambapo wadau wa sekta mbali mbali kwa mujibu wa sheria zinazorekebishwa katika mswada huu walifika na kutoa maoni yao kuhusiana na mswada huo.

Kwa msingi huo Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala inapenda kutoa shukurani zake za dhati kwa wadau wote walioshiriki kutoa maoni yao ambao wameisaidia sana kamati katika kufanya marekebisho haya.
Mhe. Spika, ninapenda pia kuwashukuru Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati yangu ya kudumu ya Baraza la Wawakilishi ya Katiba, Sheria na Utawala kwa umakini wao wakati wa kuchambua mswada huu na kuujadili.

Mhe. Spika, naomba niwatambue wajumbe hao kwa kuwataja kama ifuatavyo:-

1. Mhe. Ali Abdalla Ali - Mwenyekiti
2. Mhe. Panya Ali Abdalla - Makamo Mwenyekiti
3. Mhe. Ismail Jussa Ladhu - Mjumbe
4. Mhe. Mussa Ali Hassan - Mjumbe
5. Mhe. Suleiman Hemed Khamis - Mjumbe
6. Mhe. Wanu Hafidh Ameir - Mjumbe
7. Mhe. Mohamedraza Hassanali - Mjumbe
8. Ndg. Latifa Saleh Suleiman - Katibu
9. Ndg. Abubakar Mahmoud - Katibu

Mhe. Spika, kwa kweli serikali hii ya awamu ya saba yenye muundo wa umoja wa kitaifa imepanga kuhakikisha kuwa itazifanyia marekebisho sheria zote zilizopitwa na wakati pamoja na zile ambazo hazitekelezeki kipindi uwezo unapopatikana.

Hizi ni miongoni mwa harakati za serikali za kupitia Afisi ya Mwanasheria Mkuu kuhakikisha utawala bora unapatikana ili na sisi tuwe katika viwango vya kimataifa.

Mhe. Spika, katika mswada huu wa sheria marekebisho ya sheria mbali mbali na mambo mengine yanayohusiana na hayo inajumuisha sheria nne ambazo:

1. Sheria ya Mahakama ya Kazi ya Nam. 2 ya 1994
2. Sheria ya Udhibiti wa Kodi ya Nyumba Nam. 3. ya 1987
3. Sheria ya Mahakama Kuu Nam. 2 ya 1985
4. Sheria ya Shirika la Biashara la Taifa Nam. 11 ya 2011.

Lengo kuu ni kuleta ufanisi katika utekelezaji wa sheria hizo.

Mhe. Spika, Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala inaunga mkono vifungu mbali mbali vilivyorekebishwa katika miswada hiyo kwani inasaidia kuondoa usumbufu kwa watendaji pamoja na wananchi kwa jumla.
Mhe. Spika, baada ya maelezo haya ya awali, sasa naomba uniruhusu ili niweze kutoa maoni ya kamati kuhusu mswada huo uliopo mezani ambao tunaoujadili hivi sasa.

Mhe. Spika, hotuba hii ya maoni ya kamati inagusa tu baadhi ya maeneo ambayo kamati yetu ilihisi kuwa hayabudi kuyatolea maelezo. Maeneo hayo ni kama yafuatayo. Kuongeza neno " za nyumba" katika jina la sheria linalofanyiwa marekebisho na isomeke sheria ya Udhibiti wa Kodi za Nyumba, marekebisho Nam. 3 ya 1987.

Na katika kifungu cha 5 mstari wa kwanza kiongezeke neno "(3) na (5) baina ya 6 (1) na cha neno linarekebishwa liliopo baina ya neno "mama na kwa" lisomeke linarekebishwa.

Mhe. Spika, kimsingi katika mswada huu hakujajitokeza marekebisho mengi kwani mswada ulikuwa ni mfupi na umekamilika kiufundi. Hivyo nawaomba Waheshimiwa wenzangu Wajumbe wote wa Baraza hili wauchangie mswada huu kwa madhumuni ya kuimarisha zaidi na hatimaye kukubalika nakuupitisha.

Mhe. Spika, kwa niaba yangu na kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Mfenesini tunaunga mkono mswada huu na ninashukuru kwa kunipa nafasi na ninakushukuruni kwa kunisikiliza. Naomba kuwasilisha.

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti kwa kuwasilisha na wakati huo huo Mwanasheria Mkuu ananiarifu kuwa mapendekezo ambayo yaliyowasilishwa, kwa hivyo kama hajagaiwa kwa Wajumbe ninadhani yangegaiwa ili Wajumbe wapate kuyasoma kwa pamoja katika michango yao kwenye huu mswada, watendaji wale.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Spika, mimi kwanza ninataka niendele tena kutoa shukurani kwa Afisi ya Mwanasheria Mkuu wa Zanzibar kwa kuendelea kuboresha sheria zetu mbali mbali ambazo nyengine zimepitishwa kwa miaka mingi na nyengine hata ambazo zilizopitishwa hivi karibuni ili ziweze kwenda na wakati, lakini vile vile ziweze kwenda na matakwa ya demokrasia ya hivi sasa.

Mhe. Spika, pili ninataka niwapongeze wasaidizi wa Mhe. Mwanasheria Mkuu kwa sababu kama tunavyofahamu Mwanasheria Mkuu ana kazi nyingi, ana majukumu mengi. Kuna mengi ambayo aliyorithi ambayo anatakiwa ayaweke sawa hasa yale yaliyokuwa yana matatizo. Lakini kwa umahiri wa wasaidizi wake kwamba yale mambo ambayo mara nyingi tunashauri Barazani, basi tunashukuru sana kama mambo mengi hivi sasa yanaendelea kutatuka.

Na ninataka niseme kwamba kazi hii tuliyomtwika Mwanasheria Mkuu sio kazi ndogo, ni kazi kubwa, mahitaji na matakwa ya demokrasia na utawala bora yamekuwa mengi hivi sasa na yanakuja kwa nguvu kubwa. Sasa ni vizuri vile vile na afisi hii ninazidi kuwashauri wajitahidi kama nilivyozungumza mwanzo kwenye mswada uliopita Mwanasheria Mkuu kuwajenga kitaaluma wanasheria wake, lakini vile vile kuwatengenezea mazingira ya kimaslahi ili waweze kufanya kazi zao kwa utulivu.

Mhe. Spika, katika kazi ngumu hapa duniani ni kazi ya sheria, ya kusimamia sheria za nchi. Sasa wanasheria wetu hawa tunapokuwa hatujawaboreshea maslahi yao na mazingira yao ya kazi, kwa hivyo kwa kweli inakuwa ni mtihani mkubwa. Wanaweza wakaja kuturipulia ripulia kazi, matokeo yake serikali ikapata hasara au matatizo.
Lakini ninaamini baada ya kupitishwa mswada ambao tulioupitisha hivi karibuni, ninaamini hivi sasa Mhe. Mwanasheria Mkuu ataweza kuandaa bajeti nzuri ili sasa waweze kufanya kazi kwa kuletea marekebisho ya sheria mbali mbali kama hii iliyokuja hivi sasa.

Mhe. Spika, mswada huu ni mdogo sana wa marekebisho ya sheria. Lakini unahitaji umakini mkubwa sana, kwa sababu hakuna kitu moja kwa moja ambacho tunajadili sheria moja. Tunajadili mapitio ya sheria mbali mbali na marekebisho ya sheria mbali mbali. Pamoja na kwamba ni mfupi, lakini kuna mambo kidogo nitataka na mimi nishereheshe kwa kiasi fulani.

Mhe. Spika, nilipoangalia kifungu cha 3 katika hii sehemu ya pili ya mswada, marekebisho ya sheria ya mahakama ya kazi nambari 2 ya mwaka 1994. Kifungu cha 3 marekebisho ya kifungu cha 4(1) cha sheria mama kinafutwa badala yake kuwekwa kifungu kipya kama kifuatacho, naomba nikinukuu
Kifungu cha 14(1) kinasema;

"Mwenyekiti wa mahakama ambaye atateuliwa na Jaji Mkuu kwa ushauri wa Waziri baada ya kushauriana na tume ya utumishi ya mahakama kutoka miongoni mwa Majaji wa Mahakama Kuu".

Mhe. Spika, mimi nafurahia sana marekebisho haya, na kimsingi mara nyingi ninapokuwa nachangia huwa najaribu sana kuzungumzia kumpunguzia majukumu. Maana yake wakati mwengine huwa kuna lugha tunaitamka, sasa unajua wengi sisi sio wanasheria. Kwa hivyo, wanaposikia unazungumza lugha ya kumpunguzia madaraka Rais wanahisi kama unampunguzia nguvu za uwezo wa kiutendaji.

Lakini Mhe. Spika, kimsingi madhumuni hasa kumpunguzia majukumu, ili abakie na yale majukumu kidogo ya msingi ambayo ataweza kuyasimamia vizuri na haya majukumu mengine kwa kuwa kuna watu amewateua, nadhani kutokana na umakini wa wale aliowateua ataweza kuteua watu wa kuweza kusaidia kuendesha hizi shughuli na kwa kweli huu ndio utawala bora unavyotaka.

Sasa Mhe. Spika, hapa kama ilivyozungumzwa hapa kuna sehemu ya pili inahusiana na marekebisho ya sheria ya mahakama ya kadhi nambari 2 ya mwaka 1994, kwamba badala ya Mwenyekiti wa Mahakama hiyo kuteuliwa na Mhe. Rais kama ilivyokuwa awali, badala yake atateuliwa na Mhe. Jaji Mkuu. Sasa hii kama ilivyoelezwa kwamba wakati mwengine tunashuhudia kuna taasisi ambazo moja kwa moja zinataka uteuzi wa Mhe. Rais na wakati mwngine inachukua muda mrefu. Kwa mfano kama bodi au kamisheni ya aina yoyote, inafika pahala inamaliza muda wake. Kwa hivyo inaweza ikachukua pengine karibu mwaka mzima, na kwa kuwa katika hizi mamlaka kuna mamlaka moja hailazimishwi wala haishurutishwi kufanya kitu fulani. Lakini sasa kutokana na majukumu inakuwa wakati mwengine inachukua muda mrefu kuweza kupata uongozi katika taasisi husika.

Sasa ndani ya kipindi hiki Mhe. Spika, kunaweza kukatokezea mambo mengi ambayo inakuwa hakuna chombo cha kuweza kusimamia kuweza kusuluhisha lile jambo. Sasa hii kidogo Mhe. Spika, inainyima demokrasia nafasi yake, vile vile inakwaza shughuli nyengine. Wakati mwengine mpaka ile taasisi ikishateuliwa inabidi sasa waanze kuchukua kazi nyingi za nyuma ili kuweza kuzifanyia kazi mpaka kuweza kuendana na ile hali halisi au kwenda na wakati.

Mhe. Spika, kwa maamuzi haya ya Afisi ya Mwanasheria Mkuu kuleta mswada huu wa kusema kwamba huyu mwenyekiti wa mahakama ambaye alikuwa ateuliwe na Rais, sasa ateuliwe na Jaji Mkuu. Haya ni maamuzi ya busara sana. Juzi nilipokuwa nikizungumzia uteuzi wa wakurugenzi nikasema kwamba sasa hivi hebu hizi nafasi zitangazwe. Nilipata ufafanuzi kwamba haya mambo katika utawala bora ndio inavyotakiwa, lakini bado mapema tustahamili. Lakini mimi nashukuru angalau kuna maeneo mengine tumeanza.
Unajua Mhe. Spika, hamu ni mbaya sana, hamu wakati mwengine kila kitu unataka kufumba na kufumbua kiwe, lakini kila kitu kinakwenda na taratibu zake, na kwa sababu huwezi ukafanya jambo ambalo litakuwa halina mpango maalum. Kama alivyosema Mhe. Mwanasheria Mkuu alinitolea ufafanuzi, nilifahamu sana siku ile. Alisema kwamba haya mambo yanataka yaende kwa taratibu na kuwekwe sheria madhubuti ambazo zitakazokuwa kama muongozo kwa serikali nzima, isiwe huku wanateuliwa na Rais, huku wanaomba na huku hivi. Kwa hivyo, nafikiri na hilo wataalamu wake katika ofisi yake kwa kushirikiana na yeye mwenyewe, naamini wanaanza kulifanyia kazi. Lakini nilipoona kifungu hiki kimewekwa, kwa kweli nikaona kwamba kweli tunaweza tukabadilika kidogo kidogo ili mambo yetu yaende vizuri.

Mhe. Spika, kuna sehemu nyengine ambayo ninataka kuizungumzia inahusu sehemu ya tatu ambayo inahusiana na marekebisho ya sheria ya udhibiti wa kodi nambari 3 ya mwaka 1987, kwamba badala ya mwenyekiti wa mahakama hiyo kuteuliwa na Mhe. Rais kama ilivyokuwa hapo awali, badala yake atateuliwa na Jaji Mkuu. Suala hili sina haja ya kulisherehesha sana kwa sababu linalingana na hii sehemu ya pili ya mswada huu.

Suala la tatu ambalo nataka kulizungumzia linasema kwamba sehemu ya nne ambayo inahusiana na marekebisho ya sheria ya mahakama kuu nambari 2 ya mwaka 1985 kwa kuongeza kifungu kipya kifungu kidogo cha (2) ambacho kinatoa nafasi kwa mahakama kuu kuweza kutanuka na kuwa katika mgawanyo, yaani *division* tofauti.

Mhe. Spika, katika jambo ambalo litaweza sana kutusaidia kuondoa manung'uniko na malalamiko ya wananchi wetu wengi ni hiki kifungu ambacho tunategemea kukipitisha hivi sasa. Kutoa *loophole* kwa mahakama kuu kuweza kuongeza yale matawi yake katika usimamizi. Katika hili Mhe. Spika, mimi naomba sana Afisi ya Mwanasheria Mkuu, kuna eneo maalum katika hivyo vitengo vitakavyotanuliwa kwa mahakama kuu basi la mwanzo liangaliwe hili la mahakama ya ardhi. Mhe. Spika, tumekuwa na tatizo kubwa. Hivi sasa mahakama ya ardhi iko chini ya

Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati, wananchi wanalalamika sana na kulalamika kwao kwanza mahakama yenyewe ina uchache wa mahakimu.

Mhe. Spika, kuna baadhi ya wananchi wana mizozo yao ya maeneo yao ya uwekezaji, inafika pahala mtu tangu ameandika *write up* anataka kwenda kutafuta *loan* sehemu, au anakwenda kutafuta mkopo kwa ajili ya kuwekeza. Pengine katika eneo lake kwenye sekta mfano ya utalii. Lakini kutokana na kwamba wanatokezea baadhi ya wajanja wachache wanakwenda mahakamani kuzuia, matokeo yake kesi unaweza ukaikuta inachukua miaka miwili haijapatiwa ufumbuzi, nenda rudi, nenda rudi. Mhe. Spika, kwa kweli katika eneo ambalo tunapata malalamiko sana kwa wananchi ni eneo hili.

Mhe. Spika, na mahakama hii vile vile kuweko chini ya Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati pia inakuwa sio busara. Kwa sababu kama tunavyofahamu Mhe. Spika, tuna *separation of power*. Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati ni serikali, mahakama ya ardhi iko pale juu ya Wizara ya serikali vile vile, wanaofanya makosa ni watendaji wa ardhi, wanakwenda kuhukumiwa katika mahakama ya wizara ya ardhi. ndio maana hapa wakati mwengine hata wale wananchi huwa wanakuwa na chembe chembe za kukosa imani, sio kwamba hawana imani ya mahakama kwamba haina uwezo. Lakini je, kweli hapa haki itatendeka.

Mhe. Spika, mimi kwa kupitia sheria hii au marekebisho haya, basi Mhe. Mwanasheria Mkuu katika eneo la mwanzo la kuliondoa katika kutanua vile vitengo vya mahakama kuu, basi mahakama ya ardhi irudi iwe chini ya mahakama kuu, ili haki iweze kutendeka. Lakini sio irudi chini ya mahakama kuu tu Mhe. Spika, lakini vile vile kuongeza majaji katika mahakama hii.
Mhe. Spika, na lazima Mhe. Mwanasheria Mkuu ingawa nalo hili na yeye atakua hana uwezo sana wa kuweza kulilazimisha, lakini vile vile suala la uharakishaji wa hizi kesi, haswa hizi kesi ambazo zimeshachukua muda mrefu. Hili ni jambo ambalo nategemea Mhe. Mwanasheria Mkuu, tukisha kukubali kumpitishia na kumuidhinishia sheria hii ikishapita, basi mimi naamini suala hili ataweza kulifanyia kazi ili shughuli za wananchi ziweze kwenda kwa vizuri.

Mhe. Spika, hii ya mwisho kabisa ambayo ni sehemu ya tano, ambayo ina marekebisho ya sheria ya Shirika la Biashara la Taifa sheria nambari 11, ambayo kwa muundo wa bodi iliyokuwepo awali unabadilishwa hasa katika idadi ya wajumbe na kuhakikisha kwamba unakwenda sambamba na sheria zilizopo.

Mimi nadhani Mhe. Spika, katika marekebisho haya ya hii sheria ya Shirika la Biashara, huku kuna wale wajumbe ambao watateuliwa na Waziri, katika kifungu cha 9(1)(c) kuna mjumbe mmoja ambaye atateuliwa na waziri, miongoni mwa katika taasisi zifuatazo za kushauriana na taasisi husika. Wizara inayohusika na biashara, wizara inayohusika na fedha na wizara inayohusika na kilimo.

Mhe. Spika, mimi nadhani hivi sasa wakati umefika wa kuwashirikisha zaidi wadau, yaani *private sector* katika hizi bodi mbali mbali. Mhe. Spika, ili taasisi zetu au ili mashirika yetu yaweze kwenda vizuri, basi ni lazima sasa hivi katika hali ya uwazi, ni lazima basi ile hali ya utatu ionekane kabisa. Hii nazungumzia kwa sababu mara nyingi bodi zetu zimekuwa zikiwashirikisha watu wengi wa taasisi za serikali na wale watu wa nje, mara nyingi pengine Waziri yeye mwenyewe kwa fikra zake na kwa uono wake anaweza akamteua mtu ambaye yuko nje ya serikali. Lakini kwa kupitia sheria hii mimi nahisi kwamba huyo mjumbe mmoja atakayeteuliwa na Waziri miongoni mwa kila taasisi zifuatazo kwa kushauriana na taasisi husika. Mjumbe mmoja kutoka jumuia ya wakulima wa karafuu Unguja. Sasa hapa labda nije kufafanuliwa, kwa sababu hapa mjumbe imekusudiwa kwa hiki kifungu cha 9(2) katika huu muundo wa bodi, (c) itakuwa mjumbe mmoja au atakuwa mjumbe mmoja mmoja, kwa sababu huku imeelezwa atakuwa mjumbe mmoja ambaye atateuliwa na Waziri miongoni mwa kila taasisi katika taasisi zifuatazo kwa kushauriana na taasisi husika.

Lakini huku katika kifungu cha (c) (4) kinasema mjumbe mmoja kutoka katika jumuia ya wakulima wa karafuu Unguja na mmoja kutoka katika wakulima wa karafuu Pemba. Sasa hapa imekusudiwa mjumbe mmoja au mjumbe mmoja mmoja. Kwa sababu kama mjumbe mmoja basi ina maana huku tayari wameshakuwa wajumbe wawili. Lakini kama mjumbe mmoja mmoja, basi hapa itakuwa kuna makoseo, labda nije nisaidiwe marekebisho.

Vile vile hapa nataka niulize Mhe. Spika, Shirika la Biashara kwa kuwa linahusika na biashara moja tu ya karafuu ndio maana wakaingizwa wale wajumbe wa wakulima, au hili shirika linaweza likajaribu kuangalia uwanja mpana wa kutafuta mjumbe mwengine, au Waziri akapewa nafasi pengine tatu ili huyu mjumbe mwengine awe yeye moja

kwa moja kwa uelewa wake wa biashara mbali mbali. Kwa sababu unaweza ukawaingiza wajumbe katika hizi jumuia za wakulima wa karafuu. Wao kitu kikubwa watakachokijua ni uzalishaji wa lile zao la karafuu. Lakini hatuwezi kutafuta mjumbe mwengine ambaye anatoka *chamber of commerce*, ambaye yeye atasaidia kutoa mawazo ya kuboresha katika utafutaji wa masoko wa hizo karafuu. Kwa sababu unaposema wakulima tu, wao wataangalia tupatiwe mbegu, tupatiwe pembejeo, tupatiwe madawa lakini ule utaalamu au taaluma au uzoefu wa kufanya biashara watakuwa hawana na hili ni shirika la biashara.

Sasa kama ni shirika la biashara basi ni vizuri vile vile tukamuongezea uwezo Mhe. Waziri, ukiacha hawa wajumbe kutoka katika jumuia za wakulima wa karafuu wa Unguja na Pemba, lakini pia tumpe uwezo mwengine wa kuweza kumteua mjumbe kutoka Jumuia ya wafanyabiashara wa Zanzibar, yaani *chamber of commerce*. Kwa sababu wale wanapokaa katika mikutano yao na wanashiriki katika mikutano mbali mbali ya kimataifa, ambayo wanaweza kujaribu kutoa ushauri ni namna gani serikali yetu iweze kuboresha au iweze kujitahidi kutafuta masoko ambayo yatakuwa na uhakika, ya ushindani zaidi ili kuimarisha bei ya zao hili la karafuu.
Mhe. Spika, kwa kweli kama nilivyozungumza mwanzo, mswada huu unahitaji uchune ubongo kweli kweli, ili uweze kupata hoja za kuweza kuchangia na ndio maana nikaweza kusimama, nikasema angalau na mimi nitoe michango yangu miwili au mitatu. Lakini vyenginevyo ningesema tu kwamba napongeza na tuendelee. Mhe. Spika, pamoja na hayo ni lazima sisi tupate ile taaluma. Kwa sababu Mhe. Spika, Mhe. Mwanasheria Mkuu anapotusaidia maelezo sisi pia anawasaidia maelezo na wananchi wetu wengine ambao wanaangalia katika shughuli hii. Kwa hivyo, naamini wale wenzangu marafiki zangu wajumbe wa *chamber of commerce*, naamini haya mawazo niliyoyatoa ya kumpa mamlaka Waziri kumuongezea mtu mwengine atoke katika *chamber of commerce*, mimi nafikiri watakuwa wanayaunga mkono sana. Naamini Mhe. Mwanasheria Mkuu kwa kushauriana na Mhe. Waziri anayeshughulikia masuala ya zao la karafuu watakubaliana na hoja yangu hii.

Baada ya hayo machache Mhe. Spika, nakushukuru sana kwa kuweza kunipa nafasi hii. Kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Kwamtipura, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja, ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Spika: Ahsante sana, kuna dakika kama kumi tu, sijui kama kuna mjumbe ambaye atazitumia hizo. Namuona Mhe. Ali Salum Haji.

Mhe. Ali Salum Haji: Mhe. Spika, na mimi nikushukuru kwa kupata nafasi hii ya kuweza kuchangia mswada huu wa sheria ya mabadiliko ya sheria mbali mbali. Mhe. Spika, nimpongeze Mhe. Mwanasheria Mkuu kwa dhati kabisa kwa kuleta mabadiliko haya ya sheria mbali mbali. Kwa kweli ni jambo zuri na kimantiki ukiangalia hasa ni kweli kwamba sheria zetu nyingi zimepitwa na wakati, kuna haja ya kufanya marekebisho ili kuweza kupata ufanisi wa kazi katika maeneo mbali mbali.

Mhe. Spika, mimi nilikuwa nina mambo kama matatu baada ya kutoa pongezi kwa mwanasheria. Jambo la kwanza Mhe. Spika, nilikuwa nataka niende katika kifungu cha tano. Hapa nimpongeze mwanasheria kwa kuangalia baadhi ya sheria ambazo zitaweza kupunguza urasimu wa Mhe. Rais, kama alivyoeleza katika kifungu hiki kwa uteuzi kwamba sheria mama zinarekebishwa kwa kufutwa neno “Rais” na baadae kwamba kuna uteuzi wa Jaji Mkuu. Kwa hivyo, nimuombe Mhe. Mwanasheria Mkuu kwamba kuna haja kama alivyofanya marekebisho katika kifungu hiki, ya kuangalia baadhi ya sheria nyengine na kuweza kumshauri Rais na kupunguza nguvu zake.

Ni kweli majukumu ya Rais ni mengi na kama tutamuachia Mhe. Rais kufanya uteuzi katika kila pahala, basi baadhi ya maeneo tunaweza kukosa ufanisi na baadhi ya kazi tukaharibikiwa. Kwa sababu tuna maeneo mengi tu ambayo huwa tunapata madhara kwa kumsubiri Mhe. Rais kufanya uteuzi na muda unakuwa ni mrefu, kwa sababu hata hivi karibuni Mhe. Spika, naweza kusema kwamba tulimsubiri Mkurungenzi wa Manispaa kwa muda mrefu na taasisi hii sasa hivi imekubwa na matatizo mengi. Sasa kama kuna baadhi ya maeneo kama haya tutawapa mamlaka wale watu ambao wameteuliwa na Rais ili kuteua zile kurugenzi ndogo ndogo, nafikiri kutakuwa kuna haja nzuri na jambo zuri kuweza kuondosha majukumu yale ya Mhe. Rais, kumpunguzia angalau yale majukumu madogo madogo ambayo tunahisi yanaweza kutatuka katika maeneo mengine.

Jengine Mhe. Spika, ambalo nataka kulichangia na limenipa mashaka ni kifungu cha 7(2), ambacho kinasema;

Kifungu cha 7(2)

“Mahakama kuu inaweza kutanuliwa katika mgawanyo tofauti”.

Hapa na mimi nishukuru kwa migawanyo ambayo itatanuliwa, kama alivyozungumza mwenzangu Mhe. Hamza Hassan Juma, ni kweli mahakama zimezidiwa na kazi, kesi zinachukua muda mrefu, kadhia zinakuwa nyingi na wananchi wanalalamika katika mienendo mizima ya kisheria ya mahakama, ni jambo zuri. Lakini jambo ambalo linanipa mashaka Mhe. Spika, nataka Mhe. Mwanasheria kidogo anisaidie ni hii lugha iliyotumika hapa kwamba mahakama kuu inaweza.

Mhe. Spika, mimi sio mwanasheria na Kiswahili changu kinanipa ugumu. Kitu inaweza ni kitu ambacho nahisi ni neno ambalo halina nguvu. Hata kama utaangalia katika madhumuni na sababu Mhe. Spika, kwamba huku imetumika lugha ya Kiswahili nyengine, sasa sijui lugha hizi zitakuwa zinaoana au nguvu zake kisheria zitakuwa sawa sawa. Kwa sababu huku inasomeka inaweza, lakini katika madhumuni na sababu imezungumzwa kwamba mahakama kuu huwezi kutanuka. Sasa huku inaonesha moja kwa moja kwamba inawezeshwa kutanuka, lakini huku naona kama lugha kidogo haina nguvu. Hili neno 'ina' sijui Mwanasheria Mkuu katika kamusi la Kiswahili hii ina anaweza kuja kutufafanulia Kiswahili fasaha katika neno hili.

Jengine Mhe. Spika, ambalo nakata nilizungumzie ambalo limenipa mashaka sana kwa namna ambavyo limeshuka hili suala. Katika kifungu cha 9, naomba ninukuu Mhe. Spika.

Kifungu cha 9(2)

"Kifungu kidogo (2) na kifungu cha 13 cha sheria mama kinafutwa na kuweza kuwekwa badala yake kifungu kipya kama ifuatavyo;

(2) Itakuwa na Mwenyekiti ambaye anateuliwa na Rais, Mkurugenzi mwendeshaji na mjumbe mmoja ambaye atateuliwa na Waziri miongoni mwa kila taasisi katika taasisi zifuatazo, kwa kushauriana na taasisi husika

(i) Wizara inayohusika na biashara
(ii) Wizara inayohusika na fedha
(iii) Wizara inayohusika na kilimo
(iv) Mjumbe mmoja kutoka katika jumuia ya wakulima wa karafuu Unguja na mmoja kutoka jumuia ya wakulima wa karafuu Pemba

Mashaka yangu Mhe. Spika, ni hii hali halisi iliyojitokeza hapa na sifikirii kama bodi zetu zote ndivyo zinavyoundwa. Mara nyingi bodi zetu zinavyoundwa Mhe. Spika, tunaona kwamba hazitaji maeneo maalum, huwa zinataja tu kama wajumbe wawili au ingetuambia tu kwamba wajumbe wawili ni wakulima wa karafuu. Lakini tunapoanza kuzungumzia mjumbe mmoja kutoka Unguja, mjumbe mmoja kutoka Pemba. Sasa sijui na hizo sheria zetu nyengine ambazo zinakuwa zinataja wajumbe wa bodi kwa sifa kama hizi nazo zitakuwa zinaendelea kuanza kuainisha maeneo vile vile. Kwa sababu tuna bodi nyingi na bodi zinakuwa zinataja tu kwamba kutakuwa kuna wakandarasi wawili, lakini haisemi labda hao wakandarasi wawili mmoja kutoka Pemba na mmoja kutoka Unguja. Halafu hapa nataka nisaidiwe kwamba huyu mjumbe ambaye atateuliwa kutoka Unguja.

Kwa mfano Mhe. Spika, mjumbe mmoja kutoka Unguja kama tayari atakuwa keshateuliwa mjumbe wa bodi, lakini kinadharia kama atahamisha makazi yake kutoka Unguja kwenda Pemba ule ujumbe wake utafutika *automatic*, kwa sababu tayari itakuwa sio mkaazi wa Unguja, keshakuwa ni mkaazi wa Pemba moja kwa moja.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, hili mimi nilitaka nisaidiwe na Mhe. Mwanasheria Mkuu, ile sababu halisi waliyoona kuainisha hii mjumbe mmoja kutoka Pemba na mjumbe mmoja kutoka Unguja. Kwa sababu nina hofu kuna mambo mengi ambayo tunayaanzisha, inawezekana leo na kesho tukaja kuanzisha bodi nyengine hapa za mwani na kadhalika, je itaangalia eneo maalum kwamba labda kwa sababu mwani unalimwa Jambiani basi na mjumbe wa bodi labda ni lazima atoke Jambiani. Mimi nahisi ni vyema Mhe. Spika, labda Mhe. Mwanasheria Mkuu angetuwekea moja kwa moja kwamba wajumbe wawili ambao watatoka katika jumuia ya karafuu, ilikuwa haina haja ya kuainisha baina ya Pemba na Unguja, vyenginevyo Mhe. Spika, kutakuwa kuna haja basi na bodi nyengine nazo tukaangalia katika hali kama hii ambayo Mhe. Mwanasheria Mkuu ametueleza.

Mhe. Spika, baada ya hayo nishukuru kwa dhati na niunge mkono hoja sheria hii ya mabadiliko mbali mbali ya sheria. Ahsante.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe ninawashukuru kwa kazi kubwa tuliyoifanya leo kuanzia asubuhi. Sasa muda unakaribia tukapumzike ili tuje jioni kuendelea na kazi. Nimeombwa niwatangazie Waheshimiwa Wajumbe

wanawake, kwamba yale mafunzo yao yapo chumba kile kile kama kawaida mara tu tukitoka humu ndani, kwa hivyo muendelee na shughuli hiyo.

Basi baada ya hayo Waheshimiwa Wajumbe niakhirishe kikao hiki hadi saa 11:00 jioni leo.

(Saa 7:00 mchana Baraza liliakhirishwa hadi saa 11:00 jioni)

(Saa 11:00 jioni Baraza lilirudia)

(Majadiliano Yanaendelea)

Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa: Mhe. Spika, ahsante sana kwa jioni hii ya leo na mimi kunipa fursa ya kuweza kuchangia mawili matatu juu ya Mswada wetu huu wa Marekebisho ya Sheria ya Kurekebisha Sheria mbali mbali na Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo.

Mhe. Spika, napenda kuchukua fursa hii pia kuishukuru Ofisi ya Mwanasheria Mkuu pamoja na watendaji wote ikiongozwa na yeye mwenyewe kutokana na mswada huu wa kitaalamu ambao siku ya leo ametuletea hapa.

Mimi kwa upande wangu kwanza kabisa nilikuwa na maombi maalum. Mhe. Spika, tunaomba Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wanapotaka kufanya mabadiliko ya sheria, yaani vifungu vya sheria, basi tunaomba ile sheria mama iliyokuwa ikitumika wakati ule atusaidie kutuletea, ili tuweze kujua yatokanayo ilikuwa iko vipi, pale tunapofanya kazi hii ya kuchangia basi tuifanye kwa ufanisi zaidi. *(Makofi)*

Vile vile Mhe. Spika, mimi kwa upande mwengine nataka kuzungumzia hiki kipengele cha saba sehemu ya nne kifungu cha 3(1) cha sheria mama kilichorekebishwa na kuongeza kifungu chengine kipya cha 2 mara tu baada ya kijifungu kidogo cha (c) cha kifungu cha 3(a) kama ifuatavyo. Mahakama Kuu inaweza kutanuliwa katika migawanyo tofauti.

Mhe. Spika, hii ni hatua ya maendeleo na mimi nichukue fursa hii kumshukuru sana Mhe. mwanasheria Mkuu pamoja na watendaji wake kwa kuliona hili la kutanua mahakama zetu, ili tuweze kupunguza msongamano wa kesi ambazo zinakusanyika katika mahakama zetu na zikawa zinachukua muda mrefu mno na hili ni jambo la busara sana.

Katika kulikamilisha hili Mhe. Spika, tunaomba utaratibu huu zaidi ufike pia kwenye Mahakama za Ardhi ambako kuna mtihani mkubwa wa kesi ambazo ni za muda mrefu tena ni nyingi ambapo zinachelewa kupata ufumbuzi na kuweza kutoa muongozo mzuri, ili matatizo ambayo yamejilimbikiza pale yaweze kupungua.

Jambo la pili Mhe. Spika, napenda kufanya marekebisho kidogo sehemu ya tano kifungu cha 9(c) naomba kunukuu kidogo Mhe. Spika.

Kifungu cha 9(c) kinaeleza hivi:-

> "Mjumbe mmoja ambaye atateuliwa na Waziri miongoni mwa"…

Mhe. Spika, hili neno *miongoni mwa* linapotosha tafsiri sahihi ya hii sentensi yetu. Kwa hivyo, tunamuomba Mhe. Mwanasheria Mkuu kupitia kwako Mhe. Spika, tukubaliane kwamba hili neno miongoni mwa liondoke na badala yake iwe mjumbe mmoja ambaye atateuliwa na Waziri kila taasisi zifuatazo kwa kushauriana na taasisi husika, naomba tufanye marekebisho hayo.

Nikiendelea na mchango wangu kwenye madhumuni sehemu ya tano inayohusiana na Marekebisho ya Shirika la Biashara la Taifa Nam. 11 mwaka 2011, ambapo muundo wa bodi uliokuwepo awali unabadilishwa hasa idadi ya wajumbe, ili kuhakikisha kwamba unakwenda sambamba na sheria zilizopo.

Sasa Mhe. Spika, kila bodi zinazokuja zinakuja na miundo yake na sisi ule muundo wa mwanzo ambao uliokuwa umepitikana kule hatuujui wengine. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Mwanasheria Mkuu kupitia kwako Mhe. Spika, wakati atakapokuja hapa atusaidie kutuelekeza na ule muundo wa mwanzo ulikuwa vipi, ili tuweze kukubaliana na kipengele hichi tukipitishe bila ya matatizo yoyote.

Baada ya maelezo hayo Mhe. Spika, mimi mwenyewe binafsi pamoja na wananchi wa Jimbo la Kikwajuni naunga mkono hoja hii baada ya kupata ufafanuzi wa mambo hayo, ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Mhe. Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii jioni ya leo kutoa mchango wangu juu ya Marekebisho ya Sheria mbali mbali pamoja na mambo mengine yanayohusiana na hayo, ambayo Mhe. Mwanasheria Mkuu ametuletea.

Kwanza nichukue nafasi hii kumpongeza kwa kuona haja ya kufanya marekebisho ipo, baada ya kuanza sheria hizi ambazo nyengine ni za muda mrefu na nyengine tumezipitisha juzi. Lakini baada ya utekelezaji tumeona ni vyema tukafanya marekebisho katika baadhi ya vifungu.

Mhe. Spika, sheria hizi ambazo Mhe. Mwanasheria Mkuu amezileta mbele yetu kama zilivyo kwamba ni Sheria ya Mahakama ya Kazi ya mwaka 1994 sheria Nam. 2 na Sheria ya Udhibiti wa Kodi na Sheria ya Mahakama Kuu na Sheria ya *ZSTC* kuna vifungu mbali mbali ambavyo Mhe. Mwanasheria Mkuu ametuletea.

Mwenzangu Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa ameeleza hapa kwamba jambo zuri sana na linaweza kupunguza hoja kwa Waheshimiwa Wajumbe ambapo pale Mhe. Waziri anapotuletea *matrix* zile ambazo zitaonesha vifungu vilivyokuwepo mwanzo katika sheria fulani na vilivyorekebishwa, pengine hata kama na sababu zile za kufanya marekebisho nadhani ingekuwa jambo jema. Lakini bila ya kufanya hivyo inakuwa inatupa shida kwa kweli na itafika pahala sasa tutake kujua vile vifungu vinavyofutwa vinasemaje na sababu ya kufutwa ili tujiridhishe.

Kwa sababu Mhe. Spika, sheria hizi tunazitunga sisi hapa na tunatunga kutokana na mahitaji yaliopo na kwa wakati uliopo. Lakini inapotokea serikali au mtekelezaji wa zile sheria anahisi azifanyie marekebisho basi ni vyema tukawa tunaambiwa zile sababu na vifungu vyenyewe vilivyo. Kwa sababu tunaona hali ilivyo si rahisi Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi wakaanza kwenda kuingia *library* kuzitafuta hizo sheria.

Mimi hili Mhe. Spika, nimekuwa nikilisema sana kabla ya hata hili kuja na nikaonesha uzoefu wangu kwa wenzetu Wabunge juu ya jambo hili. Na kwa sababu nimeshawahi kushiriki kule Dar es Salaam wakati tulipokuwa tukifanya marekebisho ya Sheria ya *BoT*, tulipata nafasi ya kwenda hapa tukaonana na Kamati basi wameweka utaratibu mzuri kwa hivyo hakukuwa na matatizo tuliweza kurekebisha.

Sasa na hili nalo kwa siku zinazokuja Waheshimiwa Mawaziri wanapofanya marekebisho katika sheria mbali mbali kama hizi ni vyema ikawa vile vifungu vinavyorekebishwa vikaoneshwa kwanza vilikuwa vinasemaje na baadae vionekane vinasemaje.

Kuhusu marekebisho ya Sheria ya Mahkama ya Kazi Nam. 2 ya mwaka 1994, Mhe. Spika, Mahkama ya Kazi ipo kwa mujibu wa sheria na ni Mahkama ambayo inahitaji kuangaliwa na kwa makini sana. Kwa sababu kumekuwa na malalamiko mengi sana yanayohusiana na wafanyakazi wenyewe na wamekuwa na malalamiko mbali mbali juu ya namna wanavyokuwa *treated* katika maeneo yao ya kazi na jinsi Mahkama hizi zinavyochukua hatua juu ya wafanyakazi.

Kwa kweli mwenendo wa Mahkama hizi hautupi moyo na inafika pahala tunakuwa na dhana japokuwa dhana ni mbaya, hata dini yetu ya Kiislamu inakataza dhana. Lakini tunafika pahala tunakuwa na dhana na hii inatokana na vyombo vyetu hivi ambavyo vimewekwa kwa ajili ya kushughulikia wafanyakazi na matatizo mbali mbali hasa yanayohusu wafanyakazi na sehemu za kazi.

Sisi kama Wawakilishi wa wananchi tumekuwa tukipokea malalamiko mengi juu ya wafanyakazi, juu ya wanavyoendeshwa hasa katika maeneo ya sekta binafsi, jambo ambalo linawafanya wananchi wetu kuona kwamba ajira katika sekta binafsi sio ajira. Mtu anaweza kuwa anafanya kazi katika sekta binafsi kama hoteli ukimuuliza unafanya kazi gani atakwambia mimi sina kazi. Lakini kumbe kwa wenzetu huko kwenye nchi nyengine ajira katika sekta binafsi ndizo zenye nguvu na ndizo zenye maslahi mazuri, lakini kwa kuwa sisi hapa wafanyakazi hasa katika sekta binafsi hawashughulikiwi basi wanaiona kama vile si ajira.

Mhe. Spika, mkuu katika sehemu yake au kampuni anaweza kumfukuza tu mfanyakazi na anamwambia hivi hivi hakuna chochote nenda kokote, nenda Mahkamani nenda wapi na hakuna lolote. Mhe. Spika, haya ni mambo ambayo kwa kweli Mahkama hizi za Kazi zinatakiwa zishughulikie sana maeneo haya.

Mhe. Spika, katika marekebisho Nam. 2 ya Sheria ya Kazi ya kifungu cha 64 inazungumzia kifungu cha 14(1) cha sheria mama kinafutwa na kuwekwa badala yake kifungu kipya kama ifuatavyo. Mhe. Spika, imeelezwa hapa na Mhe. Mwanasheria Mkuu amakieleza hapa, ambapo Mhe. Spika naomba nikinukuu kidogo hapa.

Kifungu cha 14(1) kinaeleza hivi:-

> "Mwenyekiti wa Mahakama ambaye atateuliwa na Jaji Mkuu kwa ushauri wa Waziri na baada ya kushauriana na Tume ya Utumishi ya Mahkama kutoka miongoni mwa Majaji wa Mahakama Kuu".

Mhe. Spika, sasa kitasomeka hivi. Lakini kama nilivyotangulia kusema Mhe. Spika, kwamba hicho kilichofutwa kilikuwa kinasemaje na kwa nini vikabadilishwa, kulikuwa na kasoro gani ya hicho kifungu cha mwanzo cha sheria Nam. 2 kifungu Nam 14 hadi ikafikia pahala sasa ikabidi tuandike upya na mabadiliko hayo yametokana na nini.

Kwa hivyo, namuomba Mhe. Mwanasheria kupitia kwako Mhe. Spika, basi wakati atakapokuja kufanya majumuisho atupe kwa muhtasari na tujue hiki kifungu kinachofutwa na kwa nini kifutwe na hiki kinachofutwa kinasemaje.

Eneo jengine ni sehemu ya tatu ya marekebisho haya. Marekebisho ya Sheria ya Udhibiti wa Kodi, ambapo kumefanywa masahihisho kidogo, badala ya kuishia Mdhibiti wa Kodi paongezwe neno Kodi za Nyumba, yaani Sheria Nam. 3 ya mwaka 1987.

Sasa kuna kifungu hapa ambacho kimefanyiwa marekebisho ambapo kinaeleza na hapa naomba kunukuu kidogo Mhe. Spika.

Kifungu cha 6(1) kinaeleza hivi:-

> "Kwenye marekebisho ya mswada kumeandikwa vifungu vya 6(1), (3) na (5) vya sheria mama vinarekebishwa na kufuta neno "Rais" liliopo mara tu baada ya kifungu cha maneno "atateuliwa na" na kuweka badala yake kifungu cha maneno Jaji Mkuu kwa kushauriana na Tume ya Utumishi ya Mahakama".

Mhe. Spika, mimi unaponiambia kodi za nyumba najua kodi inakusanywa na *ZRB*, mimi ninavyofahamu mdhibiti wa kodi, yaani kodi ambazo zinakusanywa na *ZRB*. Kwa kweli kuna sheria tulipitisha hapa inayohusiana na kodi za nyumba ambazo zinakusanywa na *ZRB*. Lakini nilipochangamkia zaidi ni pale ambapo nimeona kuna masuala ya Jaji Mkuu kwa kushirikiana na Tume ya Utumishi ya Mahkama na neno Rais linafutwa na badala yake kutakuwa Jaji Mkuu.

Sasa Mhe. Mwanasheria Mkuu namuomba kupitia kwako Mhe. Spika, kifungu hichi basi ni vyema akatupa kile kifungu cha mwanzo ambacho kulikuwa na neno Rais na sasa tunamuweka Jaji Mkuu kwa kushauriana na Tume ya Utumishi wa Mahkama, kwamba kifungu kile kilikuwa kinasemaje na mpaka kufikia pahala sasa tukamnyang'anya mamlaka Rais ya kuteua na kumuachia Jaji Mkuu.

Vile vile eneo jengine Mhe. Spika, ni sheria ya Mahkama Kuu, ambayo ni Sheria Nam. 2 ya mwaka 1985. Eneo hili lina marekebisho mawili ya kifungu cha 3(1), ambapo kinasema kifungu cha 3(1) cha sheria mama kinarekebishwa kwa kuongezwa kifungu kipya cha 2 mara tu baada ya kifungu kidogo cha (c) cha kifungu cha 3(1) kama ifuatavyo. Halafu inasema kifungu hicho kidogo cha 2 kinasema Mahkama Kuu inaweza kutanuliwa katika migawanyo tofauti.

Mhe. Spika, tumeongeza hapa kifungu kidogo cha 2 baada ya kijifungu kidogo cha (c), ambacho kimeongezeka neno na hapa patakuwa na sababu ya kuongeza, ambapo Mahkama Kuu inaweza kutanuliwa katika migawanyo tofauti. Sasa kutanuliwa huku kukoje, kwa sababu sisi tunajua Mahkama Kuu ya Zanzibar ni moja, kwa hiyo tunapoitanua Mahkama Kuu hii, basi tunahitaji tupate ufafanuzi kwamba tunaitanua vipi, ili hizi Mahkama Kuu ziweze kufanya katika mgawanyiko tofauti na hilo nalo linahitaji ufafanuzi Mhe. Spika.

Mbali ya hiyo kwenye mtiririko wa namba 6,5,6,7 kuna (7) moja ambayo iko kwenye *bracket*, sasa hii imekosewa au kuna na vifungu chengine cha 7(1) pengine kwenye sheria hiyo kuna 7(1), (2) na (3).

Kwa hivyo, na hapa Mhe. Mwanasheria Mkuu namuomba kupitia kwako Mhe. Spika, wakati atakapokuja kutoa ufafanuzi kwamba hichi kifungu kinachofanyiwa marekebisho kifungu cha 3(1), yaani kuna utangulizi wa 1 na mimi nilifikiri hizi namba 4,5,6,7 ni namba zile, lakini kuna 1 imetangulia na hii 1 kidogo imenipa mashaka, pengine inawezekana ikawa ni *typing error*, kwa hiyo ni vyema akatupa ufafanuzi wa hii 1 ambayo imetangulia hapa mbele.

Mhe. Spika, sheria ya mwisho ambayo tunaifanyia *amendment* ni Sheria ya Shirika la Taifa *ZSTC* sheria ya Nam. 11 ya mwaka 2011, ambapo kumefutwa baadhi ya vifungu kama vile kimefutwa kifungu cha 13(2) na kuandikwa upya, ambacho kinazungumzia kuhusu muundo wa bodi.

Kwa kweli sheria hii tumeipitisha hivi karibuni sasa inaonekana huu muundo pengine umekwenda kinyume na taratibu au kinyume na sheria, sasa tumefanya marekebisho.

Lakini hapa marekebisho tuliyoyafanya naona bado yako vile vile, kwa sababu huku kwenye kifungu cha 9 cha sheria ambapo marekebisho Mhe. Waziri ametuletea kwa mujibu wa Kanuni ya 84(2) (a) anasema kuongeza aya mpya ya tano mara baada ya aya ya nne ambayo itasomeka kama ifuatavyo. Mtu mmoja kutoka Jumuia ya Wafanyabiashara Wenye Viwanda na Wakulima, ina maana kuna ongezeko.
Sasa ongezeko hili kama bodi itakuwa kama hivi ilivyo na kuongeza hivi, maana yake bado tutakuwa tunakwenda kinyume na taratibu au Sheria ile ya Mitaji ya Umma. Kwa hivyo, naona upo umuhimu wa kumuweka mtu mmoja kutoka katika Jumuia ya Wafanyabiashara Wenye Viwanda na Wakulima upo umuhimu.

Lakini pia kuna umuhimu wa kuendelea kufanya masahihisho juu ya hawa wajumbe ambao wapo hapa, pengine badala ya hichi kifungu cha nne ambacho kinazungumzia mjumbe mmoja kutoka katika Jumuia ya Wakulima wa Karafuu Unguja na mwengine kutoka katika Jumuia ya Wakulima wa Karafuu Pemba.

Kwa hivyo, hapa ama atoke mjumbe mmoja, ili tumuingize huyu mtu mmoja kutoka Jumuia ya Wafanyabiashara Wenye Viwanda na Wakulima au kupunguza mjumbe mmoja ambaye atateuliwa na Waziri miongoni mwa kila taasisi zifuatazo na kushauriana na hawa wajumbe watatu, ili sasa hesabu yetu iende sawa.

Kwa maana hiyo, ikiwa Mwenyekiti ambaye anateuliwa na Rais atakuwa na yeye ni *member* basi kiwango cha wajumbe wa bodi hii kitaongezeka. Mhe. Spika, nadhani hapa panahitaji kuangaliwa kwa makini sana, ili tuone tunarekebisha muundo wa bodi yetu, ili uende vizuri.

Jambo la mwisho Mhe. Spika, kuna kitu kimeongezeka, basi namuomba Mhe. Mwanasheria Mkuu kupitia kwako Mhe. Spika, akione huku chini kabisa kwenye eneo la madhumuni na sababu, ambapo ameelezea sehemu tofauti za mswada huu na hapo anazungumzia sehemu ya sita ambayo inahusiana na kufanya marekebisho ya Sheria ya Kuanzishwa kwa Shirika la Bandari Nam. 1 ya mwaka 1997, marekebisho ambayo yanapendekeza kuweka mazingira bora ya uendeshaji na udhibiti wa bandari na hiyo ni sehemu ya sita.

Lakini mswada huu nimeuona una sehemu kuu tano lakini kuna kitu hichi hapa sijui nacho kiliingia kimakosa au vipi. Kwa hiyo, ni muhimu nalo ambapo imejitokeza kwenye madhumuni, na sababu sehemu ya sita ambayo imeongezeka, basi na hilo tumuombe Mhe. Mwanasheria kupitia kwako Mhe. Spika, ajaribu kutupa ufafanuzi kwamba limeingia kimakosa au kwa bahati mbaya ama imekusudiwa, na atupe maelezo kuhusiana na eneo hilo ambalo limeingizwa kwenye mswada wake wa sheria.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo na mswada wetu huu ni mfupi kabisa wenye kurasa mbili, lakini ni mswada muhimu wenye marekebisho muhimu. Kwa hiyo, mimi mwenyewe binafsi na kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Magomeni tunaunga mkono marekebisho haya ya sheria mbali mbali.
Kwa kweli Mhe. Mwanasheria Mkuu aendelee kufanya marekebisho mbali mbali katika sheria hizi, kwa sababu wakati mwengine tunakuwa tunapata mashaka makubwa. Kwa mfano, hivi sasa tunayo mashaka makubwa juu ya Sheria ya Utumishi wa Umma na jinsi ya vifungu vile vinavyogongana ambavyo hata sisi wenyewe Baraza la Wawakilishi tumekuwa tukipata tabu, kuna vifungu kabisa vya sheria ya Utumishi wa Umma sisi tunasema vinagongana na Katiba. Haidhuru Mwanasheria anatwambia havigongani lakini sisi tunaona vinagongana kwa

sababu vifungu vile Mhe. Naibu Spika, vimeipa mamlaka moja kwa moja Tume ya Utumishi ya Baraza la Wawakilishi kufanya muundo wa Utumishi lakini sasa ukija ukiangalia sheria nayo imechukua mamlaka ya kufanya hivyo, sasa tunafika pahala tumekuwa tunagongana.

Sasa tafsiri hizi za sheria na pale ambapo panatokea hitilafu ni halan Mwanasheria basi uchukue *effort* za kuzifanyia marekebisho au ufafanuzi ili tuone kwamba hatugongani katika vyombo mbali mbali. Pengine mgongani huu upo kwetu sisi, pengine mgongano huu upo na kwa wenzetu sisi kwa wepesi tumekuwa tunauona. Kwa hivyo yanapotokea mambo kama haya basi yasiendelee kwa muda mrefu, yaje kwenye chombo hiki kwa sisi tunaotunga sheria. Sheria hiyo ya Utumishi wa Umma tumeitunga sisi lakini na sisi ni binaadamu tunaweza kuwa tumetunga kitu kikawa kina kasoro. Sasa pale wakati matumizi ya sheria yanapotumika tukiona tatizo basi halan marekebisho yale yaletwe hapa ili turekebishe tusije tukafika pahala tukawa tunagongana.

Baada ya maelezo hayo Mhe. Naibu Spika, mimi naunga mkono hoja kwa asilimia mia. Ahsante.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Naibu Spika, nachukua fursa hii na mimi kukushukuru na naomba nitoe mchango wangu mfupi kwenye mswada huu wa marekebisho ya sheria mbali mbali ili niweze kumsaidia Mhe. Mwanasheria Mkuu kwa ajili ya ufanisi wa Ofisi yake. Mhe. Naibu Spika, na mimi niungane na wenzangu kumpongeza Mwanasheria Mkuu kwa uamuzi wake wa kutuletea marekebisho haya ambayo bila shaka yanalenga kuleta ufanisi katika sheria mbali mbali.

Lakini Mhe. Naibu Spika, kwanza naomba Mhe. Mwanasheria Mkuu labda anielimishe pale ambapo serikali inaamua kuleta marekebisho ya sheria yoyote kunakuwa na vigezo gani? Kunakuwa na manung'uniko ya umma au kunakuwa na haja fulani tu ya serikali kwa ajili ya kufanya jambo fulani. Ninavyotegemea mimi ni kwamba sheria hizi zinatungwa kwa ajili ya watu, watu wanapoleta manun'guniko kwa maana kwamba sheria haiwafanyii haki tutarajie kwamba serikali ichukue hatua haraka kwa ajili ya kufanya marekebisho.

Kama hivi ndivyo Mhe. Naibu Spika, niendelee kumkumbusha Mhe. Mwanasheria Mkuu kwamba kama Mhe. Salmin alivyozungumza sisi tunatunga sheria mbali mbali kwa madhumuni ya kuwasaidia wananchi, lakini pale inapotokezea sheria inapoleta vikwazo kwa wananchi ni vyema serikali ichukue hatua haraka haraka ya kurekebisha sheria mbali mbali. Na nimkumbushe Mwanasheria Mkuu kwamba Baraza hili lilitunga sheria ya uvuvi miaka minne mitano nyuma lakini tangu siku ya mwanzo sheria ile ilipotungwa wananchi wa Unguja na Pemba wavuvi wote wamekuwa wakilalamika kuwa sheria ile haikuwafanyia haki. Tumekuwa tukiomba kwamba sheria ile ni vyema iangaliwe na serikali ifanye marekebisho kwa maslahi ya wavuvi na kwa maslahi ya serikali. Sasa kama kigezo ni manun'guniko ya umma basi sheria ile ina manun'guniko mengi ya umma na ni budi sasa serikali ichukue hatua hiyo kufanya marekebisho mbali mbali kwa ajili ya kuleta ufanisi kwa umma na kwa serikali kwa ujumla.

Lakini Mhe. Naibu Spika, vile vile sheria ile ya Mhe. Salmin alivyozungumza ya Utumishi wa Umma ile sheria inaleta manun'guniko kwa Baraza la Wawakilishi na pia inaleta manun'guniko kwa muhimili mzima wa dola kama Baraza la Wawakilishi. Sasa kama lengo ni manun'guniko kuondoshwa basi sheria hizi ziangaliwe kwa kina haraka sana ziweze kurekebishwa ili pasiwe na manun'guniko baina ya wale wadau wa sheria ile.

Mhe. Naibu Spika, baada ya utangulizi wangu huo kwa kumuomba Mwanasheria Mkuu sasa naomba niseme tu kwamba marekebisho aliyofanya ni ya msingi kwa madhumuni ya mswada huu na kwa ajili ya kufanya malengo ya sheria yaende sambamba na matakwa ya leo.

Mhe. Naibu Spika, niseme tu kwamba Mwanasheria Mkuu ametuletea marekebisho ya sheria mbali mbali ikiwemo sheria ile ya kutanua ya Mahkama Kuu. Lakini kabla ya kuja kwa sheria hii, hivi karibuni nimesikia Mahkama Kuu imeongeza Divisheshi mpya ya mahkama ya watoto. Sasa najiuliza kipi kinatangulia mwanzo ilikuwa itangulie mwanzo hii sheria kwa maana ya marekebisho au uamuzi wa mahkama kutanua divisheni ile ilikuwa ni sahihi. Sasa ndio picha ninaipata hapa kwamba kumbe madhumuni ya mswada huu ni kuiruhusu Mahkama Kuu kuweza kutanua mahkama yake kwa maana ya kuongeza divisheni mbali mbali. Lakini kabla ya sheria hii leo kufika hapa tayari Mahkama Kuu imetanua Divisheni ya Mahkama ya Watoto ni divisheni ambayo kwa kweli tayari inaanza kufanya kazi, sasa nilikuwa ninajiuliza tu ni kipi kimetangulia ni huu mswada wa leo au ni yale maamuzi ya mahkama kutanua Divisheni yake ya Mahkama ya Watoto.

Mhe. Naibu Spika, jambo jengine ambalo ningelipongeza sana kwa mswada huu ni kwamba kila pahala sasa ameteuliwa Rais kama mteuzi wa baadhi ya Majaji. Mimi nadhani ni jambo la kupongeza kwamba tumeona sasa

umuhimu wa kwamba Rais kila pahala tusimpe majukumu mengi. Mswada huu marekebisho haya yamelenga sasa kumpunguzia majukumu Rais kwamba baadhi ya Majaji wa mahkama fulani wateuliwe na Majaji wakuu wa Mahkama Kuu. Nadhani ni maamuzi mazuri na pia itaisaidia Mahkama zetu kuona msaada mkubwa kwa upande wa Urais. Kwa sababu miswada mingi ilikuwa Majaji hawa Rais ndio anaowateua lakini kwa mswada huu na marekebisho haya, sasa Jaji Mkuu ndiye atakaeshauriana na Tume ya Utumishi ya Mahkama kuteua baadhi ya Majaji wa mahkama mbali mbali. Ni jambo la kupongezwa na mimi naunga mkono katika suala hilo.

Mhe. Naibu Spika, lakini jambo jengine ambalo ningelisema kwamba sheria hizi ya kuanzisha Shirika la Biashara ambayo sheria tuliipitisha mwaka 2011 ni sheria mpya sana lakini tayari tumeifanyia marekebisho kwa mujibu wa mswada huu. Sasa kuna haja ya kujiuliza kama Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi je tunapotunga sheria hizi panakuwa hapana umakini kiasi hicho au serikali wanakuwa kuna jambo gani linasahaulika haraka haraka wakati sheria mpya kama hii kuifanyia marekebisho haraka. Sasa nadhani tuwe makini sana kwa niaba ya wananchi pale tunapoamua kutunga sheria tusikurupuke ili sheria angalau ichukue muda mrefu kabla kurekebishwa. Ingawa marekebisho ya sheria ni sehemu ya kukua kwa maendeleo ya nchi, lakini nadhani tungekuwa makini zaidi katika kutung sheria zetu ili wananchi sheria hizo wasaidie kwa maendeleo ya nchi yetu na maendeleo ya ustawi wa jamii.

Mhe. Naibu Spika, marekebisho ambayo Mwanasheria Mkuu ameyaleta ya sheria hizi mbali mbali nadhani ni marekebisho ya msingi na niseme tu kwamba suala la mahkama ya Kadhi sijui kwa nini tumerekebisha kifungu hiki tu lakini kuna vifungu vingi ambavyo wafanyakazi mbali mbali wa serikali na sekta binafsi wamekuwa wakikwaza na masuala ya kazi. Sasa ni kiasi gani vile vifungu vyengine vinawalinda wafanyakazi wetu kwa ajili ya kupata haki zao za msingi na kwa nini Mwanasheria Mkuu asiamue kurekebisha vifungu zaidi kwa ajili ya kutoa uwanja mpana wa maslahi ya wafanyakazi wetu.

Tumekuwa tukisikia mara nyingi hasa wafanyakazi wa sekta binafsi mahotelini, wamekuwa wakidhalilishwa, wamekuwa hawafungiwi mikataba na kampuni mbali mbali za binafsi wamekuwa wakifanya ujanja kuwafanyisha kazi wafanyakazi wetu bila ya mkataba. Maana yake wanawapa mikataba muda mfupi miezi mitatu, miezi sita kusudi kwamba kukwepa haki zao za msingi pale wanapostaafu au wanapomalizia muda wa kazi. Sasa nadhani mambo kama hayo Mhe. Naibu Spika, Mhe. Mwanasheria Mkuu angeyazingatia kutoa uwanja mpana kwa wafanyakazi wetu ili kukwepa ule mwanya wa matajiri au sekta binafsi ambazo tunatumia kuwafanya wafanyakazi wetu hasa sekta binafsi kuwafanya kukosa haki zao za msingi.

Mhe. Naibu Spika, baada ya hayo na kwa sababu mswada wenyewe ni mfupi sana mimi niseme tu Mwanasheria Mkuu azingatie zile sheria zote ambazo zinawakwaza wananchi na zinaleta manun'guniko ili zirekebishwe kwa ajili ya kuweka sawa ustawi wa jamii na maendeleo ya nchi yetu na serikali yetu.
Mhe. Naibu Spika, baada ya hayo naunga mkono mswada.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Naibu Spika, awali ya yote naomba nianze kwa kumshukuru muumba wetu Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa kutujaalia kuwa hai na wazima na kutupa nguvu ya kuendelea kusimama katika Baraza hili tukiendelea kujadili masuala yanayohusu nchi ya Zanzibar na watu wake.
Nikushukuru na wewe Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa fursa hii na mimi kuchangia machache kuhusiana na mswada wa sheria ya kurekebisha sheria mbali mbali na mambo mengine yanayohusiana na hayo. Lakini tatu Mhe. Naibu Spika, nimshukuru na kumpongeza Mwanasheria Mkuu kwa kuleta mswada huu kwa niaba ya serikali katika Baraza hili.

Mhe. Naibu Spika, kabla ya kuingia katika maudhui ya vifungu ya mswada huu naomba uniruhusu nitumie muda mchache katika mchango wangu kuzungumzia juu ya kifo kilichotokezea leo cha aliyekuwa Waziri Mkuu wa Uingereza mama Margaret Thatcher**.**

Mhe. Naibu Spika, mchana huu mama huyu ambaye wakati wa zama zake akiwa Waziri Mkuu kuanzia mwaka 1979 hadi 1991 aliitikisa dunia kutokana na ushupavu na ujasiri wake wa uongozi leo amefariki dunia. Nimeguswa na kumtaja kwa sababu Mhe. Naibu Spika, mama Thatcher ni katika watu ambao katika historia ya Uingereza wanakumbukwa kama ni alama iliyoleta mabadiliko makubwa sana katika nchi yao**.** Lakini vile vile ameweka historia katika nchi ambayo kwa maumbile ya utamaduni wake watu ni wahafidhina akawa mwanamke wa kwanza kuwa Waziri Mkuu wa nchi hiyo.

Lakini sio hilo tu Mhe. Naibu Spika, kama ni alama ya mabadiliko kwa sababu alirithi uongozi katika kipindi ambacho Uingereza ilikuwa katika mtihani mkubwa sana. Na haikutegemewa kwamba mwanamke angeweza kusimamia mabadiliko ya kuirejesha Uingereza katika heshima yake katika siasa za kimataifa lakini hata katika kuufufua uchumi wa nchi yake. Nimeguswa kumtaja Mhe. Naibu Spika, kwa sababu ni katika watu niliokuwa nikiwaheshimu sana lakini nimeona niseme hapa leo ili bila kuchukua muda mrefu kuwambia viongozi wenzetu katika nchi hii na viongozi wenzangu kwamba tunapaswa kujifunza na watu kama Margaret Thatcher ambao hawakusita kuchukua maamuzi magumu yanayorejesha heshima ya nchi yao na heshima ya watu wao na utu wa watu wao Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Naibu Spika, moja katika usemi unaokumbukwa sana wa mama Thatcher alisema, '*I am very passion as far as I get my own way in the end*. Yaani mimi ni mvumilivu sana ikiwa mwisho wake ninapata lile ambalo ninalitaka. Mhe. katika nchi kama zetu hizi na misukosuko ambayo inayotukabili na hali ambayo tunakabiliwa na kuamua mustakbali wa Zanzibar na maisha na watu wake nadhani tuna mengi ya kujifunza tutamkumbuka sana mama Thatcher na wale wote ambao kama mimi walikuwa wakimuona yeye kama ni kigezo cha uongozi nadhani wataendelea kunufaika na hazina ya uzoefu wake na uongozi wake na maandishi mengi aliyoyaacha.

Mhe. Naibu Spika, baada ya kusema hayo sasa nije katika mswada. Mhe. Naibu Spika, mswada huu unakusudia kurekebisha sheria mbali mbali na wenzangu waliochangia kuuchangia wamegusia. Lakini kubwa ninaloliona mimi katika sehemu zote, sehemu ya pili ambayo inarekebisha sehemu ya pili ambayo inarekebisha sheria ya mahkama ya Kadhi No 2 ya 1994.

Sehemu ya tatu ambayo inarekebisha sheria ya udhibiti wa kodi namba 3 ya 1987. Sehemu ya nne ambayo inarekebisha sheria ya mahkama Kuu namba 2 ya 1985, na sehemu ya tano ambayo inarekebisha sheria ya Shirika la Biashara ya Taifa nambari 11 ya 2011. Katika sehemu zote hizi sehemu nne za awali Mhe. Spika, zinafanya marekebisho yanayofanana ambayo ni kumuondolea uwezo wa kuteua Wenyeviti wa Mahkama hizi mbali mbali zilizotajwa Rais na badala yake kuyaweka mikononi mwa kiongozi wa muhimili wa mahkama, Jaji Mkuu akishirikiana na Tume ya Utumishi ya Mahkama.
Mhe. Spika, hili ni jambo la kupongezwa kwa sababu Katiba yetu katika marekebisho yaliyofanywa mwaka 2001/2002 na hata yale yaliyofanywa mwaka 2010 ambayo yameipa heshima sana nchi yetu yametambua na yameweka misingi madhubuti zaidi ya mgawanyo wa madaraka.

Mhe. Spika, kifungu au Ibara ya 5 ya Katiba ya Zanzibar 5(a) au kama wanavyosema wanasheria nikisoma kwa kiingereza 5 (A)(1) inasema Zanzibar itafuata mfumo wa mgawanyo wa madaraka kati ya mamlaka tatu, mamlaka ya utendaji, mamlaka ya kutunga sheria na kusimamia utekelezaji wa shughuli za umma na mamlaka ya kutekeleza utoaji haki.

Halafu 5(A) kifungu kidogo cha (2) kikaendelea kikasema, mamlaka ya utendaji ni Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, mamlaka ya kutunga sheria na kusimamia utekelezaji wa shughuli za umma ni Baraza la Wawakilishi na mamlaka ya kutekeleza utoaji haki ni Mahkama. Lakini haikumalizia hapo Mhe. Spika.

Kijifungu cha (3) cha kifungu hicho cha 5(A) kinamalizia kwa kusema hakuna mamlaka itakayoingilia mamlaka nyengine isipokuwa kama na kwa kadri ilivyoelezwa katika Katiba hii. Mhe. Spika, kifungu hiki kimeweka kama kawaida yetu Zanzibar kutangulia katika mambo mengi ya uandishi mzuri wa misingi ya sheria tumeweka msingi wa mgawanyo wa madaraka. Na tukitizama tutaona kwamba mhimili ule wa mamlaka ya utoaji haki wa mahkama unaongozwa na Jaji Mkuu. Sasa ilipendeza kwamba na vyombo vyengine ambavyo navyo ni sehemu ya mamlaka ya utoaji haki basi viwe vinapata nguvu zake kwa kuteuliwa na kiongozi wa muhimili huu ambaye ni Jaji Mkuu.

Kwa hivyo mimi Mhe. Spika, nataka kuanza kwa kupongeza hatua ya serikali kufanya marekebisho haya ya kurejesha mamlaka haya kwa Jaji Mkuu kwa kushauriana na Tume ya Utumishi ya Mahkama. Lakini wakati ninapongeza Mhe. Spika, nitumie fursa hii kumuomba Mwanasheria Mkuu kwamba tusiishie hapo.

Mhe. Spika, nadhani Mwanasheria Mkuu anapaswa vile vile akiangalie vizuri kifungu cha 53 cha Katiba ya Zanzibar. Kwa sababu kifungu hiki Mhe. Spika, kinatoa nafasi kwa Baraza hili kutunga sheria ambazo zinaweza kufanya baadhi ya wakuu wa Ofisi wakateuliwa na asiyekuwa Rais. Mhe. Spika, naomba nikinukuu kifungu kinasema, kifungu cha 55 cha Katiba ya Zanzibar.

‘Kwa mujibu wa Katiba hii na bila ya kuathiri masharti ya sura ya nane au sheria nyengine yoyote iliyopitishwa na Baraza la Wawakilishi, mamlaka ya kuanzisha au kufuta Afisi katika Zanzibar na (b) ya kuteua wakuu wa Afisi hizo na ya kupandisha cheo kwa ajili ya watumishi, kufukuzwa na kushughulikia na hatua za kinidhamu kwa watu walioteuliwa kushika dhamana za Ofisi hizo yamo mikononi mwa Rais’.

Nilipo mimi Mhe. Spika, ni hapa inaposema mwanzo hapo kwamba kwa mujibu wa Katiba hii na bila ya kuathiri masharti ya sura ya nane au sheria nyengine yoyote iliyopitishwa na Baraza la Wawakilishi. Kwa hivyo Katiba hiyo Mhe. Spika, inatoa nafasi kwa Baraza hili kutunga sheria ambayo inaweza kutoa mamlaka ya kuanzisha au kuteua wakuu wa Ofisi kwa kiongozi mwengine au mamlaka nyengine isiyokuwa mamlaka ya Urais au *the institution of presidence* Mhe. Spika.

Sasa Mhe. Spika, nimeona niliseme hili kwa sababu nimeona leo mwanzo mzuri kwa marekebisho haya kwamba kwa mhimili wa mahkama sasa tunasema Jaji Mkuu amsaidie Rais katika baadhi ya mambo wakuu wa hizi taasisi awateue yeye kwa mashauriano na Tume ya Utumishi ya Mahkama.
Na Mhe. Spika, Baraza hili mara nyingi Wajumbe wake katika michango mbali mbali wamekuwa wakizungumzia kwamba mamlaka ya uteuzi ni makubwa sana kwa Rais na matokeo yake kwa sababu hawezi kuwajua watu wote ndio mara nyingi watu wengine ambao wanachukua nafasi ile wanamshauri vibaya kwa kupeleka watu wanaoteuliwa ambao mara nyingi wanashindwa dhamana zao za kazi.

Sasa nadhani Mheshimiwa tukifika pahala tuka-*decentralize* tuka-*delagate* madaraka yale ya kuteua kwa mamlaka nyengine kwa kutumia kifungu hiki cha 53 cha Katiba ya Zanzibar, basi nadhani tunaweza tukaongeza ufanisi. Huo ulikuwa mchango wangu mmoja wa Mhe. Spika, nilikuwa naomba niutoe.

Lakini nikienda katika vifungu mahsusi Mhe. Spika, kwa ufupi tu kwa sababu kama nilivyosema mswada huu si mkubwa na maeneo yake mengi yameeleweka. Sidhani kama si mimi wala sidhani kama kuna Mjumbe mwengine atakayekuwa na hoja sana na maudhui ama marekebisho. Labda tutakuwa kama walivyofanya wengine tunaongezea kwa kuonesha baadhi ya maeneo mengine ambayo tunadhani kwamba yanapaswa pia yafanyiwe marekebisho.

Kwa hivyo nilianza pale mwanzo Mhe. Spika, kwa kumpongeza Mwanasheria Mkuu kwamba kaanzisha utaratibu mzuri wa kuziangalia sheria zetu na zile ambazo ukaona kwamba zinahitaji marekebisho kupitia utaratibu wa *miscellaneous amendments*, yaani marekebisho ya sheria mbali mbali ambao mara nyingi huwa yanaangalia marekebisho madogo madogo.

Sasa Mhe. Spika, nianze na hili la sehemu ya pili. Marekebisho ya sheria ya Mahkama ya Kazi. Kama nilivyosema naunga mkono wala sina matatizo na marekebisho yaliyoletwa ya kifungu cha 14(1). Lakini wamesema Wajumbe wenzangu na mimi nataka kuongezea nguvu hapo hapo Mhe. Spika, kwamba sheria ya Mahkama ya Kazi inalalamikiwa si katika eneo hili moja tu, lakini pia kuna maeneo mengine jumuia hasa za wafanyakazi wanayalalamikia. Lakini si katika sheria ya Mahkama ya Kazi tu lakini hata sheria za kazi zenyewe na kupitia utaratibu wa *lobby* Mhe. Spika, wamekuwa wakitufuata hawa na kutueleza maeneo mbali mbali ambayo wanahisi sheria zinapaswa kurekebishwa.

Mhe. Spika, tulipokuwa tukijadili rasimu wakati ule muswada wa sheria ya utumishi wa umma, basi walipokuja wafanyakazi ambao bahati mbaya wakati ule hatujaanzisha utaratibu huu wa kuwashirikisha wahusika mbali mbali. Ikabidi waliokuwa wakitufanyia *lobbing* kupitia njia za pembeni pembeni huku, walikuja na maeneo mengi walikuwa wanalalamikia juu ya ushiriki wao au wafanyakazi kupitia jumuia zao kuweza kuona kwamba wanapata haki zao na wanashirikishwa katika maamuzi ambayo yanawahusu. Wanalalamikia sana na wakati ule hasa katika maeneo ya maslahi yao, yawe maslahi kwa maana ya mishahara ya marupurupu lakini hata katika maslahi kwa maana ya haki zao masuala ya migomo na mengine. Kwa hivyo nilikuwa nadhani Mhe. Spika, wakati tunapongeza hatua hii basi Mhe. Mwanasheria Mkuu si vibaya angetafuta ikiwa ni yeye au kupitia Wizara yenye dhamana ya sekta hii kazi, basi kukawa na Wawakilishi wa jumuia za wafanyakazi ili kusikiliza malalamiko yao katika maeneo mengine ambayo wangependa yafanyiwe marekebisho.

Mhe. Spika, sehemu ya tatu inahusu marekebisho ya sheria ya udhibiti wa kodi ambayo kwa marekebisho ya Kamati ya Katiba na Sheria na Utawala imependekeza irekebishwe pia iitwe sheria ya udhibiti wa kodi za nyumba. Hili vile vile Mhe. Spika, ninavyosema kifungu kile cha 6(1) kinachohusu uteuzi wa Mkuu wa Mahkama ile hakina tatizo.

Lakini Mhe. Spika, nilikuwa nataka nitumie fursa hii na mimi kulitilia nguvu lile alilosema Mheshimiwa Mwakilishi wa Jimbo la Magomeni Mhe. Salmin Awadh.

Mhe. Spika, tumefika wakati vile vile nadhani labda Afisi ya Mwanasheria Mkuu itusaidie hapa kuangalia marekebisho tunayoyafanya ya sheria mbalimbali au tunazozipitisha basi utekelezaji wake unakuwa *synchronized* unaoainishwa na utendaji katika serikali. Mhe. Spika, hili naligusia kwa sababu linagusa moja kwa moja eneo ambalo ninaliwakilisha katika Baraza hili eneo la Mji Mkongwe. Nimeamua niliseme hapa na nitalisema tena katika Kamati, nadhani Waziri muhusika atajiandaa vizuri tutapokuja kupokea ripoti za Kamati.

Mhe. Spika, pamefanywa marekebisho katika sheria hapa ambayo iliondoa mamlaka ya kukusanya *land rents* kutoka katika Baraza la Manispaa kuyahamishia katika Bodi ya Mapato ZRB. Na sheria hiyo iko hivyo mpaka leo. Lakini Baraza la Manispaa linaonekana limeng'ngania hili, sasa unapojiuliza wanapong'ng'ania wao kukusanya hili na kuamua viwango wanatumia sheria gani na wanatumia mamlaka yepi, wakati Baraza la Kutunga Sheria la nchi hii tayari limefanya marekebisho kuondoa mamlaka yale kuyapeleka ZRB.

Lakini inasikitisha zaidi Mhe. Spika, ndio maana nikasema nitakuja kulizungumza hili tutapokuja kupokea ripoti za Kamati mbali mbali hapa. Kwa sababu inaonekana na hili Mhe. Spika, nataka niliseme hapa kwa sababu ni muhimu na wewe ukalielewa unaponituma kazi. Inaonekana mara nyengine unapotutuma kufanya kazi fulani hasa hizi za Kamati Teule za kuchunguza mambo ambayo watu huku wanafanya wanavyotaka. Unapoleta ripoti hapa ambayo huwa haiwapendezi watendaji wanaochunguzwa Mhe. Spika, wanatafuta jambo jengine na wanajisifu hasa huko nje kwamba watakukomoa wewe uliotumwa ile kazi na Mhe. Spika, uliotutuma sisi kwa kutumia njia nyengine. Hili Mhe. Spika, limeonekana. Mara baada ya au wakati tunafanya uchunguzi wa sakata la Baraza la Manispaa pakazuka ghafla mkakati wa kufanya mapitio ya viwango vya *land rents* kwa nyumba ambazo ziko katika mji wa Zanzibar, lakini zaidi *focus* iko Mji Mkongwe. Nilipouliza nikaambiwa ati mpaka iwe nyumba ya ghorofa nikashangaa mimi nikasema basi sheria ya kibaguzi kwa nini iwe nyumba ya ghorofa. Lakini nyumba za ghorofa Mhe. Spika, haziko Mji Mkongwe tu sina hakika kwamba ile nguvu inayotumika kuongeza na kudai watu wa Mji Mkongwe kuwakamua kwa kuwatia adabu sasa Mhe. Spika. Kwa sababu huwezi ukaongeza *land rent* kutoka mtu aliyekuwa akilipa kwa mfano laki moja ukamwambia kuanzia sasa utalipa milioni saba wewe. Mimi nimetafsiri Mhe. Spika, moja kwa moja kwamba ilikuwa ni kuwatia adabu na kuwakomoa watu wa Mji Mkongwe kwa sababu Mwakilishi wao ulimtuma Mhe. Spika, akawa Mjumbe katika Kamati ya kuchunguza Baraza la Manispaa na tukaleta ripoti ambayo haikuwapendeza watendaji katika Baraza Manispaa.

Mhe. Spika, nimelisema hapo na kama nilivyosema hapa nalitahadharisha tu lakini tutalizungumza zaidi katika Kamati huko, kwa sababu utaratibu kama huu hauridhishi kabisa. Na kama serikali hii imeamua kwamba ina *double standards* basi ije itwambie katika Baraza hili, kwamba tumepitisha sheria kwamba ZRB ndio mwenye mamlaka ya kukusanya kodi hizi. Lakini Baraza la Manispaa ikang'ang'ania ili kuwatia adabu wapiga kura wa Mji Mkongwe kwa sababu Mwakilishi wao ulimtuma Mhe. Spika, akawa Mjumbe katika Kamati ya Kuchunguza Baraza la Manispaa na tukaleta ripoti ambayo haikuwapendeza watendaji wa Baraza la Manispaa.

Mhe. Spika, hili hatutolivumilia hata kidogo kwa sababu litakuwa linaingilia mamlaka yetu ambayo tumepewa na wapiga kura wetu katika eneo hili. Kwa hivyo Mhe. Spika, kama nilivyosema sina matatizo na sheria hii lakini nilikuwa nataka kutumia nafasi hii kuzungumza hili.

Mhe. Spika, Sehemu ya Nne inahusu marekebisho ya Sheria ya Mahkama Kuu. Hii Mhe. Spika, mimi imenifurahisha, Mhe. Salmin Awadh alipokuwa akichangia kauliza kutanuliwa huko ni kutanuliwa kupi? Katika kifungu cha 7 cha mswada huu ambacho kimependekeza kuongeza kijifungu kidogo kipya cha pili kinachosema, Mahkama Kuu inaweza kutanuliwa katika migawanyo tofauti.

Mimi nilivyofahamu na kama sivyo Mhe. Mwanasheria Mkuu atakuja kunisaidia kunirekebisha ni kwamba hizi ni *divisions*. Tumekuwa tukianzisha Mahkama mbali mbali kama vile kuna mswada hapa unakuja wa kuanzisha Mahkama ya Biashara, lakini kuna Mahkama ya Ardhi, kuna Mahkama ya Kazi, kuna Mahkama ya mambo ya Kodi, ziko Mahkama nyingi Mhe. Spika.

Nadhani nilivyofahamu mimi ni kwamba hizi sasa zote zinatambuliwa rasmi kupitia Sheria ya Mahkama Kuu, kwamba zitakuwa ni *divisions*, ni sehemu ya Mahkama Kuu lakini ina mikono mbali mbali kulingana na yale

maeneo ambayo tunashughulikia na yote yapo chini ya Jaji Mkuu ambaye anakuwa ndiye mkuu wa muhimili huu kama katiba yetu inavyosema.

Kwa hivyo, mimi Mhe. Spika, nimelielewa hivyo na kwa sababu hiyo napongeza tu kwa sababu inafanya masuala ya utawala yakae vizuri kwamba yote yako chini ya muhimili mmoja wa Mahkama.

Nimalizie Mhe. Spika, na Sehemu ya Tano inayohusu marekebisho ya Sheria ya Shirika la Biashara la Taifa Nam. 11 mwaka 2011. Mhe. Spika, ukisoma madhumuni na sababu ya mswada huu kuna sehemu inasomeka kuhusiana na sehemu hii inasema, "Sehemu ya tano inahusiana na marekebisho ya Sheria ya Shirika la Biashara la Taifa Nam. 11ya mwaka 2011", ambapo muundo wa bodi uliokuwepo awali unabadilishwa hasa katika idadi ya Wajumbe ili kuhakikisha kwamba unakwenda sambamba na matakwa ya sheria zilizopo (*Public Investment Act)* Nam. 4 ya 2002 zinazohusiana na miundo ya Bodi.

Mhe. Spika, tunaambiwa kwamba, kwa mujibu wa hiyo *Public Investment Act* Nm. 4 ya mwaka 2002 Wajumbe wa Bodi wanatakiwa wawe ni Mwenyekiti na Wajumbe wengine kati ya watano na saba, lakini ile sheria ambayo tuliipitisha hapa iliweka wajumbe wengine wanane na mwenyekiti akiwa wa tisa. Kwa hivyo sasa marekebisho haya yaliyoletwa yanaondoa hitilafu hiyo kwa kuweka Bodi ambayo itakuwa na mwenyekiti na wajumbe wengine hawa nadhani ni sita, kwa sababu kuna Mkurugenzi Mwendeshaji, Wajumbe watatu wanaowakilisha wizara mbali mbali na wajumbe wawili hawa ambao wamependekezwa kutoka katika jumuiya hizi mbili. Kwa hivyo, nadhani hii inatoa nafasi kwamba jumla sasa watakuwa ni saba mwenyekiti na hao wengine sita hivyo itakuwa inaendana na sheria hii na ninaipongeza.

Lakini vile vile nitumie fursa hii Mhe. Spika, kama walivyosema wenzangu kwamba nadhani tunapaswa kuwa waangalifu tunapoleta miswada katika Baraza hili. Sikumbuki vizuri Mhe. Spika, nani lakini nakumbuka tulipokuwa tukijadili mswada huu ulipoletwa kuna mjumbe mmoja alitahadharisha, kwamba ule muundo ulioletwa ulikuwa unakwenda kinyume na idadi yake ilikuwa ni kubwa sana kunyume na sheria hii Nambari 4 ambayo imetajwa hapa ya *Public Investment Act*, labda hakuitaja tu, lakini alitahadharisha juu ya kuwepo kwa sheria ambayo inaongoza idadi ya wajumbe.

Sasa Mhe. Spika, mimi ni binadamu mara nyengine unaweza ukapitikiwa, lakini ninachokihisi vile vile na kama sivyo nitaomba nije nisahihishwe, kwamba inawezekana hili linasababishwa vile vile na ule utaratibu uliokuwepo siku hizi ambao natumai baada ya kupitisha ile sheria ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu na baada ya kutiwa saini na Mhe. Rais itaondoka. Nadhani kwamba ule utaratibu wa kuwa kila wizara inakuwa na mwanasheria wake na anaandaa rasimu ya mswada mara nyengine bila ya kupitia Ofisi ya Mwanasheria Mkuu halafu kunaingia ngazi nyingi zikajadili huko kati kati ndio mara nyengine yanapita mambo kama haya, yanawapita baadhi ya watu kwa sababu hakuna uoneshaji mzuri wa sheria au rasimu zilizotungwa katika wizara zile na msimamizi mkuu wa sheria ambaye ni Mwanasheria Mkuu akitambua sheria mbali mbali zilizokuwepo pale.

Kwa hivyo, nasema hii iwe ni funzo tu kwetu kwamba kama alivyosema kuwa tuhakikishe yale ambayo yametajwa katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu yatakuja kutekelezwa, kuwa rasimu za miswada zitakuwa zinapita pale ili kujiridhisha kwamba zitakwenda sambamba na sheria nyengine ili kuondosha kitu kama hiki Mhe. Spika. Kwa sababu haipendezi kuwa sheria ambayo tumeitunga mwaka juzi tu ndani ya kipindi cha mwaka mmoja au mmoja na nusu inarejeshwa katika Baraza kwa ajili ya kuja kurekebishwa.

Baada ya kusema hayo Mhe. Spika, na mimi niseme kwa niaba yangu na kwa niaba ya wananchi wa Mji Mkongwe walionileta katika Baraza hili naunga mkono mswada huu na nawatakia kila la kheri katika utekelezaji wa kazi baada ya marekebisho haya. Mhe. Spika, nakushukuru sana ahsante.

Mhe. Abdalla Juma Abdalla: Ahsante Mhe. Spika, kwa kweli mimi nina jambo dogo sana tu, kwa sababu kama walivyotangulia kusema wenzangu mswada huu ni mfupi sana hamna mambo mengi ambayo yanahitaji kuyatolea mawazo au mcango. Wenzangu waliotangulia wameshasema mambo mengi kwa kweli na tukiendelea kuchangia basi tutakuwa tunarudia humo kwa humo.

Mimi namuomba Mhe. Mwanasheria Mkuu anipe ufafanuzi wa jambo moja, nilipokuwa nasoma madhumuni na sababu kaeleza kule kila sehemu na madhumuni yake, lakini nikenda sehemu ya kwanza, ya pili, sehemu ya tatu, ya nne akenda mpaka sehemu ya sita, sasa sehemu ya sita katika mswada huu mimi sikuiona kwa sababu ni sehemu ya

marekebisho ya Sheria ya Bandari ambayo tulishaipitisha na ina mswada wake mbali si mswada huu. Sasa sijui kama hapa pana *printing mistake* au kuna kitu gani, labda pengine hili gazeti nililonalo mimi limepungua sehemu fulani nilikuwa naomba Mhe. Mwanasheria Mkuu atupe ufafanuzi wa hili.

Mhe. Spika, mimi nilikuwa naona hii sehemu ya sita labda haihusu huu mswada ambao tunaufanyia marekebisho sasa hivi. Hilo lilikuwa la kwanza.

Lakini la pili nilikuwa nataka nielimishwe vile vile hii sehemu ya tatu ambayo inahusu marekebisho ya sheria ya udhibiti wa kodi na kwanza iliandikwa kodi lakini bahati nzuri Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala ikasema kodi ya nyumba, maana yake ilipokuwa kodi tu mimi nilikuwa sifahamu vizuri na kila pahala ilikuwa imeandikwa hivi hivi kodi. Lakini kupata marekebisho yale ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala wakaongeza wao kodi ya nyumba. Sasa hapa Mhe. Mwanasheria Mkuu alipokuwa akitoa ufafanuzi asubuhi alikuwa akitaja kodi ya nyumba lakini sikuona pahala ilipokuwa imeandikwa.

Sasa tatizo langu hapa ukisoma kwenye madhumuni na sababu sehemu ya tatu anasema, "inahusiana na marekebisho ya Sheria ya Udhibiti wa Kodi, bila shaka itakuwa kodi ya nyumba, akaendelea kusema kwamba badala ya Mwenyekiti wa Mahkama hiyo". Sasa tatizo langu liko hapa, maana yake mimi nilikuwa sijui Mhe. Spika, kwamba na hii kodi ya nyumba kumbe nayo ina Mahkama yake sijui, mimi nilikuwa nadhani kuna Mahkama ya Ardhi, Mahkama ya Kazi, Mahkama ya Biashara lakini hii Mahkama ya Kodi ya Nyumba nilikuwa sijui. Sasa nafikiri labda kama itakuwa ndivyo ilivyokusudiwa hivi basi itakuwa ni elimu kwangu mimi kumbe kuna Mahkama ya Kodi ya Nyumba.

Jambo jengine Mhe. Spika, ambalo wenzangu wameligusia kwa urefu, kila aliyesimama hili amelizungumza lakini kwa sababu na mimi nimeliandika na sio kuliandika tu, bali nina mapendekezo hata ya namna lugha ilivyotumika mimi nikaandika yangu. Kifungu cha 9 Sehemu ya Tano kinahusu marekebisho ya Shirika la Biashara la Taifa, ukisoma kwenye muundo wa bodi, Bodi itakuwa na mwenyekiti ambaye atateuliwa na Rais, Mkurugenzi Mwendeshaji na Mjumbe mmoja ambaye atateuliwa na Waziri miongoni mwa kila taasisi katika taasisi zifuatazo.

Sasa tatizo langu hii lugha hapa haijakaa vizuri kiasi ambacho ukitaja mjumbe mmoja maana yake ni mjumbe mmoja ndiye atakayeteuliwa, lakini chini pana taasisi tatu halafu kuna kila taasisi maana yake sasa atakuwa si mmoja tena ni watatu, sasa ufafanuzi ukoje. Mimi nikasema labda hili linanichanganya kwa sababu ya hii lugha ilivyoandikwa. Mhe. Spika, mimi nikabuni au nikapendekeza hiki kifungu kirekebishwe ili ionekane kama ni watatu kweli sio mmoja na nitaomba kama itakubalika isomeke hivi:

'Mjumbe mmoja ambaye atateuliwa na waziri kutoka katika kila taasisi miongoni mwa taasisi zifuatazo: sasa hapa zinatajwa, wizara inayohusika na biashara maana yake atoke mmoja humo, wizara inayohusika na fedha atoke mmoja na wizara inayohusika na mambo ya kilimo atoke mmoja. Sasa hii lugha ikipangika hivi basi itakuwa inasomeka kwamba ni mjumbe mmoja kutoka kila taasisi, lakini vile ilivyoandikwa kwanza Mhe. Spika, kwa sisi ambao tunafuatilia Lugha ya Kiswahili inaleta utata hii. Mimi nitafahamu, lakini mtu ambaye anajifundisha Kiswahili leo atapata tabu sana kwa lugha hivi ilivyopangika.

Halafu nilikuwa nimeona mantiki ya hii ambayo Mhe. Mwanasheria Mkuu aliieleza kwamba iwe kama ni *formula* ya Bodi za Mashirika zitakavyokuwa na tayari ilikwishapendekezwa hivi. Hii ukiangalia ina Mwenyekiti wa kwanza, Mkurugenzi wa pili na hawa watatu wanne halafu na huku kuna mjumbe mmoja atakuwa watano huyu kwenye kifungu nambari 4. Lakini katika mapendekezo ya kamati wameongeza kifungu chengine cha tano kwa hivyo wanaongeza tena mjumbe mwengine. Sasa je, ukimuweka huyu mwengine haitakuja kuwa hii *formula* baadae ikawa na matatizo? Kwa sababu hii itakuwa na wajumbe watano, lakini Bodi za mashirika mengine zikajakuwa na wajumbe wanne kama ilivyo humu, nafikiri itakuwa inafahamika. Tukiyachukua yale mapendekezo ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala tukakubali kwamba aongezwe mtu mwengine hii formula iliyokusudiwa hapa ya kuwa na idadi hii ya wajumbe haitakuwa tayari imeshapoteza maana yake ndiko niliko.

Sasa nilikuwa naomba ufafanuzi au kama Mhe. Mwanasheria Mkuu ataona kuna haja bodi zote sasa ziwe na wajumbe kwenye idadi hiyo iliyopendekezwa na kamati basi labda tuone hapa.

Mhe. Spika, kama tulivyotangulia kusema kwamba mswada huu hauna mambo mengi lakini katika ujumla wake ni mswada mzuri na mimi binafsi na kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Chonga sina pingamizi nao naukubali kwa asilimia mia moja. Ahsante sana.

Mhe. Fatma Mbarouk Said: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kunipa fursa hii ya kuchangia katika mswada huu. Kwanza nimshukuru Mwanasheria Mkuu kwa kutuletea sheria hii, vile vile niwashukuru wanakamati kwa kutoa maoni yao.

Mhe. Spika, kama kawaida kwamba mswada huu una madhumuni ambayo ni kufanya marekebisho ya sheria tano ambazo zimeainishwa hapa Sheria ya Mahkama ya Kazi Nam. 2 ya mwaka 1994, Sheria ya Udhibiti wa Kodi Nam. 3 ya mwaka 1987, Sheria ya Mahkama Kuu Nam. 2 ya mwaka 1985, Sheria ya Shirika la Biashara la Taifa Nam. 11 ya mwaka 2011 na Sheria ya Shirika la Bandari la Zanzibar ambayo kama walivyokwishakusema wenzangu kwamba hii sheria nafikiri imeingia kimakosa. Kwa sababu sheria hii tuliikuta kwenye Shirika la Bandari iko ukurasa wa pili ambayo ni 340.

Kwa hivyo Mhe. Spika, na mimi niseme kwamba madhumuni ya mswada huu kwa kweli ni mazuri lakini nilikuwa nina dogo tu ambalo humu wenzangu wengi wameliona kama kifungu alichokisema Mhe. Abdala Juma sasa hivi kwamba, kuna sehemu ya sita inayohusiana na kufanya marekebisho ya Sheria ya Kuanzisha Shirika la Bandari nimeiona kwamba kuna matatizo hayo.

Lakini vile vile nikienda kwenye madhumuni Sehemu ya Pili inayohusiana na marekebisho ya Sheria ya Mahkama ya Kazi Nam. 1994 kwamba badala ya Mwenyekiti wa Mahkama hiyo kuteuliwa na Mhe. Rais kama ilivyokuwa awali badala yake atateuliwa na Mhe. Jaji Mkuu. Mimi Mhe. Spika, naungana mkono na hilo kwa sababu naona kwamba kuna *separation of power* nishukuru kwa kuliona hilo. Kwa sababu kama tulivyoona kwamba Rais ana majukumu mengi na hapa tuki-*separate power* inafanya kwamba Rais atakuwa na yeye atapata nafasi ya kufanya mengine.

Mhe. Spika, nikienda kwenye m swada wenyewe hasa kwenye marekebisho ya sheria Sehemu ya Pili kwanza kuna kusomwa kwa sheria na kufutwa kifungu cha 14 na kuweka kifungu kipya. Mwenyekiti wa Mahkama ambaye atateuliwa na Jaji Mkuu kwa ushauri wa Waziri baada ya kushauriana na Tume ya Utumishi Mahkama kutoka miongoni mwa Majaji Wakuu. Naona hapo Mhe. Spika, sina tatizo napo.

Nikienda Sehemu ya Tatu ya Marekebisho ya Udhibiti wa Kodi hapa kidogo nilikuwa nataka kuuliza kwamba hizi kodi za nyumba ni nyumba za aina gani, kama ni za serikali au ni nyumba za watu binafsi. Hapa Mhe. Spika, naomba akija Mhe. Mwanasheria Mkuu anifafanulie kuhusu kodi hizi.

Vile vile kwa sababu huu mswada ni mfupi kama walivyosema wenzangu lakini kuna Sehemu ya Tano ambayo inaelezea kwamba kuna kifungu kidogo cha pili kifungu cha 13 cha sheria mama kinafutwa na badala yake kuwekwa kifungu kipya nambari mbili ambacho kinasema kuwa kutakuwa na Bodi ambayo Mwenyekiti atateuliwa na Rais, Mkurugenzi Mwendeshaji lakini hapa haikutiwa kama atateuliwa na nani. Kama alivyosema Mhe. Abdalla Juma kwamba Mjumbe mmoja ambaye atateuliwa na waziri miongoni mwa taasisi katika taasisi zifuatazo kwa kushauriana na taasisi husika. Hapa kama alivyosema mwenzangu kwamba ukisema Mjumbe mmoja na halafu chini kuna wizara hizi ni bora ingefanyiwa marekebisho na badala yake kama itakuwa sahihi ingewekwa Mjumbe mmoja mmoja katika taasisi zifuatazo na huku chini zikafuata hizi taasisi.

Baada ya hayo Mhe. Spika, niseme naunga mkono mswada huu kwa asilimia mia moja kwa niaba ya Wananchi wangu wa Jimbo la Amani.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Spika, kwanza naomba kuchukua fursa hii kukushukuru kwa kunipa fursa ya kufanya majumuisho baada ya michango mbali mbali ya Waheshimiwa Wajumbe. Pili, naomba niwashukuru Waheshimiwa Wajumbe wote waliochangia kama walivyotangulia kusema mswada ni mfupi, lakini pengine ulikuwa mfupi komi tu, lakini inaonesha ulikuwa mrefu kwa sababu umepata wachangiaji 9 na dondoo karibu 23 ambazo zitahitaji pengine kutolewa baadhi ya ufafanuzi. Sasa ukisema ni mfupi mtu atauliza ufupi huo uko wapi?

Naomba niwatambue wale waliopata fursa ya kuchangia kama hivi ifuatavyo:

1. Mhe. Ali Abdalla Ali (Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala)
2. Mhe. Hamza Hassan Juma
3. Mhe. Ali Salum Haji
4. Mhe. Mahmoud Muhammed Mahmoud
5. Mhe. Salmin Awadh Salmin
6. Mhe. Hija Hassan Hija
7. Mhe. Ismail Jussa Ladhu
8. Mhe. Abdalla Juma Abdalla
9. Mhe. Fatma Mbarouk Said

Mhe. Spika, hoja zilizotolewa nyingi zilikuwa ni zakusaidia ama kuimarisha utekelezaji wa mswada huu, lakini na pia kuimarisha utekelezaji wa sheria zetu kwa ujumla hasa katika kuzifanyia mapitio. Mbali ya hilo, pia kuna hoja ambazo zilitolewa ambazo pengine na mimi inabidi nitoe maoni, nyengine nitoe ufafanuzi na kwa sababu ya muda nitaomba nizipitie kwa haraka kwa sababu ninaamini nyengine zimetolewa kwa ajili ya kusaidia kupata ufahamu zaidi.

Kwanza Mhe. Ali Abdalla alitoa maoni ya Kamati na ninashukuru kwamba Kamati ilitusaidia sana katika kuimarisha mswada huu na kuufikisha hapa ulipofika na kamati iliunga mkono marekebisho ambayo yamefanywa.

Mhe. Hamza Hassan Juma na yeye alianza kwa kutoa maoni yake na maelekezo kwa kutushajihisha kufanya kazi zaidi kuzifanyia kazi sheria zetu. Na mimi kwa kushirikiana na wenzangu na Waheshimiwa wengi walilizungumza hili naomba niwaahidi kwamba kwa kushirikiana na wenzangu pamoja na Tume ya kurekebisha sheria basi kazi hii tutaendelea kuifanya. Lakini kwa upande wa ofisi kwa marekebisho madogo madogo kama haya tumekusudia kwamba angalau kila mwaka wa fedha basi tulete sheria moja ya marekebisho ya sheria mbali mbali ili yale mapungufu ambayo yatatokea tuweze kuyafanyia kazi.

Jengine ambalo amezungumza Mhe. Hamza ambalo na Waheshimiwa wengine walilizungumza ni kuhusiana na utendaji au marekebisho kwamba kufanywa katika Mahkama ya Ardhi. Tumelisikia bahari nzuri Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati alikuwepo hapa leo tangu asubuhi, Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria alikuwepo na mimi mwenyewe tutalizingatia hilo. Ingawa marekebisho hayo yaliyofanywa kwenye Mahkama Kuu hayatohusu sana Mahkama ya Ardhi, kwa sababu Mahkama ya Ardhi ni Mahkama ya chini na marekebisho haya hayatahusu sana marekebisho katika Mahkama ile, yaani ile ni *Subordinate Court* na hii ni *High Court*.

Lakini mimi niseme kwamba kuna tatizo la msingi ambalo sasa hivi pengine linaendelea kufanyiwa kazi na hili mara nyingi huwa nalisema kwamba, kwa kweli kutokana na sheria zetu za ardhi zilivyo na usimamizi wake basi tatizo lililotokea kubwa mimi sioni vibaya kusema kwamba ile Mahkama ya Ardhi ilikuwa ni kama vile tumeipa kazi kubwa ambayo sio rahisi, ni kama vile uchukue mtu umpeufagio halafu umwambie akafagie jaa, sio kitu rahisi anaweza akachukua karne kuweza kulisafisha.

Tatizo la msingi Mhe. Spika, bado lipo pale pale kwamba kwa muda mrefu hatukuwa na usajili wa ardhi, kwanza hatukuwa na utambuzi wa ardhi zenyewe na usajili wa ardhi zenyewe. Kwa hivyo, hizi hatua ambazo sasa hivi zimeanza na hiyo kazi ilifanywa kuanzia mwaka 1989 mpaka 1994 tulitunga sheria saba mbali mbali za ardhi. Sasa sheria zile kama tutarudi katika kuzitekeleza basi hili tatizo kwa kweli litapungua kwa kiasi kikubwa kwa sababu ardhi kwanza tutaisajili na hatua hiyo kwa kweli imeanza kuchukuliwa utambuzi wa ardhi na usajili.

Mhe. Spika, nadhani wiki moja na kidogo iliyopita Mhe. Rais alizindua usajili wa ardhi sio usajili wa nyaraka mana tunaofanya sasa hivi mtakwenda kuuziana halafu utakwenda kusajili waraka husajili ardhi ndio mana mwengine anaweza akatoa waraka mwengine na mwengine akatoa hati nyengine. Lakini hili la utambuzi litafanya sasa ardhi ndio inayosajiliwa na itaondoa tatizo hili kwa kweli, tutailalamikia Mahkama ya Ardhi lakini tatizo hili kama hatujafikia kufanya utambuzi na usajili wa ardhi kwa kweli hili tatizo hata hizi Mahkama zote zikawa ndio Mahkama za Ardhi basi tatizo hili halitaondoka.
Kwa hivyo, mimi naamini kwamba serikali iko kwenye msingi au njia sahihi katika kulitatua tatizo hili ingawa itachukua muda lakini hatimaye tutafika katika kulipatia ufumbuzi.

Suala jengine ambalo Mhe. Hamza alitaka ufafanuzi na ambalo pia limezungumzwa kuhusu suala la lugha pengine hapa hapa ni kwamba ile lugha iliyotumika pengine mwengine inaweza ikampa shida, lakini sisi tunapendekeza

kwamba madhumuni yake ni hayo. Kwanza si Mjumbe mmoja isipokuwa ni Wajumbe watatu. Kwa hivyo ile lugha tunasema tutapendekeza turekebebishe iwe ni mmoja ambaye atateuliwa na waziri kutoka kila taasisi kati ya taasisi zinafuatazo kwa kushauriana na taasisi husika, halafu ndizo zifuate zile. Ninadhani itafahamika na kuondoa ule utatanishi ambao uliokuwepo.

Mhe. Spika, hoja nyengine ambayo alizungumzia Mhe. Hamza Hassan Juma lilikuwa ni suala la malalamiko juu ya sheria ya Mahakama ya Kazi. Ni kweli lakini ninadhani hapa tuzingatie pia kwamba kitu kikubwa ni kwamba hizi haki za wafanyakazi haziongozwi na ile Mahakama ya Kazi, zinaongozwa na sheria zenyewe za kazi, yaani ile sheria ya ajira na sheria ya mahusiano ya kazini (Empoloyment Act na Labour relation Act), mule muna haki ambazo zinatakiwa zichungwe na utaratibu wake umeekwa.

Miongoni mwa mambo ambayo yameekwa chini ya sheria ile ni kuekwa kitengo cha kusikiliza malalamiko ya wafanyakazi chini ya Wizara ya Kazi. Moja ni hilo. Lakini pia kuna kitengo au kuna bodi inayoitwa labour adviser board (Bodi ya Ushauri ya Kazi).

Ile bodi inamshauri waziri namna gani ya kusimamia vizuri sheria za kazi na ile bodi yenyewe imeundwa kwa pande zote tatu. Mna serikali mule ndani, mule waajiri na muna waajiriwa. Kwa hivyo ni fursa nzuri kwa waajiriwa malalamiko yao kuyapeleka pale kwa sababu wana wawakilishi wao na wakamshauri vizuri waziri namna gani ya kufanya marekebisho.

Baadae wao watakachofanya ni kutuletea sisi kwamba bwana sisi tunadhani kuna matatizo hapa tuweze kuyarekebiha. Lakini hizi taasisi zipo na pia kuna vyama vya wafanyakazi, navyo vina fursa kubwa kuweza haya kuyasimamia wakayapeleka serikalini, na ninaamini hasa kwa kupitia ile bodi ya ushauri wa kazi mambo haya yanaweza yakarekebishwa.

Lakini na jengine kuna utaratibu wanaita collective bargain, kwa kupigia collective bargain wafanyakazi wana fursa nyengine ya kurekebisha kushawazisha baadhi ya mambo ambayo yanajitokeza. Pengine hapa ni pahala pa kusema tu kwamba vyama vya wafanyakazi kama vitafanyakazi vizuri mambo mengi haya yanaweza yakaondoka. Lakini pamoja na hayo tunajua wajibu wa serikali na tutashirikiana na wizara inayohusika katika kuona yale matatizo ambayo yameonekana na yanahitaji kufanyiwa marekebisho tuweze kuyafanyia marekebisho.

Hoja nyengine iliyotolewa na Mhe. Ali Salim ambaye alizungumzia kuhusiana, kwanza kwamba kuna haja ya kuangalia maeneo mengine ili kumpunguzia kazi Mhe. Rais na hili lilizungumzwa na Waheshimiwa wengi, lakini hapa naomba kidogo nitoe ufafanuzi mdogo tu, kwamba kuna mambo mawili ni vizuri tuyafahamu katika suala hili.

Hawa wenyeviti wa hizi Mahakama tayari ni wanakuwa ni majaji ambao wameteuliwa na Rais, lakini kuna suala la pili kwamba ile kwenda kwa mwenyekiti, sisi ile tunasema si uteuzi ni kupangiwa kazi, kwamba tayari wewe umeshakuwa Jaji, anatakiwa mwenyekiti wa Mahakama hii ambayo ni sehemu ya Mahakama. Sasa kumpelekea Rais tena ndio ile kusema ni kama kuchukua tena mamlaka ya Mahakama, kwa sababu kazi ya kuwapangia kazi Majaji ni kazi ya Jaji Mkuu kwa kushauriana na Tume ya Utumishi ya Mahakama.

Kwa hivyo tulichorekebisha ni lile la kwamba Rais aendelee kufanya kazi yake ya kuteuwa Majaji kwa utaratibu ambao upo na umo ndani ya Katiba. Lakini haya ya kupangia kazi Majaji basi tuyarudishe kwao ambapo ni kwa Jaji Mkuu na Tume yake ya Utumishi ya Mahakama.

Jengine alichotaka Mhe. Ali Salim ni kwamba ni kwa nini tumesema kuwa Mahakama inaweza badala ya kusema tu itafanya tu, kama hii si amri ni kama ikipenda. Lakini kilichokusudiwa kikubwa ni kwamba ukishakusema unaweza, maana yake mtu umeshampa cheque. Kwa hivyo atakachopima yeye ni wakati gani hiyo ruhusa aitumie. Ni tofauti kama ukimwambia afanye kwa lazima utakuwa umempa amri kwamba lazima afanye, lakini unapomwambia anaweza ni kwamba maana yake umempa ruhusa kipimo chake na busara yake itategemea ni wakati gani ruhusa hiyo aitumie. Kwa hivyo hili linatumika na hakutokuwa na mgongano katika suala hili.

Lile suala la wajumbe kutoka Pemba na Unguja ninadhani limelieleza, Mhe. Mahmoud alitoa ombi la sheria mama ipatikane wakati tunapofanya marekebisho. Mhe. Spika, niseme kwamba tutajitahidi kadri itakavyowezekana lakini wakati mwengine tukumbuke kwamba hiyo sheria mama yenyewe inaweza kuwa ni kubwa sana, labda tutoe zile page na vifungu ambavyo vinarekebishwa, hilo naona halina tatizo na ninakubaliana na wewe tukiunganisha na ile

ya hoja ya Mhe. Salmin Awadh kwamba itarahisisha kufanya rejea. Kwa hivyo ni jambo ambalo tunalichukua na inshaallah tutalifanyia kazi.

Jengine ni kuhusiana na Mahakama Kuu kuweza kugawanywa katika vitengo kwamba hatua nzuri na ninadhani nimeeleza yale madhumuni yake. Labda kifungu cha 9 ulisema yale marekebisho ya lugha, ninadhani nimeyazungumza. Kuhusiana na lile suala la muundo wa mwanzo wa bodi, ninadhani pia nimefafanua.

Mhe. Salmin Awadh alitaka matrix itayarishwe. Naomba nikuahidi kwamba tutalifanyia kazi hilo na hasa sasa kwa sababu tutakuwa na uwezo wa kutoa muongozo zaidi kuhusiana na suala hili, na naomba nikuhakikishie kwamba tayari tunaandaa muongozo kuhusiana na miswada ili kuimarisha usimamizi wa miswada, bado kuna tatizo kwenye eneo hili lakini kwa kuongeza nguvu kazi katika afisi yetu na kuongeza umakini basi hili tutaweza kulifanya vizuri zaidi.

Lakini hoja ya pili aliyoizungumza ni kwamba marekebisho ya Mahakama ya Kazi, umeeleza yaliopo ambayo Waheshimiwa wengine pia wameeleza kuhusiana ilivyo na malalamiko yaliopo. Lakini ulitaka kujua kwamba kifungu cha 3 kinachofutwa kilikuwa kinasemaje na kwa nini kinafutwa na kuna mapungufu.

Ninadhani nimejaribu kukieleza kwamba kinachosema ni kuwa yule mwenyekiti wa ile Mahakama ambaye atatakiwa awe ni Jaji wa Mahakama Kuu atateuliwa na Rais...

Mhe. Spika; Waheshimiwa Wajumbe muliopo nje nikuombeni basi muingie ndani ili tumalize kazi hii baada ya muda mchache sana Mhe. Mwanasheria Mkuu atamaliza majumuisho. Kwa hivyo tuliopo nje Waheshimiwa Wajumbe tuingie ndani tumalize kazi hii. Mhe. Mwanasheria Mkuu endelea.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Kwa hivyo mapungufu yalikuwa ni hayo kwamba ile kazi ya kusema kuwa Jaji, kwanza labour tribunal ni sehemu ya Mahakama Kuu au ni divisheni ya Mahakama Kuu. Sasa nani akawe ndio mwenyekiti, tena isiwe kazi ya Rais, iwe ni kazi ya Mahakama ndio utaratibu unavyotakiwa, kwa sababu ile ni kumpangia kazi na Mahakama inawezekana ikatokea dharura yule hayupo mpaka urudi tena kwa Rais nao pia ni usumbufu. Lakini Jaji Mkuu anaweza akaseme aah! badala ya huyu basi utakwenda wewe kwa sababu lipo ndani ya mamlaka yake.

Kifungu cha 4 kodi za nyumba ulitaka ufafanuzi. Katika moja ya Mahakama au bodi za Kimahakama zilizoanzishwa muda mrefu ni bodi ya nyumba au ni bodi ya kudhibiti kodi za nyumba. Hii si kodi ile inayolipwa ya kodi kwa maana ya serikali, hii ni ile kodi anayolipa mpangaji kumlipa mwenye nyumba, yaani ni *rent*, ndio maana kwa kiingereza wanaita *rent restriction* board. Na hii haidhibiti tu zile kodi lakini inadhibiti haki ya mpangaji ndani ya nyumba na haki ya mwenye nyumba kwa mpangaji. Kwa mfano kutaka kuhamishwa, unaweza ukapata mpangaji akaja akakwambia bwana saa ishirini na nne uhame, lakini sheria hii imeekwa utaratibu ukitaka kumuhamisha mpangaji utaratibu ukoje na wewe matengenezo yepi kwa mfano, ni lazima yafanywe na mpangaji na yepi yafanywe na mwenye nyumba unless mumekubaliana vyengine kwenye mkataba.

Ni sheria iliyokuwa inalinda haki kwenye upangaji na wenye nyumba, lakini imeitwa tu ni rent restriction board lakini ukiisoma ina mambo mengi kwa kweli ya kuwasaidia hawa watu wawe na mahusiano mazuri kwa kweli.
Kifungu cha 7 kuhusiana na utanuzi wa Mahakama, naona ulikupa wasi wasi kwa kweli kidogo. Naomba nikuhakikishie Mhe. Salmin Awadh, ni utanuzi wa kawaida wa kuleta ufanisi, wa kuifanya Mahakama iweze kufanya kazi kitaalamu zaidi.

Dunia tunayokwenda nayo hivi sasa ina kitu kinaitwa specialization. Badala ya kuwa na ma-GP wengi hata madaktari, ninasikia kuna daktari wa sikio tu, kuna wa moyo, sasa na Mahakama nazo sasa hivi ndio kuna hiyo mahakama kama ya biashara, Mahakama ya Kazi. Hata hivyo Mahakama ya Ardhi kwa maana ya high court, kuna mahakama za kodi, kwa maana hizi kodi za serikali. Kwa hivyo sheria yetu ilikuwa bahati mbaya haijaeleza hiyo. Kwa hivyo sasa kwa sababu hizo haja zimeanza kujitokeza, ndio maana tukasema iruhusiwe ijitanue lakini ni utanuzi salama na ni utanuzi ambao ni wa kuongeza ufanisi.

Kuhusiana na ile kutokuwepo mjumbe kutoka Jumuiya ya mfanyabiashara katika bodi ya ZSTC nimeieleza sababu zake na mwelekeo wake, lakini mwisho ulimalizia ninakushukuru naona macho yako ni makali Mhe. Salmin Awadh ni sehemu ya sita iliyosema kwamba kurekebisha sheria ya bandari.

Ile sehemu baada ya kuandaa huu mswada ilikuwa na sheria ya bandari nayo iingie katika marekebisho mbali mbali. Lakini kutokana na mambo yaliyojitokeza mengine zaidi na umuhimu wa ile sheria ya bandari, tukataka Waheshimiwa Wajumbe mujitanue mupate nafasi ya kuweza kuizungumza kwa upana na urefu hii haya marekebisho ya sheria ya bandari. Kwa hivyo ndio maana tukaona tuitoe katika marekebisho mbali mbali na uwe mswada peke yake. Lakini bahati mbaya tulijua kuondoa mengine lakini ile ya madhumuni na sababu tukaisahau, kwa hivyo ilikuwa ni makosa ya kiuandishi. Na ninachukua ule wito wako kwamba na sheria nyengine nazo ziangaliwe, tutashirikiana na wenzangu tuweze kuziangalia.

Mhe. Hija Hassan Hija alisema vigezo vya kurekebisha sheria uliuliza. Vigezo vipo mbali mbali lakini ninachoweza kukwambia kwamba si kawaida kwa Mwanasheria Mkuu kumuendea waziri mwengine akamwambia bwana wee! Sheria yako hii ina tatizo irekebishe. Maana unasema anayevaa kitu ndiye anayejua kinapobana. Kwa hivyo kwa kawaida wao wanaleta mapendekezo.

Lakini tunachowahimiza ni kwamba tunawaambia jamani tunaandaa mswada wa marekebisho ya sheria mbali mbali, kuna mtu ana sheria yake ina tatizo basi wanatuletea tunayaagiza katika mswada. Lakini wamesikia wenzangu wote na sisi serikali pia tumesikia, tutaambizana tutajitahidi kulifanyia kazi suala hilo.

Ninashukuru sehemu kubwa uliyozungumzia ni kwamba kupongeza hii hatua iliyochukuliwa lakini ulitahadharisha kwamba tuwe makini na wengine pia walilizungumzia hili katika kuandaa hizi sheria, kwa sababu sheria hii ni ya karibuni na sasa hivi tunaifanyia marekebisho. Ni kweli hilo tulipitikiwa na tukasema basi tulifanyie marekebisho. Mwisho ulitoa wito wa sheria nyengine tuliziangalie, inshaallah tutaziangalia.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu mbali ya lile la mama Magreth Thatcher, kwa kweli ndio kwanza ninalisikia kutoka kwake, ni favourite wa wengi ambao wanapenda mambo yaende. Kwa hivyo ninaamini mara nyingi sifa hufa baada pengine mtu akishaondoka duniani, pengine wengine hivi sasa watatafuta vitabu vyake wasome.

Marekebisho ya kumuondoa Rais uwezo, ninadhani nimelieleza na hilo la kuchukua hatua nyengine, ninadhani juzi nimelieleza hapa kwamba ni suala ambalo linahitaji muelekeo wa jumla baada ya vipande vipande. Ninadhani hizo hatua zinachukuliwa lakini na huku tunakoelekea pengine tutakuwa na fursa ya kufanyia mapitio makubwa pengine kama sio Katiba ni kwenye sheria zetu, tutapata fursa hiyo ya kuangalia haya kwa upana wake.

Jengine alilizungumzia kuhusu marekebisho ya Sheria ya Mahakama ya Kazi. Ninadhani nimelieleza pia na zile taasis ambazo zipo za kupeleka malalamiko, naomba sana kwamba tuzitumie na ninaamini kwamba tunaweza tukapata tukaona kwamba zile sehemu zinazohitaji marekebisho katika sheria.

Lakini mengine mimi ninasema si sheria, wakati mwengine ni usimamizi. Kama kuna jambo kubwa tuliimarishe ni usimamizi wa sheria zetu na tutaona kwamba sheria zetu nyingi ni muhimu au bado zinafaa bado.

Ninashukuru kwa ule ufafanuzi uliotoa kwamba huu utanuzi aliokuwa Mhe. Salmin Awadh ninashukuru umesaidia kufafanua kwamba hizi zitakuwa ni divisheni za high court na ni muhimu kwa sasa hivi.

Mwisho ulitoa wito wa kwamba tuwe makini katika kupitisha sheria zetu, tumesikia na inshaallah tutalifanyia kazi.

Na mwisho Mhe. Abdalla Juma Abdalla ufafanuzi wa sehemu ya sita, ninadhani nimetoa majibu kwamba yalikuwa ni makosa ya uandishi, kwamba umepata elimu kuwa ulikuwa hujui kuwa Mahakama ya Nyumba ipo na tena ni muda mrefu kuliko Mahakama ya Kazi. Hii ilianza mwanzo zaidi.
Lile ambalo umetahadharisha kwamba jee tukiongeza mtu katika bodi haitongeza idadi, ninadhani nimelitolea ufafanuzi, kwamba kwa kweli tulichofanya tumepunguza mtu mmoja tu, kwa hivyo idadi itakuwa ni sawa pamoja na lile ambalo Waheshimiwa Wajumbe walilieleza ambalo bado tutakuwa tuna nafasi.

Mhe. Fatma ninakushukuru kwa kutuunga mkono katika marekebisho haya na uliuliza tu kwamba kodi za nyumba ni za aina gani, ninadhani nimezifafanua kwamba ilipoanza sheria hii ilikuwa ikitumika huko kwa Mhe. Jussa tu, maana huko ng'ambu kwa sheria za zamani zilikuwa zikijulikana kwamba ni hut, kuna zone ukijenga nyumba hata kama ni kibanda kinatambulika kama ni nyumba, lakini ukiingia kwenye zone ya ng'ambu hata ukijenga nyumba basi inajulikana ni kibanda na ilikuwa na sheria zake zikiitwa Hut Regulation, huku mjini kwa Mhe. Jussa ndio

ikitumika sheria ya nyumba, lakini sasa ninadhani zimeenea kila pahala. Kwa hivyo ninadhani sasa sheria inatumika kila pahala. Ninashukuru kwamba lile suala la lugha nimejaribu kulieleza.

Mhe. Spika, mwisho nikushukuru kwa fursa hii ya kajaribu kutoa ufafanuzi lakini na pia niwashukuru Waheshimiwa Wajumbe nimejaribu kutoa ufafanuzi, lakini na pia mumetupa mawaidha, maoni tunayachukua na hatutayakalia lakini tutayafanyia kazi inshaallah ili kupata mafanikio.
Mhe. Spika, baada ya kusema hayo naomba kutoa hoja.

(Hoja imetolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

KAMATI YA KUTUNGA SHERIA

Sehemu ya Kwanza

Utangulizi

Kifungu 1 Jina fupi na kuanza kutumika

Sehemu ya Pili

Marekebisho ya Sheria ya Mahakama ya Kazi Nam.2. 1994

Kifungu 2 Kusomwa
Kifungu 3

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, kwanza naomba nimshukuru Mhe. Mwanasheria Mkuu kwa ufafanuzi alioutoa kuhusiana na hoja mbali mbali tulizozitoa. Awali sikuwa na hoja lakini baada ya ufafanuzi wake kidogo nimeghadhibika kidogo kumuuliza swali dogo ili tuelewane katika kupitisha kifungu hiki.

Mhe. Mwenyekiti, kinasomeka na ninaomba nikinukuu, 14 (1) “Mwenyekiti wa Mahakama ambaye atateuliwa na na Jaji Mkuu kwa ushauri wa Waziri na baada ya kushauriana na Tume ya Utumishi ya Mahakama kutoka miongoni mwa Majaji wa Mahakama Kuu”.

Sasa awali kabla ya ufafanuzi wa Mwanasheria Mkuu sikuona tatizo wa haya maneno “kwa ushauri wa Waziri”, lakini baada ya ufafanuzi wa Mwanasheria Mkuu nilivyomfahamu amesema kwamba sababu hasa alipokuwa akitueleweshe kuwa tusipochanganya na yale madaraka ya Rais kwa ujumla wake akasema haya ni kuwapangia kazi Majaji ambao tayari wameshateuliwa na Rais ambao wapo katika Mahakama Kuu na ni suala la kuwapangia kazi mamlaka ya Jaji Mkuu.

Sasa baada ya ufafanuzi huo nimekuwa ninajiuliza na ninaomba ufafanuzi wake kwamba ikiwa haya ni madaraka ya Jaji Mkuu katika kusimamia utendaji wa Mahakama na kuwapangia Majaji ambao tayari wameshateuliwa na Rais.

Tunamuhusishane waziri katika kumpangia Jaji ambaye ameshateuliwa na Rais kwamba Jaji yupi akaongoze divisheni ya Mahakama ya Kazi.]
Nilikuwa ninaomba ufafanuzi wa Mwanasheria Mkuu kwa sababu ninahisi mimi pengine itawezekana kwamba hawa walalamikiwa katika hizo kesi inaweza ikawa ni waziri mwenyewe. Sasa anapokuwa yeye pia anashirikishwa katika ushauri wa Jaji gani akaongoze divisheni hii, kidogo inanipa mashaka na pengine inaweza kupelekea mgongano wa maslahi (conflict interest). Nilikuwa naomba ufafanuzi Mhe. Mwenyekiti, katika hili. Ninashukuru.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nikubaliane na concern ya Mhe. Jussa hasa kwa maneno yalivyotumika. Lakini establish practice au utaratibu ambao umezoeleka kwanza waziri hahusiki kusema kwamba Jaji yupi apangiwe katika ile Mahakama ya Kazi.

Lakini mara nyingi ushauri unakuwa kwa upungufu uliopo kwa matatizo ambayo yametokea katika usimamizi wa masuala au mashauri yaliopo katika ile Mahakama, mara nyingi yeye Waziri ndiye anakuwa anajua, na hapa ni Waziri anayeshughulikia masuala ya kazi na sio Waziri wa sheria.
Kwa hivyo kwa kawaida yeye ndiye anashauriana na na Jaji Mkuu kuhusiana na utendaji wa ile Mahakama na mambo ambayo yanajitokeza, kwa sababu mara nyingi wao ndio watumiaji wakubwa na malalamiko mengi yanakwenda kwa Waziri anayehusika na masuala ya kazi.

Kwa hivyo ndio maana utaratibu uliozoeleka ni kwamba katika hili Jaji Mkuu huwa anashauriana na Waziri kuhusiana na ama haja ya kuwepo mwenyekiti au utendaji wa ile Mahakama na baadae Jaji Mkuu mwenyewe ndio hufanya maamuzi kulingana na yale ambayo yanajitokeza katika ule utendaji wa Mahakama.

Lakini kuwepo ni suala la kiutawala tu lakini halihusishi Waziri muhusika kuingilia katika uteuzi wa hawa Majaji.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, pamoja na kuwa mara nyingi Mhe. Mwanasheria Mkuu anapotufafanulia mambo hapa hasa yanapohusu utanuzi anakuwa anafahamika sana. Lakini katika hili naona utanuzi wake umetuhangaisha zaidi baada ya kutusaidia.
Mhe. Mwenyekiti, kwa hivi kilivyokaa mimi kinanipa mashaka katika kukipitisha hapa hiki kifungu na ninaona kwa maelezo yake kama vile inaonekana kwamba kinampa madaraka Waziri wa Kazi kwamba, na mimi nilifahamu hivyo hivyo by the way Mhe. Mwenyekiti, ni Waziri wa Kazi na sio wa Katiba na Sheria kwamba anashauriwa katika kumteuwa kwa sababu hiki kifungu Mhe. Mwenyekiti, kinasomeka kwamba kifungu cha 14 (1) cha sheria mama kinafutwa hicho kilichoopo na kuekwa badala yake kifungu kipya kama ifuatavyo, sasa hicho kipya kinasomeka 14 (1) "Mwenyekiti wa Mahakama ambaye atateuliwa na Jaji Mkuu kwa ushauri wa Waziri na baada ya kushauriana na Tume ya Utumishi wa Mahakama kutoka miongoni mwa Jaji wa Mahakama Kuu".

Na nikisoma kwa kiingereza ambacho ninaamini Mhe. Mwanasheria Mkuu mtaalamu zaidi kuliko hata hiki Kiswahili. Kiingereza Mhe. Mwenyekiti, ndio inaonesha hasa makusudio haidhuru ninajua kwamba dhamira ya watunga sheria itatafsiriwa katika Kiswahili kwa sababu ndio nyaraka za Baraza la Wawakilshi, lakini tunasoma pamoja na ndio maana tunapewa pamoja mswada wa kiingereza na tunapewa hii extraordinary; mswada wa Kiswahili na extraordinary ya kiingereza.

Mhe. Mwenyekiti, wa kiingereza unasomeka hivi kwenye ukurasa wa 312 wa kile kijalizo katika Government Gazette, kinasema *14 (1)* "*The Chairman of Court who shall be appointed by the Chief Justice upon adise by the Minister after the consultation with the Judiciary Service Commission from among Judges of High Court*".
Sasa Mhe. Mwenyekiti, ndio maana nikasema kidogo kinanipa mashaka. Kwa hivyo, ama tuyaondoshe maneno kwa ushauri wangu, kwa ushauri wa Waziri au Mhe. Mwanasheria Mkuu kama haraka anaweza kutushawishi akakirekebisha kwa lugha yake yeye, kwa maneno ambayo yatafanya yalete tafsiri hiyo iliyokusudiwa, sio tafsiri ya kumshauri Jaji Mkuu iwe Jaji gani aende akaongoze mahakama ya kazi, naomba nikae lakini tuliridhishe hili ili tupitishe sheria ambayo inakwenda vizuri na misingi ya utawala bora.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti, nimemuelewa sana Mhe. Jussa. Kwanza kuna msingi ule wa kikatiba wa mamlaka ya Mhe. Jaji Mkuu na Tume ya Utumishi ya Mahakama kupangia kazi majaji. Hili la kushauriwa au kushauriana ni suala la kiutawala, sasa kama CJ ata-*abdicate* mamlaka yake aliyopewa na katiba, kwa sababu tu ya kuheshimu ushauri hilo litakuwa ni suala la khulka, lakini sio suala la kisheria kusema ukweli. Kama tunaona kuwa hilo linaweza likamfanya Jaji Mkuu aachiwe huru wakati uhuru ule kapewa na katiba na sheria hii imetoa *mandate* kwake na tume yake ya utumishi ya mahakama. Kama tunaona hilo lita-*prejudice* haki za watu, mimi wala sina shida kuondoa jambo ambalo tunaona lina athari ya kukwaza haki za watu kusema ukweli.

Mhe. Spika, mimi kwa nafsi yangu kusema kweli, dhamira yangu hainifanyi kuona kwamba hili linaweza likakwaza utendaji wa Jaji Mkuu, kwa sababu hapa kifungu kiko wazi kwamba yeye ndio atateua. Lakini Waziri kazi yake ni kiutawala kushauriwa kwa sababu ya mazingira yenyewe ile mahakama inavyofanya kazi, kwamba iko sehemu ya kwao. Hii imetoka mbali, mwanzo alikuwa akimteua Waziri hasa huyu Mwenyekiti, lakini baadae tena imekwenda ndio mpaka tukafikia hapa tulipofika. Kwa hivyo, mimi kusema kweli kama hili tunaona litakwaza haki za watu, basi sina kabisa tatizo la kuyaondoa haya maneno, lakini najua msingi chini ya katiba ni mamlaka ya Jaji Mkuu na tume yake ya utumishi wa mahakama.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, mimi nashawishika kwamba kwa kutambua dhamira njema ya Mhe. Mwanasheria Mkuu katika kufanya jambo lolote ambalo hata kwa namna ya mbali kabisa linaweza likatafsiriwa kuasi haki za watu, basi mimi napendekeza haya maneno kwa ushauri wa Waziri tuyaondoe.

Mhe. Mwenyekiti, tusitazame watu, inawezekana leo kukawa na Jaji Mkuu anayejiamini akatumia misingi ya katiba akasimamia haki yake. Inawezekana leo kukawa na Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wananchi Kiuchumi na Ushirika kama alivyokuwa Maalim Haroun hapo akaheshimu misingi hii. Lakini kesho na kesho kutwa unaweza kuwa na watu wengine katika nafasi zote hizo mbili ambao wanaweza wasisimamie ile misingi ambayo tunaitarajia wala wasione kuwa wana nguvu na ujasiri wa kutumia katiba zilizowekwa.

Mhe. Mwenyekiti, iko mifano sitaki kwenda katika vifungu hivyo, kwa sababu hatujadili sasa hivi, tunapitisha vifungu. Mimi nilikuwa nasema tu kwamba kama Mhe. Mwanasheria Mkuu ataridhika, basi haya maneno kwa ushauri wa Waziri tuyaondoe. Kwa sababu kama nilivyosema, ilivyokuwa kiutawala bado haiondoshi kutumia taratibu za kiutawala kushauriana, lakini tusiingize ndani ya sheria.

Kwa hivyo, nilikuwa naomba Mhe. Mwenyekiti, kwamba ushauri wangu Mhe. Mwanasheria Mkuu tukubali kuwa maneno kwa ushauri wa Waziri tuyaondoe na badala yake isomeke kama vile vifungu vingine vilivyokuwa vimetajwa kule, kuwa moja kwa moja ni Jaji Mkuu na tume yake ya utumishi basi tuiache hivyo hivyo Mhe. Mwenyekiti, huo ni ushauri wangu, ahsante.

Mhe. Mwenyekiti: Hivi itakuwa amekiuka wajibu wake au madaraka yake Jaji Mkuu, kama atakuwa anapata *advice silently*. Hapa nakusudia kwamba kama atachukua ushauri bila ya kuwemo ndani ya sheria hii kutoka kwa Waziri, itakuwa amekiuka madaraka yake. Nadhani itakuwa hajakiuka, basi kama ni hivyo nadhani Mhe. Mwanasheria Mkuu hebu zingatia hili la kuondoa maneno hayo.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyotangulia kusema kwamba najua mtu mwenye busara hata jambo lenye mamlaka yake anaweza akatafuta tu, maana kichwa kimoja sio sawa na viwili. Inawezekana kuna mambo yeye hayajui, lakini ushauri wa mwenzake ukamsaidia. Lakini kwa haya maneno kuyaondoa, mimi naona hayaifanyi sheria hii isitekelezeke, kwa hivyo kuyaondoa mimi naona ni sahihi ili iridhishe nyoyo zetu Wajumbe tunaopitisha sheria hii.

Kifungu 3 Kufutwa Kifungu cha 14(1) na kuwekwa kifungu kipya pamoja na marekebisho yake.

Mhe. Mwenyekiti: Marekebisho ndio hayo kuondoa kwa ushauri wa Waziri, hayo yanaondoka. Na tukiondoa hapa tunaondoa na kule kwenye Kiingereza vile vile. Kimekubaliwa.

Sehemu ya Tatu

Marekebisho ya Sheria ya Udhibiti wa Kodi za Nyumba
Marekebisho Nam. 3 ya mwaka 1987

Kifungu 4 Kusomwa.
Kifungu 5 Marekebisho ya Kifungu cha 6(1) pamoja na marekebisho yake.

Sehemu ya Nne

Marekebisho ya Sheria ya Mahakama Kuu
Nam. 2 ya mwaka 1985

Kifungu 6 Kusomwa.
Kifungu 7 Marekebisho ya

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, nilipokuwa nachangia kifungu hiki nilitaka kidogo Mhe. Mwanasheria Mkuu anielimishe kwamba lengo la kufanywa marekebisho haya ni kuipa mamlaka mahakama kujitanua au kuanzisha divisheni. Nikasema kwamba hivi karibuni nilisikia Jaji Mkuu akizindua mahakama ya watoto kama ni divisheni ya mahakama kuu, kwa hivyo mahakama kuu ile divisheni ya watoto imeanzishwa mwanzo kabla ya kuja hii sheria. Kwa hivyo, nataka aniridhishe tu ilikuwa ni sahihi au.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti, kwanza niombe radhi kwa Mhe. Hija Hassan sikulidharau hilo, lakini kusema kweli sikuliona wakati napitia kwa haraka haraka. Mhe. Mwenyekiti ile mahakama ya watoto kuna sheria yake maalum ya kuanzisha mahakama ya watoto, ambayo tunaita ni *Juvenile Court*. Mapendekezo mengi yalikuja namna gani ya kuifanya ile mahakama ya watoto iwe ya kisasa. Kwa hivyo, siku nyingi ipo kusema kweli na imekuwa ikifanya kazi, pale wanapelekwa washtakiwa ambao ni chini ya ule umri wa miaka 18 wanaposhtakiwa.

Kwa hivyo, mahakama hii ilikuwepo, pia kwa upande mwengine mahakama sasa imepata vifaa vya kisasa vya kuweza, kwanza inapotokea mahakama ile, lakini inapotokea pia mahakamani shahidi ni mtoto, hasa katika hizi kesi za unyanyasaji wa watoto. Kwa hivyo, ile mahakama ina huduma na vifaa ambavyo vitamuwezesha mtoto kutoa ushahidi bila ya kupata shida, bila ya kuogopa na bila ya kuona tabu. Kwa hivyo, kilichowekwa pale ni huduma kwa mahakama ambayo tayari ipo na kwa utaratibu ambao upo. Hili linaloanzishwa hapa ni suala jengine ambalo pengine mahakama nyengine zitakuja hapo baadae. Nilitaka kusema hayo tu Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, nashukuru tuendelee.

Kifungu 7 Marekebisho ya Kifungu cha 3(1).

Sehemu ya Tano

Marekebisho ya Sheria ya Shirika la Biashara ya Taifa
Nam. 11 ya mwaka 2011

Kifungu 8 Kusomwa.
Kifungu 9 Kufutwa Kifungu

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Ahsante Mhe. Mwenyekiti. Mhe. Mwenyekiti, kwa jumla sina tatizo na marekebisho yaliyofanywa na baada ya mjadala na ufafanuzi wa Mwanasheria Mkuu umetuweka pahala pazuri, na kwa sababu Kamati pia walirekebisha. Kwa sababu yule mjumbe mmoja wa jumuia ya wafanyabiashara wenye viwanda na wakulima Zanzibar alikuwa ameachwa, ameingizwa. Lakini nilikuwa nataka kutahadharisha tu, ndio maana nimenyanyuka na hili labda pia ni zinduo jengine la watu wetu wanapotutayarishia hii miswada katika magazeti ya serikali na vijalizo vyake, kwamba Mhe. Mwenyekiti, ukisoma ya Kiingereza bado yale marekebisho yaliyofanywa yanawataja wajumbe wa bodi kama walivyokuwa katika hiyo sheria ambayo tumesema kwamba ilikuwa na matatizo.

Kwa hivyo, nambari ya kirumi (v) inayotaja mjumbe kutoka *police officer* hii ya Kiingereza. Sasa nilikuwa nimenyanyuka kutahadharisha tu kwamba mara nyengine sijui watendaji wetu wanapokuja kufanya mjumuiko wa marekebisho yote, huwa wanatumia ipi. Najua kama nilivyosema kwamba kikatiba na kanuni zetu tunazotumia hasa kwa muongozo ni wa Kiswahili na ndio maana hapa tunaotumia katika kupitisha vifungu. Katika Kiingereza nilikuwa nataka kutahadharisha tu kwamba bado imetamka hiyo, wajumbe ukiwasoma ni wale ambao tumetaka tuwarekebishe na wametajwa vile vile.
Kwa hivyo, nilikuwa nataka nilitaje, lakini vile vile imezindua kuwa tunapoandaa hivi vitu tuwe waangalifu zaidi. Kwa sababu kwa mfano mdogo tu Mhe. Mwenyekiti, lile ambalo wajumbe wengi wanazungumzia la madhumuni na sababu kwamba lilifika kujumuisha sehemu ya sita ambayo haimo humu, inahusiana na mswada wa marekebisho ya sheria ya bandari ambayo tuliijadili peke yake. Hata ukija katika Kiingereza bado pia katika madhumuni na sababu kuna maelezo kuhusiana na sehemu ya sita ambayo pia haipo. Kwa hivyo, inaonekana kwamba mara nyengine watendaji wetu wanakuwa hawako waangalifu na hatutegemei mambo kama haya kwamba yote lazima Waziri na mtu kama Mwanasheria Mkuu wawe wanayapitia wao, kwa hivyo nadhani iwe ni zinduo kwetu kwamba tuwe makini.

Mhe. Spika, kama nilivyosema zaidi nilitaka kutahadharisha katika hiki kifungu cha 9, tukisoma kwa Kiingereza bado kunatamkwa *police officer* ambayo tumesema kwamba inatakiwa mjumbe wake ndio aondoke. Baada ya marekebisho hayo Mhe. Mwenyekiti, nasema, nadhani tumeridhika na ufafanuzi wa Mhe. Mwanasheria Mkuu na tukichukulia kwamba *record* sahihi ni yale aliyofafanua kwamba wajumbe ni wale aliowataja yeye. Nadhani tutakuwa tuko sahihi Mhe. Mwenyekiti, nadhani tuendelee, ahsante.

Kifungu 9

Mhe. Fatma Mbarouk Said: Kifungu hiki nambari 9 napenda nikisome, kimesema kwamba kifungu kidogo (2) cha kifungu cha 13 cha sheria mama kinafutwa na kuwekwa badala yake kifungu kipya kama ifuatavyo.

(a) Bodi itakuwa na Mwenyekiti ambaye atateuliwa na Rais
(b) Mkurugenzi mwendeshaji na mjumbe mmoja ambaye atateuliwa na Waziri.

Lakini hapa Mkurugenzi Mwendeshaji, huko mbele kuna na, lakini mimi naona kama ni kiunganishi. Hapa haikutajwa kwamba huyu Mkurugenzi Mwendeshaji atateuliwa na nani.

Vile vile kifungu (c) nilisema kwamba mjumbe mmoja ambaye atateuliwa na Waziri miongoni mwa kila taasisi katika taasisi zifuatazo. Nilitoa pendekezo kwamba mjumbe mmoja mmoja ambaye atateuliwa na Waziri miongoni mwa taasisi. Lakini hata hivyo, hapa taasisi nahisi labda ingekuwa tamu zaidi, labda tungesema miongoni mwa Wizara inayohusika na biashara, wizara inayohusika na fedha na wizara inayohusika na kilimo. Nahisi pawe na marekebisho hayo.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nitangulie kwa kumuomba radhi Mhe. Fatma ni kweli alizungumzia lile suala la Mkurugenzi Mwendeshaji, kwamba hakutajwa anayemteua na mimi sikulitolea ufafanuzi. Lakini Mkurugenzi Mtendaji ukisoma sheria yenyewe ya ZSTC vifungu vyengine inataja atateuliwa na nani na kwenye hii bodi anaingia yeye kama ni X *office member*. Kwa hivyo, moja kwa moja hakuna haja tena ya kusema nani anayemteua kwa sababu yeye hateuliwi anaingia kwa nafasi yake.

Kuhusu lile la ile lugha iliyotumika pale, Mhe. Mwenyekiti, ni kwa sababu tu kwamba katika uandishi wa kila kitu kuna ule utamaduni wake. Sasa lugha aliyoisema Mhe. Fatma ni kweli ni maridhawa na ni tamu kama alivyosema mwenyewe, lakini ni ule utamaduni tu wa kiuandishi.

Mhe. Mwenyekiti, naomba nimkumbushe Mhe. Fatma kwamba sheria zote hizi huwa zinasomeka na sheria nambari 7 ya mwaka 1984, sheria ya tafsiri ya sheria ambayo lile lenye utata katika kutafsiri sheria ile inakusaidia katika kupata tafsiri ya hii sheria ilivyokusudiwa. Sasa kwa uandishi hapa kwa sababu tumesema kwamba ni mjumbe mmoja kutoka kila taasisi hii, halafu zikatajwa ni wazi kwamba haiwezekani kuwa aliyekusudiwa ni mjumbe mmoja, isipokuwa ni mjumbe mmoja kutoka kwenye kila hii taasisi kwa maana hiyo ni mjumbe mmoja mmoja kama alivyosema yeye. Lakini kwenye uandishi utamaduni ni ile kuandika kwamba mjumbe mmoja kutoka kila taasisi hizi zilizotajwa na bila shaka itaweza kufahamika. Kwa hivyo, nakubaliana na lugha yake ni nzuri, lakini ningemuomba sana kwamba nyinyi mnaotunga sheria mna lugha yenu mnayotumia katika maandishi. Vile vile na hii ndio ambayo imezoeleka Mhe. Mwenyekiti, na ninaamini kwamba inafahamika.

Mhe. Fatma Mbarouk Said: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, namkubalia.
Kifungu 9 Kufutwa kifungu cha 13(2) na kuwekwa kifungu kipya

(Baraza lilirudia)

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Spika, ilivyokuwa Kamati ya Kutunga Sheria iliupitia mswada wangu kifungu kwa kifungu na kuukubali pamoja na marekebisho yake. Sasa naliomba Baraza lako tukufu liukubali. Naomba kutoa hoja.

Mhe. Waziri wa Kilimo na Maliasili: Mhe. Spika, naafiki.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, niwahoji basi wale wanaokubaliana na mswada huu pamoja na marekebisho yake wanyanyue mikono. Wanaokataa. Waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)
Mswada wa Sheria ya Marekebisho ya
Sheria Mbali Mbali ya mwaka 2013

(Kusomwa kwa mara ya tatu)

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Spika, naomba kutoa hoja kwamba Mswada wa Sheria ya Kurekebisha Sheria Mbali Mbali ya Mwaka 2013, usomwe kwa mara ya tatu. Naomba kutoa hoja.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Spika, naafiki.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, niwahoji wanaokubaliana na mswada katika kusomwa mara ya tatu wanyanyue mikono. Wanaokataa. Waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)
(Mswada wa sheria ulisomwa mara ya tatu na kupitishwa)

Mhe. Spika: Kuna shughuli nyengine Katibu. Muongozo wa Spika, Mhe. Ismail Jussa Ladhu.

Muongozo

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Spika, naomba nitumie kanuni ya 79(1) kuomba muongozo wako au wa serikali, kikanuni ni wako. Kanuni ya 79(1) Mhe. Spika, inasema
Kanuni ya 79(1)

> "Kila mswada wa serikali utatangazwa katika gazeti la serikali katika toleo angalau moja, lakini iwapo matoleo yatazidi moja kuwe na kitambo kisichopungua siku saba kati ya toleo la kwanza na la pili"

Naomba nitumie kanuni hii Mhe. Spika, kuomba muongozo wako, kwa sababu kesho tukijaaliwa tunategemea kujadili mswada wa mwisho unaohusu mahakama ya biashara. Sasa tuligaiwa katika kikao kilichopita gazeti rasmi la serikali, ambapo mswada huu ulikuwemo kuanzia ukurasa 364 mpaka 378 na bila shaka tulikuwa na muda mrefu tukiufanyia kazi. Sasa leo hii hapa mimi na wenzangu tumepewa gazeti jengine au nakala ya gazeti jengine la gazeti la serikali ambalo tarehe yake ni ile ile 24 Disemba kama lililopita, lakini ndani yake kuna mswada mmoja tu ambao ni huo huo wa mswada wa sheria ya kuanzisha mahakama ya biashara Zanzibar na mambo mengine yanayohusiana na hayo.

Kwa hivyo, nilikuwa naomba muongozo wako au ikiwa kupitia kwako Waziri atusaidie, ili tusiende kujihangaisha bure kwenda kuupitia tena, kitu ambacho mimi nimeshakipitia, atwambie kama kuna marekebisho katika hii tuliyogaiwa leo, tujue tukafanye tena hiyo kazi. La kama ni ule ule basi tujue tunatumia gazeti rasmi la serikali ambalo tulipewa kipindi kilichopita ambayo pia ilikuwa na miswada mingine. Mhe. Spika, nilikuwa naomba muongozo wako, ahsante.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Spika, ni kweli tarehe 24 Disemba lilitoka gazeti la serikali na mswada huo wa sheria ya mahakama ya biashara ulitolewa. Mhe. Spika, kwa mujibu wa utaratibu mswada huo pamoja na miswada mingine, ilipelekwa katika Kamati mbali mbali na kamati iliyopelekwa ni Kamati ya Katiba na Sheria. Mhe. Mjumbe alikuwa ni mjumbe wa Kamati ya Katiba na Sheria.

Mhe. Spika, baada ya kupelekwa katika Kamati ya Katiba na Sheria, wakaujadili mswada huu kwa kirefu sana, wakatoa makosa mengi ya uandishi, yaani *printing errors.* Sasa wao wakaelekeza kwamba uwe *reprinted*, yaani yale makosa yasahihishwe lakini uandikwe vizuri. Sasa kilichofanywa ni *reprinting* ya sheria hiyo, ni mswada ule ule lakini yale makosa ya ku-*print* maneno madogo madogo, yale ndio yote yamerekebishwa yametiwa katika mswada huu.

Kwa hivyo mswada huu uliogaiwa leo ni sawa sawa na ule wa tarehe 24, isipokuwa yale makosa ambayo wali-*direct* wao wenyewe Kamati ya Katiba na Sheria, kwamba uwe *reprinted* ili ukae vizuri, ndivyo tulivyofanya kwa maagizo yao. Mhe. Spika, nakushukuru.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Spika, kwanza nashukuru kwa ufafanuzi huo wa Waziri, ili tuelewane vizuri na tukija kesho tuwe tumekuja vizuri. Kama nimemfahamu vizuri, kwa sababu hapa tumepewa huo, lakini pia tumepewa na yale marekebisho ambayo yana saini yake ambayo yalikuwa yametambua yale marekebisho yaliyokuwa yamependekezwa na Kamati. Kwa hivyo, kama nimemfahamu vizuri ni kwamba haya ambayo tumegaiwa yakiwa na saini yake kama ni marekebisho ya Kamati yatakuwa tayari yote yamo humu, kwa hivyo mtu

akiwa amesoma waraka au nakala hii rasmi tuliyopewa leo, itakuwa haina haja tena ya kufanya marejeo kwa hii, kwa sababu marekebisho haya yatakuwa tayari yamo humu. Kwa hivyo, nilikuwa naomba hilo la pili liwekwe sawa ili tukichangia kesho tusipate tabu, huwa tunafanya *cross reference* katika nyaraka tofauti. Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Spika, kwa kuwarahisishia Wajumbe ndio maana tukafanya *reprinting*. Kwa hivyo, yale masahihisho ambayo nimetia saini yangu yote yamo katika mswada tulou-*reprint.* Kwa hivyo, haina haja tena ya kusoma yale marekebisho ambayo Kamati ya katiba na sheria iliyaelekeza, yote yamo katika mswada ambao umetolewa.

Mhe. Spika: Nafikiri kwa maelezo yaliyotoka na ufafanuzi uliotolewa, hii ni kurahisisha hata uchangiaji. Unajua wakati mwengine kama kuna marekebisho yako mengi kidogo, huwa Waheshimiwa Wajumbe wanashindwa kufanya rejea na akawa anazungumza jambo ambalo tayari limerekebishwa ndani ya Kamati.

Sasa kuondoa tatizo hilo na ili kuweza kufanya shughuli hiyo iende vizuri na isilete tatizo kwa Waheshimiwa Wajumbe wakati wa kuchangia, basi marekebisho yale yamekuwa ni *cooperate* katika huu mswada uliokuwa *reprinted*, nafikiri ndio hivyo. Tunashukuru.

Waheshimiwa Wajumbe, basi baada ya kazi hiyo nzuri mliyoifanya, nichukue nafasi hii kuwashukuru kwa mashirikiano makubwa ambayo mmeyatoa katika kufanikisha shughuli zetu. Kwa kuwa hakuna shughuli nyengine kwa leo, basi moja kwa moja niakhirishe kikao hiki mpaka kesho tarehe 09/04/2013 saa tatu barabara za asubuhi.

(Saa 1:35 usiku Baraza liliakhirishwa mpaka tarehe 09/04/2013
Saa 3:00 za asubuhi)